
# Fasihi ya Kiswahili kwa Shule za Sekondari

## Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano




Taasisi ya Elimu Tanzania

# Fasihi ya Kiswahili
## kwa Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi
### Kidato cha Tano



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1525

Jina la Chapisho: Fasihi ya Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9912-753-02-0

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 27 Mei 2024 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Tano katika Ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Mihtasari wa mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE READING ONLY

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2024

ISBN: 978-9912-753-02-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168/ +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE READING ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya vielelezo .......... vii

Vifupisho .......... viii

Shukurani .......... ix

Dibaji .......... x

Sura ya Kwanza: Dhana na chimbuko la fasihi .......... 1

Dhana ya fasihi .......... 1

Mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya fasihi .......... 2

Nadharia za chimbuko la fasihi .......... 3

Sura ya Pili: Fasihi simulizi na fasihi andishi .......... 6

Tanzu na vipera vya fasihi simulizi .......... 6

Tanzu na vipera vya fasihi andishi .......... 28

Uhusiano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi .......... 56

Mchango wa fasihi simulizi katika maendeleo ya fasihi andishi .......... 58

Athari za sayansi na teknolojia katika maendeleo ya fasihi simulizi na fasihi andishi .......... 59

FOR ONLINE READING ONLY

Mchango wa fasihi simulizi na fasihi andishi katika maendeleo ya jamii ........ 60

**Sura ya Tatu: Kutathmini kazi za fasihi** ........ 64

Mitazamo kuhusu fani na maudhui ........ 64

Uhusiano wa fani na maudhui katika kazi za fasihi ........ 66

Dhima za vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi ........ 66

Nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi ........ 68

Uchambuzi wa nadharia teule za uhakiki wa kazi za fasihi ........ 69

Kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia nadharia za kifasihi ........ 76

Kutathmini mchango wa nadharia teule za uhakiki wa kazi za fasihi katika maendeleo ya ushairi na tamthiliya ........ 88

**Sura ya Nne: Maadili katika fasihi** ........ 91

Maadili katika nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya ........ 91

Ulinganisho wa maadili yaliyomo katika kazi za fasihi na imani za jamii ........ 98

Mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya ........ 102

Uhusiano wa mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na

FOR ONLINE READING ONLY

tamthiliya na matendo ya jamii ........................................ 107

Athari za kiimani na kimtazamo katika bongo fleva
zinavyojidhihirisha katika jamii ........................................ 112

**Sura ya Tano: Ujumi katika kazi za fasihi** ........................................ 116

Ujenzi wa ujumi katika kazi za fasihi ........................................ 116

Uchambuzi wa mbinu zilizotumika kujenga ujumi
katika kazi za fasihi ........................................ 118

Maana na matumizi ya lugha katika matini za fasihi ........................................ 124

Mbinu za kifasihi zinavyoathiri kupatikana kwa maana
katika kazi za fasihi ........................................ 130

Misingi ya ujenzi wa hoja zenye mantiki na ushawishi ........................................ 133

Kutathmini kazi za fasihi kwa kutumia misingi ya ujenzi
wa hoja zenye mantiki na ushawishi ........................................ 134

Kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi kwa kutumia
maarifa ya kifasihi ........................................ 136

**Sura ya Sita: Kubuni kazi changamani za fasihi** ........................................ 142

Miktadha ya utunzi wa kazi changamani za fasihi ........................................ 142

Fursa zinazotokana na kazi za kifasihi ........................................ 145

FOR ONLINE READING ONLY

Mchango wa TEHAMA katika kukuza fursa za utunzaji, usambazaji, usomaji na uuzaji wa kazi za fasihi ........ 148

Hatua za utunzi wa kazi za fasihi ........ 149

Kanuni za kutunga maigizo, mashairi na hadithi za watoto ........ 153

**Faharasa** ........ 160

**Bibliografia** ........ 166

FOR ONLINE READING ONLY

# Orodha ya vielelezo

**Kielelezo cha 2.1:** *Tanzu na Vipera vya Fasihi Simulizi*

**Kielelezo cha 2.2:** *Tanzu na Vipera vya Fasihi Andishi*

FOR ONLINE READING ONLY

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| **DUP** | Dar es Salaam University Press |
| **EAEP** | East African Education Publishers |
| **EALB** | East African Literature Bureau |
| **EAPH** | East Africa Publishing House |
| **EPD** | Educational Publishers and Distributors Ltd. |
| **ITV** | Independent Television |
| **KAUTTU** | Kampuni ya Utamaduni Tafsiri na Uchapishaji |
| **Kur.** | Kurasa |
| **Mf.** | Mfasiri |
| **Mh.** | Mhariri |
| **OUP** | Oxford University Press |
| **TATAKI** | Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili |
| **TBC** | Tanzania Broadcasting Corporation |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **TPH** | Tanzania Publishing House |
| **UKUTA** | Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania |
| **Wah.** | Wahariri |

FOR ONLINE READING ONLY

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali zilizoshiriki kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Mtakatifu John's (SJUT) na Chuo Kikuu Mzumbe (MU). Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Prof. Fikeni E.M.K. Senkoro, Dkt. Athumani S. Ponera, Dkt Adria N. Fuluge, Bw. Jailan M. Hafidh, Bi. Asia M. Akaro, Bi. Janeth G. Joseph, na Bi. Monica W. Manyanga.

**Wahariri:** Prof. Kulikoyela Kahigi, Dkt. Angelus J. Mnenuka na Dkt. Tumaini J. Sanga

**Msanifu:** Bw. Katalambula F. Hussein

**Mchoraji:** Bw. Hance E. Wawar

**Mratibu:** Bi. Monica W. Manyanga

Vilevile, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wote wa shule za sekondari walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE READING ONLY

# Dibaji

Kitabu hiki cha *Fasihi ya Kiswahili: Kidato cha Tano* kimeandikwa mahususi kwa mwanafunzi wa Kidato cha Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Fasihi ya Kiswahili wa mwaka 2023 uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Baadhi ya maudhui ya kitabu hiki yamehamishwa kutoka katika Kitabu cha Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha Tano na Sita cha mwaka 2019. Kitabu hicho kiliandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2009 uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kitabu hiki kimegawanywa katika sura sita: Dhana na chimbuko la fasihi, Fasihi simulizi na fasihi andishi, Kutathmini kazi za kifasihi, Maadili katika fasihi, Ujumi katika kazi za kifasihi, na Kubuni kazi changamani za kifasihi. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, shughuli za kufanya, pamoja na vielelezo ambavyo vinachochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura kuna mazoezi yenye lengo la kupima na kujenga uelewa pamoja na ujuzi katika somo hili. Hivyo basi, mwanafunzi unapaswa kufanya mazoezi na shughuli zote zilizomo kwenye kitabu hiki pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu. Pia, unapaswa kuandaa mkoba wa kazi kwa ajili ya kutunza kazi mbalimbali zinazotokana na ujifunzaji.

Jifunze zaidi kupitia Maktaba Mtandao *https://ol.tie.go.tz/videos*

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Kwanza
# Dhana na chimbuko la fasihi

## Utangulizi

*Fasihi inatuwezesha kufikiri kwa kina na kufahamu tamaduni na masuala mbalimbali ya kijamii pamoja na kuwasiliana kwa ufasaha. Katika sura hii, utajifunza juu ya dhana ya fasihi, mitazamo mbalimbali ya dhana hiyo ya fasihi, na chimbuko la fasihi. Umahiri utakaojenga katika sura hii utakusaidia kukuza uelewa na kutathmini maarifa hayo.*

*Maisha bila Fasihi*

**Shughuli ya 1.1**

Kwa kutumia vyanzo vya maktabani, mtandaoni, au vinginevyo, bainisha matini ambazo unadhani ni fasihi, na eleza kwa nini unadhani hivyo.

## Dhana ya fasihi

Wataalamu mbalimbali wameielezea dhana ya fasihi kwa namna tofauti. Kwa ujumla wanakubaliana kuwa fasihi ni sanaa bunifu ya lugha inayosawiri hali mbalimbali za maisha. Hali hizi ni pamoja na mahusiano, hisia za watu, mazingira, migogoro na mengineyo. Sanaa ya fasihi inajidhihirisha katika tanzu kama vile tamthiliya, riwaya, ushairi, semi na nyinginezo.

**Shughuli ya 1.2**

Kwa kutumia mifano ya fasihi unayoifahamu, toa maoni yako kuhusu dhana ya fasihi.

**Shughuli ya 1.3**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, fafanua mitazamo kuhusu dhana ya fasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

Kuna mitazamo mbalimbali inayojadili dhana ya fasihi. Mtazamo wa kwanza unajiegemeza kwenye kisawe cha neno fasihi kwa kiingereza, yaani *literature*. Mtazamo huu unadai kuwa *literature* ni jumla ya maandishi yote yaani kila kitu kilichoandikwa ni fasihi. Mtazamo huu umeelezewa na Wellek na Warren (1986), Hata hivyo, dhana hii inapingwa na baadhi ya wanazuoni wa fasihi. Kwa mfano, Mulokozi (2017) anadai kuwa dhana ya *literature* inatofautiana na dhana ya fasihi. Katika lugha ya Kiingereza, maana moja wapo ya *literature* ni maandishi yoyote, ilhali katika Kiswahili, dhana ya "fasihi" inazingatia fasihi kama sanaa na aina zote za fasihi.

Mtazamo wa pili unadai kuwa fasihi ni hisi ambazo zinajifafanua kwa njia ya lugha. Wafuasi wakuu wa mtazamo huu ni Sengo na Kiango (1975). Wataalamu hawa wanasema kuwa ili mwanafasihi aweze kuandika au kueleza jambo kifasihi lazima aguswe na hisia fulani. Wataalamu hao wanasema kuwa hisi ni kama kusikia njaa, baridi, joto, uchovu au kuumwa. Mtazamo huu pia umekosolewa na baadhi ya wanazuoni. Kwa mfano, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa mtazamo huu unachanganya mambo matatu ambayo ni fasihi yenyewe, mambo yaelezwayo na fasihi, na mtindo wa kifasihi. Kwa mujibu wa mtazamo huu, fasihi inaweza kuelezea hisi lakini fasihi yenyewe si hisi. Kwa mfano, fasihi huweza kuelezea hisi za mapenzi lakini fasihi yenyewe si mapenzi.

Mtazamo wa tatu unaitazama fasihi kama sanaa ya lugha yenye ubunifu bila kujali kama imeandikwa au la. Mtazamo huu unaafikiwa na Kirumbi (1975), Mutembei (2006) na Senkoro (2011). Kwa mujibu wa mtazamo huu, hata nyimbo na masimulizi ya kisanaa ni fasihi, ijapokuwa hayakuandikwa. Kirumbi anasema kuwa fasihi ni taaluma ya sanaa inayowasilishwa kwa njia ya lugha katika muundo wa maandishi au matamshi. Senkoro (2011) ana mtazamo sawa na wa Kirumbi anapoieleza fasihi kuwa ni "sanaa itoayo maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno ambayo hutamkwa ama huandikwa."

Mtazamo wa nne unadai kuwa fasihi ni maandiko bora ya kisanaa yenye manufaa ya kudumu. Akizungumzia mtazamo huu, Summers (1989) anasema kuwa fasihi ni sanaa inayojumuisha zaidi maneno yaliyoandikwa. Mtazamo huu unaupa uzito ufundi wa kubuni lakini unafinya mawanda ya fasihi kwa kuhusisha mawazo yaliyo bora tu ambayo, hata hivyo, ni vigumu kuyaainisha.

Mtazamo wa tano unaeleza kuwa fasihi ni matokeo ya matumizi ya lugha kwa njia isiyo ya kawaida ili kuleta athari maalumu. Miongoni mwa waasisi wa mtazamo huu Roman Jakobson. Mtazamo huu huona kuwa fasihi hukiuka taratibu za

FOR ONLINE READING ONLY

kawaida za matumizi ya lugha katika sarufi, maana na sauti ili kumvutia na kumuathiri msikilizaji au msomaji. Mtazamo huu humfanya msomaji aitafakari lugha yenyewe badala ya kuutafakari ujumbe unaowasilishwa na lugha hiyo. Vilevile, fasihi inaonekana kuelemea zaidi upande wa fani na kupuuza maudhui, maana na muktadha wa kazi za fasihi.

Kutokana na mjadala huu, tunaweza kusema kuwa mitazamo hii yote inahusisha fasihi, maisha na jamii. Yaani, fasihi ni sanaa inayotumia lugha kuwasilishia hali mbalimbali zinazomhusu mwanadamu na maisha yake. Tunaposema "lugha" hatuna maana ya usemaji wa kutumia sauti tu, bali hata mawasiliano ya kutumia ishara na vitendo.

**Shughuli ya 1.4**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, jadili ubora na upungufu wa kila mtazamo kuhusu dhana ya fasihi.

**Zoezi la 1**

1. Ni kwa vipi si kila andiko ni fasihi?
2. Eleza ni kwa namna gani fasihi ni sanaa.
3. Jadili umuhimu wa fasihi katika maisha ya mwanadamu.

## Nadharia za chimbuko la fasihi

**Shughuli ya 1.5**

Soma matini mbalimbali zinazopatikana mkondoni na maktabani zinazohusu nadharia za chimbuko la fasihi, kisha zielezee kwa ufupi.

### Dhana ya nadharia

Wataalamu wanaeleza kuwa nadharia ni maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Nadharia za chimbuko la fasihi ambazo Senkoro (1987) na Mulokozi (2017) wanazitaja ni nadharia za kidhanifu na kiyakinifu.

### Nadharia ya kidhanifu

Msingi wa nadharia hii ni mawazo ya kudhani, yasiyotokana na uhalisi. Waasisi wa nadharia hii ni wanafalsafa wa Kiyunani, wakiwamo Plato na Sokrate. Wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa fasihi na sanaa vimetoka kwa Mungu. Hivyo, mwanafasihi huipokea sanaa ikiwa tayari imeivishwa na Mungu.

FOR ONLINE READING ONLY

Wachambuzi wengine wenye mtazamo wa kidhanifu ni Felician Nkwera na John Ramadhan. Katika insha yake kuhusu fasihi, Nkwera (1976) anasema "Fasihi ni sanaa ambayo huanzia kwa Muumba, humfikia mtu katika vipengele mbalimbali... (ni) hekima ambayo mtu ameshirikishwa apate kumtambua Muumba wake". Akiunga mkono mtazamo huo, Ramadhan (1975) anasema kwamba, ingawa fasihi ni hisi, kitendo cha mtu kuibuni kazi ya sanaa ni uigaji wa Mungu ambaye ndiye mfalme wa sanaa zote. Mawazo ya wafuasi wa nadharia hii hayana uthibitisho wowote zaidi ya kumtenga msanii na jamii yake kwa kumkweza na kuonekana yuko karibu na Mungu kuliko wanajamii wengine. Aidha, wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa mwanafasihi hawezi kubuni kitu chochote zaidi ya kuiga sanaa ambayo tayari Mungu ameitengeneza.

**Nadharia ya kiyakinifu**

Kwa mujibu wa Senkoro (1987), chimbuko la sanaa na fasihi ni mazingira halisi ya jamii, hususani sanaa ya mwanzo iliyofungamana na kazi za uzalishaji mali. Hii inamaanisha kwamba chanzo cha fasihi na sanaa ni binadamu (jamii) na mazingira yake. Katika harakati za kukabili mazingira yake, ilimlazimu binadamu kufanya kazi. Binadamu wa mwanzo aliishi katika mazingira yasiyo rafiki. Hivyo, ilimlazimu kutumia silaha ili apambane na mazingira hayo. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa kutafuta njia za kurekebisha silaha zake (mawebutu) kwa kuyachonga ili yawe na ncha kali. Uchongaji huo ndio ulikuwa sanaa yenyewe. Kwa hiyo, hisia za kisanaa zimefungamana na maendeleo ya mtu katika kupambana na mazingira yake na katika kufanya kazi. Nadharia hii ina mwelekeo wa kukubalika zaidi, kwani inakubaliana na fikra kuwa wanadamu walianza mawasiliano kupitia kazi zao. Kwa mantiki hiyo, chimbuko la sanaa ni kazi.

Kadiri binadamu alivyozidi kuendelea, alikuwa na mahitaji mengine zaidi ya mahitaji ya msingi. Mahitaji hayo yaliamsha hisia za kuchora vielelezo vya shughuli zake za kujikimu. Michoro ya mapangoni iliyopo Kondoa (Tanzania) ni mifano mizuri ya vielelezo hivyo. Kuzuka kwa lugha kuliongeza aina nyingine ya sanaa ambayo ni fasihi.

Fasihi, kama zilivyo sanaa nyingine, ilitokana na kazi alizofanya binadamu katika kupambana na mazingira yake. Fasihi ilianzia katika wimbo wa kazi. Baadaye, tanzu nyingine za fasihi zilitungwa na kusimuliwa kwa madhumuni ya kufunza, kukosoa, kuadibu, kuchokoza fikra na kuliwaza jamii baada ya kazi. Kadiri maendeleo ya uzalishaji mali yalivyoongezeka, binadamu akapata muda wa kupumzika na kustarehe kwa njia ya sanaa. Fasihi ilianza kutengana na kazi

FOR ONLINE READING ONLY

za uzalishaji na kuanza kuwa shughuli maalumu ya kijamii ambapo ilitendwa katika matukio mbalimbali, kama vile sherehe na ibada.

Nadharia nyingine inayoelezwa na Mulokozi (2017) ni ya mwigo au uigaji. Nadharia hii inazingatia ubunifu wa mwanadamu katika kuiga maumbile na mazingira yaliyomzunguka kwa kusawiri vitu vilivyomo katika hali mbalimbali. Akigusia dosari kuu ya nadharia hii, Mulokozi anasema kuwa katika kusisitiza mno uigaji, suala la ubunifu wa kisanaa na kifasihi linasahauliwa.

**Shughuli ya 1.6**

Jadili ubora na upungufu unaojitokeza katika nadharia za chimbuko la fasihi.

## Tamrini

1. Kwa kutumia mifano, fafanua maana ya dhana zifuatazo:
   (a) Fasihi
   (b) Mtazamo
   (c) Nadharia
   (d) Chimbuko
2. Dhana ya fasihi huelezwa kwa mitazamo mbalimbali. Jadili mitazamo hiyo.
3. "Ujifunzaji wa fasihi hauna umuhimu wowote." Jadili hoja hii.
4. Chunguza fasili za dhana ya fasihi zifuatazo kisha, eleza zinafanana na kutofautiana katika vipengele vipi?
   (a) Fasihi inahusisha ufundi wa matumizi ya lugha katika kuwasilisha dhana na matukio mbalimbali yanayomhusu binadamu na mazingira yake (Ponera, 2014).
   (b) Fasihi ni sanaa ya lugha yenye ubunifu inayosawiri vipengele vya maisha, mahusiano, mazingira na hisia za watu katika muktadha fulani (Mulokozi, 2017).
   (c) Fasihi ni sanaa itumiayo lugha ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa na unaoendana na jamii husika (Mlaga, 2017).

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Pili

# Fasihi simulizi na fasihi andishi

## Utangulizi

*Fasihi simulizi na fasihi andishi ni sanaa muhimu ambazo mtu huzitumia kwa malengo ya kujiburudisha, kuelimisha na hata kuhifadhi utamaduni wa jamii. Katika sura hii, utajifunza kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi na fasihi andishi na pia utajifunza uhusiano uliopo baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Aidha, utajifunza kuhusu mchango wa fasihi simulizi katika maendeleo ya fasihi andishi na mchango wa fasihi kwa jumla katika maendeleo ya jamii. Umahiri utakaoujenga katika sura hii utakusaidia kuchambua na kutathmini vipengele mbalimbali katika maisha.*

*Nyenzo ya kuwasilisha mawazo katika miktadha mbalimbali*

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 2.1**

Kwa kutumia vyanzo vya mkondoni na maktabani, chunguza tanzu na vipera vya fasihi simulizi kisha jibu maswali yafuatayo:

(i) Nini tofauti ya utanzu na kipera?

(ii) Kuna tofauti gani kati ya utani na majigambo?


(iii) Kuna tofauti gani kati ya utanzu wa hadithi na semi?

(iv) Sanaa za maonesho zina sifa zipi?

(v) Nini tofauti ya misemo na misimu?

### Tanzu na vipera vya fasihi simulizi

Wataalamu mbalimbali (kwa mfano Mulokozi na Wamitila) wamegawanya fasihi simulizi katika tanzu na vipera mbalimbali ambavyo vimeoneshwa katika Kielelezo namba 2.1.




**Kielelezo namba 2.1:** *Tanzu na vipera vya fasihi simulizi*

Yafuatayo ni maelezo ya tanzu na vipera hivyo:

**Shughuli ya 2.2**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maarifa, fafanua utanzu wa hadithi na vipera vyake.

**Hadithi**

Hadithi ni utungo unaotumia lugha ya mjazo (nathari) ili kueleza kisa fulani kwa mpangilio wa matukio. Mpangilio huo hutumia wahusika ambao ndio watendaji wa matukio hayo. Vilevile, hadithi huwa na kisa kinachofululiza tangu mwanzo hadi mwisho ili kukamilisha muundo wake.

Hadithi huwasilishwa na msimuliaji mbele ya hadhira katika mandhari maalumu kama vile chini ya mti mkubwa, sebuleni, darasani au uwanjani. Vilevile, huweza kuwasilishwa kwa njia za kidijiti. Aghalabu, simulizi hufanyika katika muda maalumu, hususani baada ya kazi. Kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2.1, utanzu wa hadithi una vipera vitano ambavyo ni ngano, tarihi, visasili, vigano, na soga.

FOR ONLINE READING ONLY

### (a) Ngano

Ngano ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu. Ni kipera cha mwanzo kabisa katika utanzu wa hadithi. Kwa kawaida, mtunzi wa ngano hajulikani. Ngano hupokezanwa na kuendelezwa kutoka kizazi hadi kizazi. Maudhui yake hujikita katika maadili, uhusiano na mwenendo mzuri katika jamii. Aghalabu, ngano ni hadithi za burudani ambazo husimuliwa katika mazingira ya starehe na mapumziko. Ngano ina vipera vidogo kadha. Baadhi ya vipera hivyo ni **kisasuli, hurafa, hekaya** na **istiara**.

**Kisasuli**

Kisasuli ni hadithi ya kisanaa yenye kueleza usuli na sababu za jambo, tukio au hali. Mathalani, zipo hadithi zinazoeleza kwa nini mnyama fulani anapenda kushirikiana na wanadamu au ameumbika kwa namna fulani. Tazama mfano wa kisasuli cha hadithi ya "Kwa nini nyoka hana miguu?"

*Kwa nini nyoka hana miguu?*

Siku moja Nyoka pamoja na wanyama wengine walialikwa kwenye sherehe nyumbani kwa mfalme. Kule walikula na kunywa! Baadaye mfalme aliwaita ili wapewe zawadi. Kwa sababu ya uroho wake, Nyoka hakusikia wito. Alipozinduka, alikuta miguu yote, hata ile hafifu ya Tandu na Buibui, imeshatolewa; akabakia anajiburuza kwa tumbo lake. Mpaka leo hii nyoka hana miguu (Balisidya, 1987).

**Hurafa** ni ngano zenye wahusika wanyama tu. Wanyama hao huwakilisha tabia na matendo ya binadamu kwa kurejelea masuala yanayopatikana katika jamii. Maudhui katika hurafa hueleza kuhusu tabia nzuri au mbaya za binadamu, kama vile woga, ulafi na tamaa. Katika hurafa, wanyama wanaotumiwa ni kama vile sungura, fisi na kobe. Sungura huwakilisha ujanja, kutokata tamaa na kutochoka. Fisi huwakilisha tamaa, ulafi, woga, uzembe na ujinga. Kobe huwakilisha ukimya, busara na utulivu. Aidha, ni mhusika ambaye hufanya vitu kimyakimya lakini huibuka mshindi. Ufuatao ni mfano wa hurafa:

*Sungura na Fisi*

Siku moja Sungura alipokuwa matembezini alikutana na Fisi. Fisi alimwangalia Sungura na kumuuliza, "Wewe unayekodoa macho hivi unaenda wapi, au kuila nyama yako?" Sungura akamwangalia Fisi na kumwambia, "Nimeambiwa na Simba nimsubiri hapa ndipo tuandamane hadi kwake nikamtayarishie ini la Fisi analolitamani sana." Fisi akamwangalia Sungura na kumwuliza, "Huyo Simba yuko wapi?" Sungura akaita kwa sauti ya juu, "Simbaaaaaa!"

FOR ONLINE READING ONLY

Baada ya kuita kwa sauti hiyo, Sungura alijigeuza kidogo, akapiga mluzi na kusema kwa sauti nzito, "Naja sasa hivi. Naandama nyayo za Fisi aliyepita hapa. Natamani kumkamata ili nipate ini lake nikuletee ukanitayarishie kama tulivyoagana. Mara tu Fisi alipoyasikia hayo, aligeuka na kutimua mbio kuelekea kichakani. Sungura alibaki alikokuwa na kuangua kicheko.

Hekaya ni ngano zenye visa visivyo vya kawaida vinavyoambatana na masaibu na pengine hata ujanja wa mhusika mkuu ambaye huweza kuwa mtu au mnyama. Hekaya hujengwa na visa vingi vinavyotofautiana. Mhusika mkuu katika hekaya hupitia misukosuko mingi hadi kukaribia kushindwa. Hata hivyo, katika hatua za mwisho kabisa, mhusika huyu huweza kuibuka mshindi kwa namna isiyotarajiwa.

Lengo la hekaya ni kumtia mtu moyo asikate tamaa anapopitia changamoto za aina mbalimbali. Kimsingi, kinachohimizwa ni kutumia akili kutatua matatizo ya maisha. Kwa kumtumia mhusika sungura, kwa mfano, tunahimizwa kuwa wajanja na kutokujidharau hata kama ni wadogo. Umbile dogo linaweza kuwakilisha pia uwezo wa kiuchumi kama vile kuwa na mtaji mdogo. Mtu anaweza kutumia mtaji mdogo kufanya biashara mpaka kufikia kiwango cha kuwa mfanyabiashara mkubwa. Ufuatao ni mfano wa hekaya:

*Mfanyabiashara na Wakeze*

Hapo zamani, kulitokea mfanyabiashara mmoja aliyekuwa na mali nyingi sana. Basi alioa mke, baadaye akaongeza mke wa pili (Bi mdogo). Wakaishi hivyo. Alitokea kumpenda zaidi Bi. Mdogo na kumnyanyasa Bi. Mkubwa (mke wa kwanza).

Siku moja, alikuwa na safari ya kwenda kununua bidhaa za duka lake. Basi akamwambia Bi. Mdogo ataje mahitaji yote ambayo angependa aletewe kama zawadi. Bi. Mdogo akataja vitu vingi. Naam, kwa kuwa mfanyabiashara yule alikuwa akimpenda sana, hakusita kumhakikishia kwamba angemletea. Kwa shingo upande, alimwendea vilevile Bi. Mkubwa na kumwambia ataje zawadi ya kumletea. Yule Bi. Mkubwa akamwambia mumewe asisumbuke ila amletee pete na kipande cha akili. Basi, kwa dharau yule bwana akakubali.

Basi tajiri yule akafunga safari akafika huko, akanunua vifaa vyake vyote alivyovihitaji kwa ajili ya duka lake. Vilevile, akanunua vitu vyote kama vile nguo ambazo Bi. Mdogo alimtuma, pamoja na pete ya Bi. Mkubwa. Sasa akakwama wapi apate kipande cha akili. Akazunguka maduka yote, asipate. Mwishowe, akaona ni upuuzi kuendelea kutafuta kipande hicho.

FOR ONLINE READING ONLY

Basi, katika ghadhabu yake, akawa akimtukana huyo Bi. Mkubwa, jinsi alivyokuwa mpumbavu. Ikatokea kwamba Bi. Kizee mmoja akamsikia alivyolalamika na kuapiza. Yule Bi. Kizee akamuuliza kwa nini alikuwa akilalamika. Yule bwana akamsimulia kisa chote. Bi. Kizee akamwambia yule bwana kuwa asipate taabu kwani kipande hicho anacho nyumbani. Wakafuatana kuelekea nyumbani kwa huyo Bi. Kizee. Kufika karibu na kule nyumbani, Bi. Kizee akamweleza kwamba kipande hicho kiko nyumbani kwa yule bwana, ila tu akitaka kukipata sharti atakapokaribia nyumbani kwake ajipake kinyesi, halafu aone jinsi wake zake watakavyompokea.

Basi tajiri akafanya kama alivyoagizwa. Alipokaribia nyumbani kwake, akajipaka kinyesi mwili mzima, akawa hovyo kabisa kisha akabisha hodi kwanza nyumbani kwa Bi. Mdogo. Bi. Mdogo kufungua mlango katika harakati za kumlaki, akaona mumewe kajaa kinyesi mwili wote. Bi. Mdogo akafoka sana na kumwambia asithubutu kuingia mle ndani hadi awe ameoga vizuri.

Basi yule bwana katika hali hiyohiyo, akaenda kwa Bi. Mkubwa. Bi. Mkubwa akamwona mumewe katika hali ile, akasikitika sana. Akamvua nguo zenye kinyesi, akamwosha, na kumvika nguo nyingine.

Ndipo yule bwana akamwambia mke wake, "Pete na kipande cha akili vyote nimepata. Isipokuwa kipande cha akili nimekipata hapahapa." Akachukua zawadi zote, hata zile za Bi. Mdogo, akampa yule Bi. Mkubwa, na kumfukuza Bi. Mdogo.

Wakaishi raha mustarehe.

*Riwaya ya Kiswahili* (Madumulla, 2009: 94 - 95)

**Istiara** ni hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana iliyofichika. Kwa hiyo, maana huwasilishwa kwa njia ya mafumbo. Kwa mfano, hadithi mashuhuri ya zimwi linalovamia kijiji na kuwameza wanakijiji wote isipokuwa mwanamke mmoja mjamzito ni istiara. Katika hadithi hiyo, mama huyo mjamzito baadaye anajifungua mtoto na kumlea akiwa mafichoni. Mtoto anapokua anamuuliza mama yake kwa nini wako peke yao kijijini, wakazi wengine walikwenda wapi. Mama yake anamweleza kuwa watu wote walimezwa na zimwi ambalo linaishi katika msitu ulio karibu na kijiji hicho. Mtoto anaamua kwenda kupambana na zimwi hilo hadi analiua. Baada ya kuliua analipasua tumbo na kuwatoa watu wote waliomezwa wakiwa bado hai. Watu wanafurahi na kumfanya

FOR ONLINE READING ONLY

mtoto huyo kuwa kiongozi wao. Kiistiara, hadithi hii huweza kuwakilisha ukoloni na mapambano ya kujikomboa. Zimwi linamwakilisha mkoloni, na mtoto ni mkombozi. Pia, hadithi hii inaweza kuwa ishara ya kupigania haki ya aina yoyote (Thomas, 2011)

Kwa kawaida, ngano huwa fupi kwa sababu ya muundo wake wa kuwa na kisa kimoja. Wahusika wa ngano ni bapa kwa maana kwamba mhusika akiwa mwema ni mwema mwanzo hadi mwisho wa hadithi, vivyo hivyo kwa mhusika mwovu. Lengo kuu la ngano, mbali na kuburudisha, ni kuadibu, kuadili na kuelimisha jamii. Hujaribu kujenga utu bora kwa kueleza wema na ubaya.

**(b) Tarihi**

Tarihi ni hadithi zinazohusu matukio muhimu ya kihistoria. Msingi wa hadithi hizi ni matukio ya kihistoria. Matukio haya yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni au mchanganyiko wa ukweli na ubunifu. Aghalabu, wahusika wa hadithi hizi ni binadamu. Miongoni mwa mifano maarufu ya tarihi ni *Tarihi ya Kilwa.* Tazama mfano ufuatao:

**Mji wa Kilwa na Watawala Wake**

Hapo awali, Mji wa Kilwa ulikuwa ukitawaliwa na Waswahili wenyewe. Kiongozi wa mwisho kabla ya ujio wa wageni alijulikana kwa jina la Mndimbo. Alitawala mpaka karne ya saba. Watawala waliofuata walikuwa wenye asili ya Kiarabu. Sultani wa kwanza, Ali bin-Hasan, alianza kutawala mwaka 1200BK. Inasemekana alitengeneza sarafu ya kwanza. Utawala wake ulifuatiwa na al-Hasan bin Daudi, ambaye alikuwa mjukuu wa Ali, lakini wengine walipinga kwa kuwa alikuwa mpwa wake na utawala wake ulikoma miaka ya 1300BK. Utawala mwingine ulianza mwaka 1300 ambapo al-Hasan bin Talut alianza kutawala. Al-Hasan bin Talut alikuwa mtawala wa kwanza katika ukoo wa tawala za Abu' l-Mawahibu. Alikuwa na sarafu chache sana zinazoashiria kipindi kifupi cha utawala wake. Mtoto wake aliyeanza kutawala alijulikana kwa jina la Sultani Sulaiman bin al-Hasan. Isivyo bahati, mtawala huyu haoneshwi katika orodha za Masultani katika fasili ya Kiarabu ingawa kuna sarafu nyingi ambazo zinasemekana zilikuwa zake. Alishika madaraka kwa miaka miwili tu. Mwaka 1320 al-Hasan bin Sulaiman alianza kutawala. Mtawala huyu alitembelewa na Ibn Batuta mnamo mwaka 1331. Inasemekana, huyu ndiye aliyejenga husuni kubwa na alikuwa na sarafu nyingi. Kuna habari kuwa Mafia ilichukuliwa na Kilwa katika utawala huu. Mtawala aliyefuata ni Daudi bin Sulaiman; huyu alikuwa ndugu wa al-Hasan bin Sulaiman. Inasemekana alikuwa na sarafu chache sana na ndiye mtawala wa mwisho kutengeneza sarafu kabla ya ujio wa Wareno (Massamba, 2017).



FOR ONLINE READING ONLY

**(c) Visasili**

Visasili ni hadithi zinazoelezea chimbuko au asili ya jamii, ukoo, au kundi fulani. Huelezea pia tamaduni mbalimbali na namna jamii fulani ilivyofika katika eneo fulani. Kadhalika, visasili huelezea na kufafanua masuala ya kimaumbile na kiimani yanayomhusu na kumsumbua binadamu kama vile maradhi na kifo. Visasili hueleza pia maana ya maisha na hatima ya mwanadamu kulingana na imani za jamii inayohusika. Kwa kawaida, visasili huheshimiwa na kuaminiwa na wanadamu, na huhusishwa na kuwa vielelezo vya miviga na ibada zao. Mfano wa kisasili ni hadithi za mataifa mbalimbali kuhusu kuumbwa kwa ulimwengu na vilivyomo. Mfano mzuri ni hadithi ya Wakikuyu ya "Gikuyu na Mumbi" ambayo inapatikana katika kitabu cha *Naushangilia Mlima Kenya* (Kenyatta, 1966), simulizi ya "Asili ya jina la Wakinga" kutoka kwa Wakinga, na simulizi ya "Adamu na Hawa" kutoka Mashariki ya Kati ambayo inapatikana katika *Biblia* na *Kurani*.

**Mfano wa Kisasili**

**Asili ya Jina la Wakinga**

Wenyeji wa jamii ya Wakinga wanapatikana Nyanda za Juu Kusini katika eneo lenye vilima, uoto mzuri wa asili na vijito vinavyotiririka kama mkufu usio na mwisho. Wenyeji wa jamii hii walikuwa na shughuli mbalimbali tangu enzi za zamani. Walijishughulisha na ufuaji chuma, viazi, ngano na njegere. Palipo na ustawi hapakosekani adui. Jamii hii ilikuwa na mbinu zake za siri za ulinzi ambazo kila mwanajamii alifundishwa katika makuzi yake. Wakinga walikuwa na maadui na walipigana vita mara kwa mara na kuvishinda vita hivyo. Adui alipovamia ardhi ya Wakinga, kiongozi alijitokeza na kupiga kelele 'Vakinga Vakinga!' (maana yake jihadhari) akiwa amepanda juu ya kilima. Baada ya hapo kila mwanajamii alitambua kuwa hiyo ni vita na kila mmoja aliwajibika kupambana. Wazee waliongoza jamii nzima kwa kutoa ushauri na kuombea ushindi, vijana walichukua silaha za kivita, wanawake na watoto walikimbilia kwenye mahandaki. Huo ndio mwanzo wa Wakinga kuitwa Wakinga kulikotokana na sauti hiyo ya tahadhari.

**(d) Vigano**

Vigano ni hadithi fupifupi za kifasihi simulizi. Mafunzo yake hutolewa kwa kutumia lugha ya picha kama ilivyo kwa methali. Hadithi hizi zina hadhi ya methali ingawa hutumia taswira pana kuliko methali. Kimsingi, hadithi za namna hii hutolewa kama vielelezo, hasa wakati wa mazungumzo au maongezi. Lengo kuu huwa ni kumkanya na kumfunza anayesikiliza.

FOR ONLINE READING ONLY

Kwa mfano, kigano kinaweza kueleza kuhusu mzazi aliyempenda mno mtoto wake wa pekee kiasi cha kutothubutu kumkemea au kumrudi. Hatimaye, mtoto alijenga tabia mbaya. Basi, msimulizi husema kwa methali: *Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.*

Aghalabu, vigano hutokea katika mazungumzo na, wakati mwingine, hutungwa papo hapo. Kwa mantiki hiyo, vigano vingi huwa havienei kwa sababu hufungamanishwa na muktadha wa maongezi na hutungwa kwa ajili ya mada husika tu. Kwa hiyo, hupotea baada ya mada kuwasilishwa.

**(e) Soga**

Soga ni hadithi fupifupi za utani na ucheshi. Hadithi hizi husimuliwa kwa mfuatano wa matukio yanayochekesha. Soga hujengwa juu ya tukio moja tu. Tukio hilo, aghalabu, hulenga kuchekesha kwa kubeza na kukejeli. Pia, hueleza mambo ya ukweli unaoumiza kwa njia ya ucheshi ili kupunguza ukali wa ukweli huo. Soga hupatikana au hufanywa na watu wa jamii zenye historia ya kufanyiana utani kama vile jamii za Wanyaturu na Wakurya, Wahaya na Waha, Wachaga na Wapare. Kwa ujumla, soga hujikita katika kuburudisha na, wakati mwingine, kuelimisha jamii. Tazama mfano wa soga inayowahusu Wamakonde hapa chini:

**Kisa cha Mmakonde na Ngedere**

Mmakonde mmoja alikwenda shambani kwake, akamkuta ngedere akila mahindi shambani mwake. Ngedere alipomwona Mmakonde akakimbilia juu ya mti. Mmakonde akamwona kule alikojificha, akamwambia: "Wee ngedere *nimechakuona*; *uchijifanye n'janja*, *telenka* hapa chini nikupige *nchale* ili upate adhabu moja tu. Vinginevyo, *n'kupige nchale* ukiwa hukohuko juu ya *nti*, upate adhabu mbili: Adhabu ya kupigwa *nchale*, na adhabu ya kuanguka kutoka juu ya *nti* baada ya kupigwa *nchale*. Je, wewe ungekuwa ngedere ungefanyaje?

**Shughuli ya 2.3**

Tumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, kufafanua semi na vipera vyake kwa kuzingatia maana na sifa.

**Semi**

Semi ni tungo fupifupi za fasihi simulizi, na aghalabu, hutumia picha, tamathali na ishara. Semi hutumika kutoa mafunzo, nazo zimegawanyika katika vipera mbalimbali kama vile methali, misemo, mizungu, mafumbo, na vitendawili.

**(a) Methali**

Methali ni semi za kimapokeo zenye hekima na busara zinazoelezea falsafa na uzoefu wa jamii fulani kwa muhtasari. Semi hizi hubeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Methali hutumika kusisitiza, kuelimisha, kuonya au kupongeza kwa njia za busara. Aghalabu, methali hujengwa kwa sitiari. Sitiari hizo hujitokeza katika pande mbili za methali ambazo hubainishwa kwa mkato. Angalia mifano ifuatayo:

(i) Mtaka yote kwa pupa / hukosa yote.

(ii) Usipoziba ufa / utajenga ukuta.

(iii) Aisifuye mvua / imemnyea.

(iv) Chanda chema / huvikwa pete.

(v) Mtaka cha uvunguni / sharti ainame.

Mifano ya hapo juu inaonesha kuwa methali hubeba dhima mahususi. Kwa mfano, methali (i) inawaasa wanajamii kutofanya mambo mengi kwa wakati mmoja. Ni vyema kumakinikia jambo moja ili kulifanya kwa ufanisi, ndipo uanze jambo jingine. Katika mfano wa (ii), jamii inaaswa kurekebisha tatizo katika hatua za mwanzo, yaani kabla madhara makubwa hayajatokea.

**(b) Misemo**

Misemo ni tungo zitumiazo picha, ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi ili kuelimisha au kuadilisha. Misemo hufananisha maisha na matukio au vitu. Wakati mwingine, misemo hutumika kutambulisha mazingira maalumu au kuijulisha hadhira kuhusu hali fulani ya kijamii. Angalia mifano ifuatayo:

(i) Bendera hufuata upepo.

(ii) Elimu ni bahari.

(iii) Ukubwa jalala.

Mfano wa (i) unaonesha hali ya maisha, kwani wapo watu ambao hufuata mkumbo bila kufikiria wala kuhoji kwa nini wanafanya jambo fulani na, hatimaye, kujikuta kwenye matatizo. Katika mfano wa (ii), elimu inafananishwa na bahari. Bahari ni kubwa, na haina mwisho, vivyo hivyo kwa elimu. Elimu hutupatia maarifa na ujuzi wa aina mbalimbali. Pia, elimu haina ukomo, kwani binadamu hujifunza kila siku. Mfano wa (iii) unalinganisha hali ya mtu kuwa mkubwa wa umri au cheo, na kutupiwa lawama hata kama hajatenda kosa, kama lilivyo jalala ambapo watu hutupa taka za aina mbalimbali.

FOR ONLINE READING ONLY

**(c) Mizungu**

Mizungu ni kauli zenye mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio. Mbali na vitendawili vya kawaida, kuna vitendawili vingine vijulikanavyo kama mizungu. Mizungu hii hutumia zaidi mafumbo. Kwa mfano, inaelezwa kwamba mtu hawezi kumwoa ndugu wa damu. Ukinzani huu umetumika kuonya ndugu wasiwe na uhusiano wa kimapenzi. Mizungu hutumia mafumbo ya hali ya juu, kwa hivyo hutumiwa na watu wazima katika miviga ili kueleza dhana na mawazo mbalimbali kwa maongezi au nyimbo. Mifano mizuri ya mizungu inayohusu jambo hili ni:

(i) Ua zuri sana limeota kwenye miiba; hivyo, huwezi kulichuma.

(ii) Papai limeiva nyumbani, ila siwezi kulila.

Mizungu hutumia lugha ya picha inayoonesha ukinzani wa fikra. Ukinzani husaidia kumfikirisha msikilizaji na kumpa changamoto ya kutafuta jibu. Mifano mizuri ya mizungu ni:

(i) Adui rafiki (moto)

(ii) Nimezishika lakini siwezi kuzitumia (mhasibu na fedha)

**(d) Mafumbo**

Mafumbo ni kauli au maelezo yanayoficha maana ambayo humtaka msikilizaji kuyafumbua. Kwa mfano, watu wanamteta mtu, ikitokea mtetwaji anakuja mahali hapo, mmoja wao anaweza kusema *wifi kaja* au *shangazi kaja*. Hii huwasaidia kubadilisha maongezi baada ya kufumbua *wifi* au *shangazi* kuwa ndiye mtu anayetetwa ingawa mtu huyo si wifi wala shangazi wa mtu yeyote katika kundi hilo.

Aidha, kwenye mazingira ambapo watu wanaongea lakini hawataki mmoja wao ajue maongezi yao, labda kwa sababu ni domokaya, mmoja wao anaweza kuwatahadharisha wenziwe kwa kusema hivi, *Ooho! Mkorosho umeanguka!* Inabidi waelewe kwamba "mkorosho ulioanguka" ni mmoja wao. Hivyo, wataongea kwa tahadhari kubwa. Aghalabu, mafumbo mengi huwa ni kejeli dhidi ya watu wenye tabia mbaya. Mafumbo yana malengo ya kuelimisha, kuwezesha mawasiliano, kuburudisha, kukosoa na kuonya kuhusu mambo yanayotendeka miongoni mwa wanajamii.

**(e) Vitendawili**

Vitendawili ni semi fupifupi za mafumbo zenye kutumia lugha ya picha, tamathali na ishara kueleza jambo lililofichika. Jambo hilo ndilo jibu la fumbo. Kwa

FOR ONLINE READING ONLY

kawaida, kitendawili hupewa jibu kwa neno moja au zaidi au maelezo. Kama ilivyo katika kazi nyingine za fasihi, vitendawili hutumika kuburudisha, kukuza uwezo wa kufikiri, kupamba lugha, kukosoa au hata kukejeli. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Pango langu limejaa mawe - **kinywa.**

(ii) Nyumba yangu ina nguzo moja - **uyoga/mwavuli.**

(iii) Blanketi la babu lina chawa - **mbingu na nyota.**

(iv) Bibi amejitwisha machicha ya nazi - **mvi.**

Uundaji wa vitendawili hutegemea mazingira ambako kitendawili hicho hutumika. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Watoto wa sultani wamevaa kofia.

(ii) Nimenunua sungura nimemvika kofia.

(iii) Nikune kichwa nikupe moto.

Jibu la vitendawili hivi vyote ni **njiti ya kiberiti.**

Tofauti ya vitendawili vya (i), (ii) na (iii) inatokana na mazingira. Kitendawili cha (i) kimeundwa katika mazingira ambayo sultani aliwahi kuishi. Kitendawili cha (ii) kimeundwa katika sehemu yenye wafugaji au pori lenye sungura. Kitendawili cha (iii) kimeundwa katika mazingira yanayoakisi udugu, ambapo ni rahisi mtu kuomba kukunwa kichwa.

**Shughuli ya 2.4**

Tumia maktaba au maktaba mtandao na vyanzo vinginevyo kujadili maana, sifa na vipera vya ushairi simulizi.

### Ushairi simulizi

Ushairi simulizi ni utanzu wa fasihi simulizi ambao huwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya uimbaji au ughani badala ya usemaji wa kawaida. Ushairi simulizi ulianza wakati binadamu alipoanza kufanya kazi. Kupitia lugha, binadamu alibuni nyimbo za kazi. Nyimbo hizo ndizo msingi wa fasihi simulizi. Nyimbo za kazi zilitungwa kwa kuzingatia mapigo ya zana za kazi ili ziweze kukumbukwa kwa urahisi.

FOR ONLINE READING ONLY

Ushairi simulizi hujipambanua na tanzu nyingine za fasihi simulizi kutokana na matumizi ya mizani, lugha ya mkato, lugha ya mafumbo na uimbaji au ughani. Mbali na kuzingatia mambo hayo yanayohusu ushairi kwa jumla, ushairi simulizi una sifa ya kutungwa papo kwa papo na kufungamana na muktadha au tukio mahususi. Vipera vya ushairi simulizi ni nyimbo, mashairi, ngonjera, maghani na tenzi. Wakati mwingine, mashairi huambatana na ala za muziki za jadi ama za kisasa.

**(a) Nyimbo**

Nyimbo ni tungo za kishairi zinazowasilishwa kimuziki kwa kutumia sauti iliyo katika mpangilio fulani wa mahadhi na melodia, na inayozingatia mapigo ya kiurari. Mahadhi au tuni ni sauti mahususi ya uimbaji wa wimbo fulani, na melodia ni mpangilio na mwendo wa uimbaji wenye kuzingatia urari wa mapigo au ridhimu aghalabu hutofautiana kati ya jamii moja na nyingine. Nyimbo huweza kuimbwa na kuchezwa pamoja na ala za muziki. Nyimbo huimbwa na mtu mmoja au kundi la watu. Wakati mwingine, kikundi cha waimbaji huwa na kiongozi na wafuasi wake. Kiongozi huanzisha wimbo, halafu wafuasi huitikia mkarara. Kiongozi wa nyimbo huitwa manju. Nyimbo zinaainishwa kwa kuzingatia dhima, hadhira inayoimbiwa na muktadha unaofungamana nazo. Kutokana na vigezo hivyo, tunapata baadhi ya aina kama ifuatavyo: tumbuizo, bembezi, kongozi, nyimbo za dini na wawe. Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu aina hizi:

(i) Tumbuizo ni nyimbo za furaha ziimbwazo katika matukio mbalimbali kama vile harusini na ngomani.

(ii) Bembezi/chombezi ni nyimbo za kubembelezea watoto.

(iii) Kongozi ni nyimbo za kuaga na kukaribisha mwaka.

(iv) Nyimbo za dini ni nyimbo zinazoimbwa kwa lengo la kumsifu Mungu au miungu.

(v) Wawe ni nyimbo za kilimo zinazopatikana karibu katika makabila yote ya Tanzania.

(vi) Mbolezi ni nyimbo zinazoimbwa kufuatia matukio ya huzuni, hasa ya vifo.

(vii) Nyimbo za watoto ni nyimbo zenye maudhui mahususi kwa ajili ya watoto.

FOR ONLINE READING ONLY

### (b) Mashairi

Mashairi ni tungo zenye kuelezea au kuonesha kwa ufupi wazo au jambo au hisi fulani kuhusu binadamu na mazingira yake. Mambo hayo huelezwa katika mpangilio maalumu wa maneno fasaha yenye muwala, aghalabu kwa lugha ya kitamathali yenye kugusa moyo. Tunaposema mpangilio wa maneno tunamaanisha kuwa mpangilio wa maneno katika shairi hufuata kanuni tofauti na ule wa nathari. Si lazima shairi kufuata kanuni za miundo ya sentensi inayotumika katika lugha husika. Mathalani, badala ya kuandika *usikate tamaa maishani* huweza kuandikwa *maishani usikate tamaa* - mpangilio ambao ni tofauti na mpangilio wa kawaida. Baadhi ya tungo za taarabu ni ushairi simulizi.

#### Ngonjera

*Ngonjera* ni neno la Kigogo lenye maana ya "twende pamoja" au "tuambatane." Kipera hiki kilikuwapo toka zamani ila kilihuishwa mwishoni mwa miaka ya 1960 na Mathias Mnyampala katika harakati zake za kuelezea siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Ngonjera ni mazungumzo au majibizano ya kishairi kuhusu mada fulani. Kwa kawaida, ngonjera haziimbwi, hughaniwa. Aghalabu, majibizano hayo huwa na washiriki wa pande mbili, upande wa wanaopinga na upande wa wanaotetea hoja. Wahusika hawa hutumia lugha ya kiishara pamoja na miondoko ya mwili kama vile mikono, macho na midomo. Kutokana na wahusika kutumia miondoko, ngonjera huitwa ushairi wa maigizo. Katika ngonjera, suluhisho hupatikana mwishoni mwa majibizano, ambapo pande mbili zinazopingana hukubaliana. Ingawa ngonjera za Mathias Mnyampala ni fasihi andishi, lakini zinaweza kutendwa jukwaani. Mfano mzuri ni ngonjera ya Mkopo wa Fedha ya Mathias Mnyampala inayopatikana katika kitabu cha Ngonjera za Ukuta. Ngonjera hiyo ni majibizano ya papo kwa papo.

Mkopaji

*Hodi Bwana nimekuja, nina shida na tatizi*
*Nijile kutaka haja, arubani ghawazi*
*Tazileta kwa pamoja, siku mbili zizi hizi*
*Tafadhali nikopeshe, haondoe shida yangu*

Mkopwaji

*Nimekwisha kusikia, tuliza yako nafusi*
*Haja nitakukidhia, Inshallah kitu hukosi*

FOR ONLINE READING ONLY

*Shida yako ni rupia, takujalia fulusi*
*Hebu njoo Jumamosi, bado nashauri moyo*

Mkopaji
*Hodi Bwana nawasili, kwa ile yetu miadi*
*Unihesabie mali, arubani nakidi*
*Muaminishe Jalali, nifanyie itikadi*
*Tafadhali nikopeshe, haondoe shida yangu*

Mkopwaji
*Moyo wangu siamini, kukuhesabia mali*
*Shuruti lete dhamini, ambaye msema kweli*
*Shilingi arubaini, kulipa huna dalili*
*Hebu njoo Jumapili, bado nashauri moyo*

*Ngonjera za Ukuta: Kitabu cha kwanza* (Mnyampala, 1967:22)

**(c) Tenzi**

Tenzi ni tungo ndefu zinazoeleza tukio fulani linalotokea au lililowahi kutokea katika jamii; au zinazofafanua jambo au fikra fulani. Tenzi huwa na kisa kimoja kinachoelezwa kwa kina. Kisa hicho kinaweza kuwa maelezo kuhusu wasifu wa mtu fulani, jambo fulani la kihistoria au jambo lolote. Sifa ya kusimulia au kuelezea jambo kwa urefu ndio husababisha tenzi kuwa na beti nyingi kuliko mashairi au aina nyingine za ushairi.

**Utendi** ni utungo wenye masimulizi marefu kuhusu matendo ama matukio ya kishujaa na wasifu wa mashujaa. Utenzi na tendi huwa na muundo wenye kufungamana na mahadhi ya ala ya muziki inayotumika au melodia ya uimbaji. Kwa kawaida, hazina urari wa vina na mizani. Tenzi zenye urari wa vina na mizani ni zile zenye kufuata kanuni za ushairi andishi wa Kiswahili japo chimbuko au utungaji wake ni wa kisimulizi. Mifano ya tenzi hizo ni *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* (Mulokozi, 1997) na *Utenzi wa Mwanakupona*. Mfano wa tendi ni *Utendi wa Fumo Liyongo* (Kijumwa, 1913) katika *Tenzi Tatu za Kale* (Mh. Mulokozi, 1999). Katika tenzi hizo, mishororo haikugawanywa katika vipande viwili. Kila ubeti huwa una mistari minne; mistari mitatu ya kwanza ikiwa na vina vyenye urari na ule wa mwisho ukiwa na kina tofauti. Pamoja na vina hivyo kuwa na urari sawa, hubadilika toka ubeti mmoja hadi ubeti mwingine. Kina kinachorudiwa katika

FOR ONLINE READING ONLY

mstari wa mwisho, huitwa bahari. Ufuatao ni mfano wa beti za *Utendi wa Fumo Liyongo* ambao unatokana na utendi simulizi:

*Niweleze kwa utungo,*
*Hadithi yake Liyongo,*
*Niweleze na mazingo,*
*Mambo yalomzingiya.*

*Liyongo kitamakali,*
*Akabarighi rijali,*
*Akawa mtu wa kweli,*
*Na haiba kaongeya.*

*Kimo kawa mtukufu,*
*Mpana sana mrefu,*
*Majimboni yu marufu,*
*Watu huya kwangaliya.*

*Ni mwanamume swahihi,*
*Kama simba unazihi,*
*Usiku na asubuhi,*
*Kutembea ni mamoya.*

*Kisa katiti kutuwa,*
*Mkobani akatowa,*
*Zitu alizotukuwa,*
*Nyumba ndima nisikiya.*

*Katowa kinu na mti,*
*Na jiwe na kupaza kuti,*
*Na zunguze si katiti,*
*Na mawe ya kupikiya.*

*Tenzi Tatu za Kale* [Kijumwa, katika Mulokozi (Mh) (2009)]

FOR ONLINE READING ONLY

Beti hizi ni sehemu ya simulizi ya kiutendi inayomhusu Fumo Liyongo. Simulizi hii inaakisi maudhui ya kipindi cha miaka ya 900-1500 BK. Hivyo, lugha iliyotumika ni ile inayoakisi kipindi hicho. Pia, simulizi katika utendi huu inahusu masuala kama vile nguvu za kimwili, kiakili, kisihiri, kivita na kiume (urijali).

**Shughuli ya 2.5**

(a) Tunga kazi kwa kutumia kipera kimojawapo cha ushairi.

(b) Chagua suala mtambuka mojawapo katika jamii kisha andaa majigambo.

**Shughuli ya 2.6**

Jadili sanaa za maonesho kwa kuzingatia maana, aina na sifa zake.

**Sanaa za maonesho**

Balisidya na Muhando (1976) wanadai kwamba sanaa za maonesho ni sanaa ambazo huwasilisha wazo ana kwa ana kwa kutumia usanii wa utendaji. Utanzu huu hujumuisha kipera chochote chenye mambo yafuatayo:

(i) Dhana ya kutendeka (tendo);

(ii) Mtendaji (fanani);

(iii) Uwanja wa kutendea (jukwaa);

(iv) Watazamaji (hadhira); na

(v) Kusudio la kisanaa (maudhui).

Sanaa za maonesho huwa kwenye umbo linalotendeka. Huweza kugawanyika katika makundi mawili ambayo ni sanaa za maonesho za jadi na sanaa za maonesho mamboleo. Sanaa za maonesho za jadi ni zile zilizochipuka katika jamii za Kiafrika. Sanaa hizi hujumuisha majigambo, miviga, vichekesho, ngomezi, tambiko, utani, maigizo na michezo ya watoto. Ingawa miviga kama vile ibada, sherehe, jando na unyago ni matukio ya kijamii au kimila yenye kuvuka mipaka ya kisanaa, lakini inajumuishwa hapa kwa kuwa sanaa hutawala utendaji na uwasilishaji wa maudhui yake. Wakati wa uwasilishaji wa shughuli hizi, watu hufanya vitendo vya kisanaa kama vile uigizaji wa visasili, uchezaji ngoma, uimbaji na utongoaji mashairi, vikiambatana na matendo ya mwili. Kwa njia hii, watu huweza kuwasiliana wao kwa wao au kuwasiliana na miungu. Ijapokuwa dhima ya sanaa hizi hufanana kwa namna ya jumla, huwa kuna tofauti mahususi katika vipengele vya utendaji kati ya jamii au kabila moja na jingine.

FOR ONLINE READING ONLY

Wakati wa ukoloni, sanaa za jadi, hasa zile zilizohusiana na imani za dini, zilipigwa vita. Hali hii ilisababisha sanaa kama vile matambiko kupotea katika baadhi ya jamii. Sanaa nyingine zimedumu mpaka leo kutokana na wito wa kitaifa wa kudumisha utamaduni wa Kitanzania na uimara wa jamii wa kutunza utamaduni wao.

Sanaa za maonesho mamboleo ni zile zilizotokana na athari za ujio wa wageni. Sanaa za namna hii ni vichekesho na maigizo.

**Majigambo**

Majigambo ni masimulizi ya kujisifia au kujikweza kwa mtu kuhusu mambo aliyowahi kufanya. Mambo hayo huwa ni ya kishujaa kama vile kupigana vita, kuua wanyama wakali au kufanya jambo lolote kubwa la kishujaa. Kwa kawaida, majigambo husimuliwa katika lugha ya kishairi na yanaweza kujitokeza katika fasihi andishi na fasihi simulizi, zikiwamo bongo fleva na taarabu. Mjigambi hufanya matendo mbalimbali. Aghalabu, mjigambi hubeba silaha kama vile mkuki na ngao au upinde na mishale. Kama mjigambi ametoka kuua simba, kwa mfano, ataonesha matendo ya jinsi alivyopambana na simba hadi kumshinda.

Makabila yenye sanaa za majigambo ni yale ya Ukanda wa Ziwa (kama vile Wakurya, Wasukuma na Wahaya), yale ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania, hususani Wahehe, na ya Kaskazini mwa Tanzania, hasa Wamasai. Majigambo hufanyika wakati wa sherehe za harusi na za kuwapokea au kuwapongeza mashujaa. Pia, hufanyika kwenye mikutano inayoitishwa na watawala. Majigambo huambatana na ngoma na nyimbo za kusifu. Mjigambi hutokea katika kikundi kinachocheza na kujigamba. Baada ya kumaliza, mjigambi mwingine hufuata. Mara nyingi, mjigambi wa mwisho huwa yule aliyetenda jambo la kishujaa kuliko wote au yule anayeijua vizuri sanaa ya majigambo.

Lengo kuu la majigambo ni kujenga ari ya ushujaa, ukakamavu na ujasiri. Mtu anayefanya kitendo cha kishujaa, hushangiliwa na kupewa heshima kubwa katika jamii yake. Kwa msingi huu, vijana huhamasika kuwa wajasiri na wakakamavu ili kulinda hadhi na heshima ya jamii zao. Ijapokuwa, wajigambi wengi kwa kawaida, huonekana kuwa wanaume hasa katika ngoma za kujigamba na kwenye vikao vya pombe hata wanawake hujigamba katika miktadha tofauti ikiwamo ile ambayo inawahusisha wanawake peke yao. Mfano mzuri ni katika taarabu, hasa zile za mipasho. Kwa ujumla, majigambo hulenga kudumisha utu na heshima ya mtu katika jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

### (a) Matambiko

Matambiko ni ibada zinazoambatana na utoaji wa sadaka kwa Mungu, miungu na mizimu. Tangu zamani, jamii mbalimbali zilifanya matambiko ili kutoa shukrani, kusifu, kuomba msamaha na kadhalika. Tambiko ni tukio halisi ambalo baadhi ya matini zinazotumika huwa na maneno ya kisanaa. Licha ya matumizi ya lugha ya kisanaa kama vile tamathali za semi, taswira na lugha ya mafumbo kwa ujumla, matini za ushairi wakati mwingine husheheni nduni za ushairi ndiyo maana linaingizwa katika kundi la sanaa za maonesho. Kwa kawaida, matambiko hufanywa na watu maalumu katika jamii. Matambiko hufanyika katika maeneo maalumu. Kwa mfano, watambikaji katika baadhi ya jamii za Kanda ya Ziwa huelekeza maombi yao kwa *Namhanga* (Mungu Mkuu), *Mugasa* (mungu wa wavuvi) au *Kalungu* (mungu wa wawindaji). Utendaji wa tambiko hili huenda sanjari na matumizi ya maleba, vyungu na pembe maalumu. Sadaka zitolewazo na jamii ya Wakerewe hujumuisha kuku, mbuzi, kondoo, ng'ombe, vyakula vya nafaka na pombe huitwa *empahe*.

### (b) Miviga

Miviga ni sherehe au shughuli zinazofanywa na jamii katika kipindi maalumu cha mwaka au katika muktadha maalumu. Sherehe hizo zinaweza kuwa za jando na unyago, harusi, au kutawazwa kwa Mtemi. Miviga ni sherehe zihusuzo mtu kutoka katika kundi au wadhifa fulani na kuingia katika wadhifa mwingine. Mathalani, anaweza kutoka katika rika la utoto kwenda ujana (jando na unyago) na ujana kwenda utu uzima (kuoa au kuolewa). Kadhalika, miviga ni matendo ya kimila ambayo wakati mwingine huhusisha sehemu kubwa ya jamii.

Miviga huambatana na maigizo na nyimbo zinazoendana na tukio husika. Katika harusi, nyimbo zinazoimbwa ni za ndoa; na katika mazishi nyimbo zinazoimbwa ni za maombolezo. Katika miviga, ngoma mbalimbali huchezwa. Aghalabu, wazee hutoa mafunzo na mawaidha, hususani kwa watoto na vijana.

### (c) Vichekesho

Vichekesho ni aina ya sanaa ya fasihi simulizi. Katika sanaa hii, watu husimulia visa na mikasa ambavyo huwafanya wasikilizaji na watazamaji wacheke. Vichekesho vinahitaji ubunifu mkubwa ili kupata jambo litakaloibua hisia na kuvunja mbavu. Lugha inayotumika katika vichekesho ni nyepesi na iliyojaa picha ambazo watazamaji wana uwezo wa kuzitambua. Hii ni kwa sababu hutumia mifano ya vitu vinavyojulikana wazi kwa hadhira au vinavyopatikana katika mazingira yao. Aidha, vichekesho hutumia mbinu ya kejeli, dhihaka na utani.

FOR ONLINE READING ONLY

Kama ilivyodokezwa katika maelezo ya sanaa za maonesho kwa ujumla, vichekesho ni mojawapo ya sanaa mamboleo; vichekesho vingi vimetokana na kuletwa kwa tamthiliya za kizungu zilizobeba na kuongelea utamaduni wa kimagharibi. Baadhi ziliongelea matatizo ya kijamii ya wakati wa ukoloni, mathalani suala la mgongano kati ya miji na vijiji, na uzuzu au ushamba wa Mwafrika anayetoka kijijini na kuingia mjini kwa mara ya kwanza. Maigizo hayo hayakuwa na maana kubwa kwa Waafrika zaidi ya kuwachekesha kupitia katika vitendo vilivyofanywa kwenye jukwaa. Kwa hiyo, Waafrika wakadhani kuwa jambo muhimu katika vichekesho ni kuchekesha.

Kimsingi, dhima ya vichekesho si kuchekesha tu, bali vichekesho huelimisha pia. Mifano ya vichekesho ni kama ile inayopatikana katika vipindi vinavyorushwa na vituo vya redio, mitandao ya kijamii, na runinga. Mifano ya vipindi vya kwenye runinga ni Mizengwe (*ITV*), Futuhi (*Star TV*), Vitimbi Show (*Channel Ten*), na Kitimtim (*DSTV*).

**(d) Ngomezi**

Hii ni sanaa ya kuwasiliana kupitia midundo ya ngoma. Baadhi ya jamii hupeana taarifa za matukio mbalimbali kupitia ngoma. Aghalabu, taarifa hizo huwa katika hali ya mafumbo, kiasi kwamba, wenyeji wa jamii husika tu huweza kubaini maana ya midundo husika. Hii yatokana na ukweli kuwa midundo katika sanaa hii hufuata kanuni maalumu zinazojulikana na wanajamii hao tu. Kanuni hizo hubebwa kupitia vipengele vya aina ya ngoma zinazotumika, muda wa kupigwa kwa ngoma pamoja na kasi au mwachano wa upigaji. Kanuni hizi huwasaidia wanajamii kupata ujumbe unaowasilishwa. Kwa mfano, katika jamii ya Wayao kuna ngoma inayojulikana kama *Ngula-ntwe* inayopigwa kwa ajili ya kutoa ujumbe kuhusu matukio mbalimbali ya kitanzia. Kutokana na mapigo na midundo ya ngoma, ujumbe huo huweza kufasiliwa kuwa: "Simba amevamia na kuua mifugo", "Simba amejeruhi mtu ila hajamuua", "Simba ameua mtu", au "Kesho wanaume wote wanatakiwa kwenda kwenye msako wa simba mvamizi."

**(e) Utani**

Ni hali ya kufanyiana mizaha au masihara baina ya watu ambapo hali hii ni tofauti na desturi za kutokuheshimiana. Wanajamii wenye uhusiano wa kutaniana, hutaniana mahali popote wakutanapo kama vile msibani, harusini, hata kwenye sehemu za kazi. Utani huweza kuwa kati ya mtu na mtu, ukoo na ukoo au kabila na kabila. Utani kati ya mtu na mtu huwa kati ya babu/bibi na wajukuu, mtu na shemeji au wifi na wifi. Kadhalika, utani kati ya kabila na kabila, aghalabu, huwa kati ya makabila yenye asili ya kuishi katika eneo moja au yaliyokuwa na

FOR ONLINE READING ONLY

maingiliano ya muda mrefu. Makabila yote ya Mkoa wa Mara, kwa mfano, ni watani wa Wanyaturu na Wanyiramba (Singida) na Wahaya (Kagera).

Utani hujenga uhusiano na ushirikiano mzuri baina ya wanajamii. Vilevile, utani hutunza historia ya jamii zinazotaniana. Aidha, utani huwafunza watoto upendo na majukumu, mathalani, utani wa mjukuu wa kike na babu anapomwita mke wake na kuomba amfanyie jukumu fulani, mtoto huyo hujifunza jukumu lake atakalolitekeleza akiwa mkubwa. Vilevile, utani hukumbusha wanajamii majukumu yao. Mathalani, katika misiba, watani hutumia tukio kukumbusha watu kujuliana hali wanapokuwa wazima na kusaidia kazi zihusuzo msiba. Kama zilivyo dhima nyingine za fasihi, utani huburudisha kwenye matukio ya furaha na huzuni. Ikumbukwe kwamba, utani unaweza kusababisha ugomvi endapo mhusika hajui kuwa anayemfanyia mzaha ni mtani wake.

**(f) Maigizo**

Maigizo ni sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha au kutoa ujumbe fulani. Maigizo haya yanapoletwa jukwaani na kuoneshwa kwa hadhira huitwa drama. Mara nyingi, maigizo ya Kiafrika huambatana na utambaji wa hadithi, vichekesho, nyimbo, matendo ya kijadi kama vile harusi, jando na unyago. Wahusika hutakiwa kutumia lugha ya kifasihi inayoendana na hadhira. Zipo aina mbalimbali za maigizo, zikiwamo maigizo ya misibani na mivigani, maigizo ya watoto na ya burudani.

**(g) Michezo ya watoto**

Watoto hucheza michezo mingi yenye kuambatana na usanii. Michezo hiyo hutofautiana majina kulingana na mahali. Katika michezo hiyo, kuna kuimba, kucheza, kurukaruka, kukimbia, kughani, kujigamba na kuigiza. Baadhi ya michezo hiyo ni: kiota, ukuti, pembea (bembea), kitikiti, kibuzi na kombolela. Aghalabu, michezo hiyo huambatana na nyimbo, majibizano, vitendo na maigizo. Kwa mfano, katika mchezo wa kiota, watoto hunyanyuka pale walipoketi na kuanza kutangatanga huku na huku ilihali wakiimba mpaka kila mmoja anapopata mahali pake na kukaa. Watoto huimba hivi:

**Kiota**

Sisi ndege twaruka

Twatafuta kiota

Kiota

Kiota

Kiota

FOR ONLINE READING ONLY

Ta la la la la la

Kiota

Wimbo wa mchezo huu huambatana na vitendo vya kutembea na kuzunguka. Michezo mingi ya watoto hujumuisha pamoja nyimbo na vitendo.

Maigizo ya watoto ni aina nyingine ya michezo ya watoto. Watoto huigiza michezo inayoakisi mazingira yanayowazunguka kama vile nyumbani, shuleni, shambani, hospitalini, barabarani, kanisani, msikitini na porini. Pia, watoto huigiza mambo wanayoyaona kwenye runinga, hasa watoto waishio mijini. Kwa mfano, huigiza michezo ya kivita, sherehe mbalimbali, vikundi vya nyimbo, miziki na michezo ya kuigiza.

Maigizo ya watoto, kama ilivyo kwa kazi nyingine za fasihi, yana vipengele vya fani na maudhui. Maudhui ya michezo ya watoto, kwanza, huhusu maisha ya nyumbani kwa sababu ndiyo maisha wanayoyaona mara kwa mara. Watoto huigiza maisha ya nyumbani kwa kuakisi maisha halisi ya familia, hususani yale wanayoyaona kwenye kaya zao. Mathalani, kama baba au mama ni mkali, mtoto atakayewaigiza, ni lazima atakuwa mkali, pengine kuzidi ukali anaouona kwa wazazi wake; vivyo hivyo, kama baba au mama ni mpole na mkarimu basi muigizaji ataigiza upole na ukarimu wao. Ikiwa mzazi ni mchapakazi, basi muigizaji atakuwa na tabia hiyo. Kama ni nadhifu, mwigizaji naye atajitahidi kuwa nadhifu. Kwa hiyo watoto waigizao nafasi ya wazazi wao, huakisi tabia ya wazazi hao.

Kwa kawaida, hakuna matini inayokuwa imeandaliwa kabla ya mchezo, bali maigizo ya watoto hubuniwa papo kwa papo. Watoto wanapokutana hukubaliana aina ya mchezo na kugawana majukumu ya kila mhusika; wakati mwingine, watoto wenyewe huchagua nafasi watakazoigiza. Uigizaji wa michezo ya watoto huambatana na ubunifu ambapo kila mtoto (mhusika) hubuni uigizaji wa uhusika wake. Katika maigizo yanayohusisha wanyama, kwa mfano, kama igizo lina mhusika simba, mtoto anayeigiza kama simba ni lazima awe na sifa za ubabe, sauti nzito na nguvu. Halikadhalika, atakayeigiza kama jogoo, awe na sauti kali ili atakapowika asikike.

Aidha, watoto huchagua nafasi kulingana na uwezo wao na jinsi jamii ilivyoainisha majukumu mbalimbali kama ya udaktari, ualimu, uaskari na mengineyo. Kwa hiyo, watoto huchagua nafasi za kuigiza kutokana na kazi wazipendazo. Wakati mwingine kupitia michezo hii, ndoto za watoto huchomoza na watoto wengine huanza kuishi na ndoto zao.

FOR ONLINE READING ONLY

Baadhi ya sifa za maigizo ya watoto ni kuwa na muundo wa moja kwa moja na kutohitaji maleba mahususi.

**Shughuli ya 2.7**

Tumia vyanzo mbalimbali kuchunguza michezo mitatu ya watoto, kisha bainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika utunzi wa michezo hiyo.

## Zoezi la 2.1

1. Kwa kutumia mifano fasili dhana zifuatazo:
   (a) hurafa (b) soga (c) lakabu
   (d) istiara (e) visasuli (f) hekaya
   (g) ngomezi

2. Kwa kutumia mifano, eleza tofauti kati ya ngano na vigano.

3. Kwa kutumia mifano anuwai, tofautisha vichekesho na maigizo.

4. Jadili athari za utani unaofanyika katika jamii yako.

5. "Si kila mchezo wa watoto ni fasihi simulizi." Jadili kauli hii kwa hoja maridhawa.

6. Kwa kutumia mifano, tofautisha dhana zifuatazo:
   (a) tendi na tenzi
   (b) maghani na nyimbo
   (c) visasili na visakale
   (d) vitendawili na mizungu
   (e) visasili na visasuli

7. Chambua mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika ngano, visasili, na soga.

8. Sikiliza ngano mbili kutoka kwa wenzako kisha andika insha fupi kueleza mafunzo yaliyomo katika ngano hizo.


FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 2.8**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani eleza sifa za fasihi andishi na tanzu zake.

## Tanzu na vipera vya fasihi andishi

Kama ilivyo kwa fasihi simulizi, fasihi andishi pia ina tanzu zake. Kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali kama vile Wamitila (2002) na Mulokozi (2017) kuna tanzu nne za fasihi andishi ambazo ni ushairi, hadithi fupi, tamthiliya na riwaya. Kadhalika, tanzu hizo zimegawanyika katika vipera. Tazama Kielelezo namba 2.2.




**Kielelezo namba 2.2:** *Tanzu za fasihi andishi*

**Shughuli ya 2.9**

Kwa kutumia vyanzo vya maktabani au vinginevyo, jadili dhana na chimbuko la ushairi wa Kiswahili.

### Ushairi

Mulokozi (2017) anaueleza ushairi kuwa ni "sanaa ya lugha ya mkato yenye ubunaji inayosawiri au kueleza jambo, hisi, hali au maono kwa namna yenye kuvutia hisia na katika mpangilio wa maneno wenye urari na wizani." Inamaanisha kuwa ushairi husawiri mawazo, hisi au tukio kwa muhtasari katika mpangilio maalumu wa lugha teule ya kitamathali. Kwa hiyo, ushairi hutofautiana na tanzu nyingine za fasihi andishi katika umbo na matumizi ya lugha. Tanzu nyingine hutumia lugha ya mjazo ya kinathari lakini ushairi hutumia lugha ya mkato, yenye

FOR ONLINE READING ONLY

kueleza maudhui yake kimuhtasari; na aghalabu, huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara. Kama ilivyo kwa ushairi simulizi kwamba ndio utanzu wa kwanza kabisa wa fasihi simulizi, ushairi andishi nao ulikuwa utanzu wa kwanza wa fasihi andishi.

**Historia fupi ya ushairi wa Kiswahili**

Tarehe mahususi za kuanza kwa ushairi wa Kiswahili, hususani umbo la ushairi linaloonekana leo, ni za kukisia. Kilicho bayana ni kwamba, kabla ya karne ya 10 ushairi wa Waswahili ulikuwa ukitungwa na kughaniwa kwa ghibu bila kuandikwa. Hali ilibadilika kuanzia karne ya 10 wakati Uislamu ulipoanza kuenea Uswahilini; na hivyo, kueneza hati ya Kiarabu. Kuanzia wakati huo, baadhi ya Waswahili walianza kutunga na kuandika mashairi, hasa tenzi na tendi, kwa kutumia hati hiyo.

Wataalamu hugawa maendeleo ya ushairi wa Kiswahili katika mihula mbalimbali. Kwa mfano, Kezilahabi (1983) anabainisha mihula minne ambayo ni: muhula wa urasimi, muhula wa utasa, muhula wa urasimi mpya, na muhula wa sasa.

**Muhula wa Urasimi** ni kipindi maalumu kinachochukuliwa kuwa msingi wa kuwekwa kwa sheria au kanuni ya jambo fulani. Urasimi wa ushairi wa Kiswahili ulipata mashiko katika karne ya kumi na nane (1700-1800). Katika kipindi hicho, kulikuwa na tungo kama vile *Utenzi wa Hamziyya* (bin Uthman, 1690), *Utenzi wa Tambuka* (Bwana Mwengo, 1728), *Utenzi wa Al-Inkishafi* (bin Nasir, 1800) na *Utenzi wa Mwanakupona* (Mwanakupona bint Mshamu, 1858). Tungo hizi zilitanguliwa na tungo zilizohusu simulizi za Fumo Liyongo na zikafuatiwa na tungo za Muyaka bin Haji. Baada ya hapo, ulifuatia ukame wa tungo kwa kipindi cha takribani miongo mitano (1885 - 1945). Kulikuwa na tungo chache; ndiyo maana muhula wa pili unaitwa **muhula wa utasa**. Sababu za ukame huu ni pamoja na matukio ya vita yaliyotokea ulimwenguni. Baada ya hapo, ukafuatia **muhula wa urasimi mpya** ambapo kulikuwa na watunzi kama vile Shaaban Robert, Kaluta Amri Abedi na Mathias Mnyampala. Huu ni muhula ulioshuhudia kuimarishwa kwa kanuni za utungaji wa ushairi wa Kiswahili kama vile *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (Abedi, 1954). Kisha, ulifuatia **muhula wa sasa**. Muhula huu ulianza wakati mataifa ya Afrika Mashariki yalipopata uhuru kutoka kwa wakoloni. Hiki ni kipindi kilichokuwa na wasomi wengi wa ngazi ya chuo kikuu waliojihusisha na utungaji, uhakiki na utafiti kuhusu masuala ya fasihi, ukiwamo ushairi. Hali hii mpya ilisababisha kuwapo kwa fikra mpya katika ushairi wa Kiswahili; ndipo ulipoibuka mjadala kuhusu ushairi usiofuata urari wa vina na mizani. Mjadala huo hujulikana kama **Mgogoro wa Ushairi** ambao umeelezwa kwa urefu katika kitabu cha Mulokozi na Kahigi (1982).

FOR ONLINE READING ONLY

### Vipera vya ushairi andishi

Ushairi andishi umegawanyika katika vipera vitatu. Vipera hivyo ni mashairi, tenzi na ushairi wa maigizo.

#### (a) Mashairi

Kuna mitazamo miwili inayohusu mashairi: mtazamo wa kimapokeo na mtazamo wa kisasa.

#### Mtazamo wa kimapokeo

Huu ndio mtazamo wa awali kuhusu mashairi ya Kiswahili. Wafuasi wa mtazamo huu wanasisitiza mambo yafuatayo: kanuni za urari wa vina na mizani, na lugha nzito ya mkato. Urari wa vina na mizani hulifanya shairi liimbike kwa urahisi kwa mahadhi yanayofahamika. Tazama mfano wa beti zifuatazo:

**Maisha**

*Maisha kitendawili, kitegue kwa busara,*
*Uitulize akili, huku ukiwa tohara,*
*Uhimili kila hali, yaweza kwako kung'ara,*
*Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.*

*Maisha kama bahari, yenda mpera mpera,*
*Vyovyote uwe tayari, kwa kujiweka imara,*
*Na kumuomba Kahari, akunyooshee dira,*
*Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.*

*Maisha ni kujituma, ili uipate tira,*
*Ushughulike kulima, au kuunda minara,*
*Mwiko kujiweka nyuma, utakumbwa na idhara,*
*Tukiimudu subira, maisha hayatuwengi.*

*Diwani ya Tunzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein (Juma (Mwana wa Nyasa), 2016).*

FOR ONLINE READING ONLY

Shairi hili lina mizani linganifu. Kila mshororo una mizani kumi na sita na vina vinavyofanana mwishoni mwa kila mshororo kwa shairi zima. Vina vya kati vinafanana katika kila ubeti. Kila ubeti umeundwa na mistari minne, ambapo huu ni muundo wa *tarbia*.

**Mtazamo wa kisasa au masivina**

Huu ni mtazamo wa wanamabadiliko wanaodai kwamba si lazima shairi liwe na urari wa vina wala ulinganifu wa mizani. Mtazamo huu ulianza mwishoni mwa miaka ya 1960 na kushadidiwa mwanzoni mwa miaka ya 1970. Wafuasi wa mtazamo huu ni Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi na Jared Angira. Wafuasi wengine ni Mugyabuso Mulokozi, Kulikoyela Kahigi, Said Ahmed Mohamed na Theobald Mvungi. Kulikoyela Kahigi na Mugyabuso Mulokozi wameandika *Mashairi ya Kisasa* (1973), *Malenga wa Bara* (1976) na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1982), Said Ahmed Mohamed ameandika diwani kadhaa zikiwamo '*Sikate Tamaa* (1983) na *Kina cha Maisha* (1984).

Wafuasi wa mtazamo huu wanaamini kuwa maudhui yanaweza kuwasilishwa bila kujikita katika sheria za vina na mizani. Wanadai kuwa, kama ambavyo mabadiliko yanatokea katika nyanja nyingine, ni lazima pia yatokee katika ushairi. Ikumbukwe kwamba, wenye mtazamo huu hawapingi kanuni za wanamapokeo, ila wamepanua wigo wa mashairi. Kwa mfano, zaidi ya nusu ya mashairi yaliyomo katika *Diwani ya Malenga wa Bara* (Kahigi na Mulokozi, 1976) ni ya kimapokeo. Wanausasa wanatilia mkazo matumizi ya lugha kuliko muundo wa shairi. Tazama mfano wa shairi la kisasa la "Kuchambua Mchele":

*Habari zilifika kutoka Arusha,*
*Tukaanza kuchambua mchele wa Ujamaa,*
*Macho mbele, macho pembeni tukitoa mchanga,*
*Tukafanya kaburi dogo la mchanga.*

*Tukaanza kutoa chenga, moja moja,*
*Vidole vikafanya kazi kama cherehani,*
*Usiku na mchana; macho yakauma,*
*Tukafanya kichuguu kidogo cheupe.*

*Kichomi (Kezilahabi, 1988)*

FOR ONLINE READING ONLY

Ukichunguza beti hizi mbili, utaona kwamba hakuna mizani linganifu wala urari wa vina. Kilichozingatiwa ni uteuzi wa maneno wenye kujenga picha na kumvutia msomaji au msikilizaji.

Wanausasa wanasisitiza mshairi awe na uhuru katika kutunga mashairi, na kueleza mawazo yake bila kubanwa na kanuni za wanamapokeo. Kitu cha msingi katika shairi ni mpangilio wa maneno, lugha ya picha au taswira, tamathali za semi, hisia za kishairi na ujumbe.

**(b) Tenzi**

Dhana ya tenzi imekwishaelezwa katika kipengele cha fasihi simulizi. Mambo machache ya kuyaongezea katika kipengele hiki ni kwamba, mara nyingi, tenzi huanza na dua, ambapo mwandishi humwomba Mungu amwongoze katika uandishi wake. Kwa kawaida, tenzi huwa na beti nyingi kuliko shairi la kawaida, lakini tenzi nyingi ni fupi kuliko tendi.

Beti za utenzi zinatakiwa ziwe hamsini na kuendelea. Hata hivyo, urefu wa utenzi hutegemea uzito wa maudhui na ujuzi wa mwandishi. Aghalabu, mstari wa utenzi huwa nusu ya mshororo wa shairi la kimapokeo. Hivyo, utenzi huwa na mizani minane. Vilevile, vina katika mishororo mitatu ya kwanza, hufanana lakini mshororo wa mwisho huwa na kina tofauti. Kina hiki ambacho huitwa bahari hakibadiliki katika utenzi mzima. Tazama mfano katika baadhi ya beti za utenzi ufuatao:

**Utenzi wa hati**

1. *Leo nataka binti,*
*Ukae juu ya kiti,*
*Ili uandike hati,*
*Ndogo ya wasia.*

2. *Mimi kwako ni baba,*
*Hati hii ya huba,*
*Andika iwe akiba,*
*Asaa itakufaa.*

FOR ONLINE READING ONLY

3. *Bado ungali kijana,*
*Na dunia ngumu sana,*
*Kukufunza kukuona,*
*Ni jambo welekea.*

*Maisha Yangu na Baada ya miaka Hamsini* (Robert, 1966: 6)

Beti za hapo juu zinaonekana wazi kuwa zimeundwa na mishororo minne. Kina cha mshororo wa mwisho "a" ni tofauti na vina vya mishororo mingine mitatu katika beti zote.

**Ushairi wa maigizo**

Huu ni utanzu mmojawapo wa ushairi wa Kiswahili. Utanzu huu tunaweza kuuweka katika michepuo miwili ambayo ni ngonjera na ushairi wa kidrama.

**(i) Ngonjera**

Ngonjera ni aina ya ushairi andishi ambao huhusisha mabishano ya pande mbili. Upande unaojua na ule usiojua jambo fulani. Kwa hiyo ushairi wa ngonjera huandikwa kidayalojia ukihusisha pande mbili. Lengo kuu ni kuonesha udhaifu wa hoja kinzani kwa kuzikosoa hoja hizo ili, hatimaye, hoja zilizolengwa zionekane kuwa na ushawishi mkubwa. Tazama mfano ufuatao wa ushairi wa beti chache za ngonjera:

**Ngonjera ni kitu gani?**

**MDADISI**

*Ngonjera ni kitu gani, nasikia kila mara,*
*Yatamkwa midomoni, tena mbele ya hadhara,*
*Je, maana yake nini, nami nipate busara,*
*Maana yake ngonjera, nambie nami nijue.*

**JAWABU**

*Ngonjera zina kiini, cha mafunzo ya busara,*
*Mafunzo yenye kipini, cha kuamsha fikira,*
*Za mawazo akilini, na kugeuza majira,*
*Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi.*

FOR ONLINE READING ONLY

**MDADISI**

*Ni mafunzo yapi hayo, ya hekima na ubora?*
*Yatiayo wangu moyo, kwa jitihada na ghera,*
*Ufanisi yaletayo, ya kugeuza majira,*
*Maana yake ngonjera, nambie nami nijue.*

**JAWABU**

*Mafunzo yatolewayo, kwa usemi wa hadhara,*
*Mema yachangamshayo, kwa tabasamu ya sura,*
*Ni ghibu itumikayo, kwa fikira na busara,*
*Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi.*

*Ngonjera za Ukuta: Kitabu cha Kwanza (Mnyampala, 1970:5)*

**(iii) Ushairi wa kidrama**

Huu ni ushairi unaotumiwa katika baadhi ya tamthiliya kama mtindo mmojawapo wa kuandika mazungumzo ya wahusika. Hivyo, hauwezi kutenganishwa na fani ya tamthiliya (Mulokozi, 2017). Ufuatao ni mfano wa ushairi huu:

**Mwanamke**

*Ndugu zangu, pulikeni ndugu zangu*
*Sasa si kama zamani*
*Sasa umetawala uwazi*
*Uwazi na utambuzi*
*Tusipigwe na bumbuwazi*
*Tusijisabilie kirahisi*
*Kwa ndoa yenye wasiwasi!*
*Mume mwenyewe kumwakisi*
*Bali hukufanya kisisi*
*Ukanipa mchumba mwenye ukakasi...*

FOR ONLINE READING ONLY

**Mfalme:** *Mwenzako lakini kakukosa nini?*
*Mwenzako kakufanya nini?*
*Mimi bado sijaamini*
*Kwa kweli baya mimi sijalibaini*
*Basi jambo hilo lanikata maini*
*Na kunivunjia matumaini*
*Mbona unaivunja ihsani*
*Yake sisi tul'omwamini*

*0Posa za Bikisiwa* (Mohamed, 2013)

Kwa jumla, kuna sifa mbalimbali za kisanaa zinazoutofautisha ushairi na tanzu nyingine za riwaya pamoja na tamthiliya.

## Zoezi la 2.2

1. Soma kauli hizi mbili kisha jibu maswali (a) na (b) yanayofuata:

   (a) "Katika kitabu hiki, tungo za Euphrase Kezilahabi, Kulikoyela Kahigi, Mulokozi na wengineo watungao tungo tutumbi zisizokuwa na sanaa yoyote nimezitupa pembeni … Muundo wa mashairi yote yaliyomo kitabuni humu ni ya asili ya Kibantu. Kila utungo wa shairi umefungika upande wa mistari; umefungika upande wa vina; ni lazima mistari iwe na vina; umefungika upande wa mizani; ni lazima kila mstari uwe na idadi sawa ya mizani. Mashairi yote yaimbwe; yaweza pia kusomwa au kusemwa tu. Tungo zisizotimiza yote hayo si mashairi."

   *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka (Mayoka, 1986)*

   (b) Washairi wa mapokeo, sasa wacheza lala salama,

   Katika mionzi hafifu, ya jua machweoni,

   Na mahadhi yagaagaa, juu ya bahari ya utenzi.

FOR ONLINE READING ONLY

Yameshindwa chini kuzama, kwenye kina cha urazini,

Nao wahenga vibandani, nje tena hawatoki,

Hakuna tena ngoma, ya kugeana kani,

Na ushairi umehama, umerudi upeponi,

Lakini majani makavu, sasa hayatingishiki,

Nayo madirisha ya nyumba, imara yamefungwa,

Waliomo ndani wahofu, hasira ya mizimu.

*Kichomi (Kezilahabi, 1988)*

(i) Toa maoni yako kuhusu hoja ya kuwa ili utungo uitwe shairi, sharti ukidhi vigezo vya kauli 1(a)

(ii) Tathmini ukweli wa kinachosemwa katika kauli (b) ukihusianisha na hali halisi ya sasa ya ushairi wa Kiswahili.

2. Soma shairi la kisasa, kisha bainisha vipengele mbalimbali vya ushairi.

3. Soma beti ishirini (20) za utenzi uupendao kisha chambua vipengele vya fani na maudhui.

4. Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Amina**

1. Amina umejitenga, kufa umetangulia,
Kama ua umefunga, baada ya kuchanua,
Nakuombea mwanga, peponi kukubaliwa,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

2. Nilitaka unyanyuke, kwa kukuombea dua,
Sikupenda ushindike, maradhi kukuchukua,
Ila kwa rehema yake, Mungu amekuchagua,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Majonzi hayaneneki, kila nikikumbukia,
Nawaza kile na hiki, naona kama ruia,
Mauti sijasadiki, kuwa mwisho wa dunia,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

*Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (Robert, 2003:5)

Maswali

(a) Andika ujumbe wa shairi.
(b) Bainisha mloto wa ubeti wa pili.
(c) Bainisha vina vya kati na vya mwisho vya ubeti wa pili.
(d) Orodhesha utao wa ubeti wa kwanza na ukwapi wa ubeti wa tatu.
(e) Orodhesha mizani ya uketo wa kibwagizo cha shairi hili.

**Shughuli ya 2.10**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, jadili dhana na historia ya hadithi fupi ya Kiswahili.

### Hadithi fupi

Hadithi fupi ni simulizi za kubuni zinazosawiri tukio, tabia, mgogoro au kipengele cha maisha kwa ufupi. Hadithi za namna hii huwa na tukio moja au mawili na hutumia mawanda finyu. Kwa kawaida, hadithi fupi haina uchangamano mkubwa wa matukio, na hutumia wahusika wachache.

### Historia ya hadithi fupi

Chimbuko la utanzu wa hadithi fupi ni hadithi simulizi na andishi zinazopatikana katika lugha nyingi duniani. Baadhi ya fani zilizochangia kuchipuka kwa hadithi fupi ni ngano, hekaya, visa, michapo na tendi. Kuzuka kwa fani ya hadithi fupi huko Marekani na Ulaya katika karne ya 19 kulisaidiwa sana na kuchipuka kwa utamaduni wa kusoma magazeti, kwani visa vingi vilichapishwa katika magazeti hayo. Uhusiano huu kati ya hadithi fupi na magazeti au majarida bado upo hadi leo.

Historia ya hadithi fupi haitofautiani sana na historia ya riwaya ya Kiswahili. Visa vya mwanzo vilivyochapishwa kwa Kiswahili ni mkusanyiko wa hekaya na ngano. Baadhi ya hadithi hizo ni zile zinazopatikana katika vitabu vifuatavyo:

FOR ONLINE READING ONLY

*Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870), *Hekaya za Abunuwasi* (1928) na *Alfu Lela Ulela* (1928). Hadithi hizi zilikuwa za kimapokeo na zenye kuingiliana na fasihi simulizi. Visa halisi vya kwanza katika hadithi za lugha ya Kiswahili vilianza miaka ya 1950 katika magazeti ya *Mamboleo*, *Mwafrika*, *Baraza*, *Nyota Afrika* na *Kiongozi*. Katika miaka ya 1960, visa hivi vilianza kuchapishwa kwenye vitabu. Baadhi ya watunzi mashuhuri wa hadithi fupi za Kiswahili ni Gabriel Ruhumbika, Alex Banzi, Joseph Kiimbila, Kyallo Wamitila na Owen Onyango. Baadhi ya mikusanyiko ya hadithi fupi iliyochapishwa ni *Misingi ya Hadithi Fupi* (Msokile, 1992), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (Mbatiah, 2000), *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*, (MacOnyango, 2006), *Mizungu ya Manabii na Hadithi nyingine* (Habwe, 2010), *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine* (Wamitila, 2010)

**Sifa za hadithi fupi**

Hadithi fupi huwa na sifa au kaida zinazoitofautisha na riwaya. Nazo ni kuwa na:

(i) urefu wa kusomeka kwa mkao mmoja. Kwa kawaida hadithi fupi haizidi maneno 10,000;

(ii) muundo sahili;

(iii) wahusika wachache ambapo, aghalabu, mhusika mkuu huwa mmoja au wawili. Wahusika hawa hawakui kitabia wala hawakui kulingana na maendeleo ya kisa;

(iv) dhamira chache ikilinganishwa na riwaya. Mara nyingi, huwa na dhamira kuu moja katika kisa kikuu kimoja; na

(v) mawanda finyu ya kiwakati na kijiografia.

**Aina za hadithi fupi**

Hadithi fupi huainishwa katika makundi mawili: *hadithi fupi dhati* na *hadithi fupi pendwa.* Hadithi fupi dhati huwekwa katika makundi yafuatayo: hadithi fupi za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kifalsafa.

Hadithi fupi za kijamii huzungumzia masuala mbalimbali ya kijamii kama vile ndoa, jinsia, mapenzi na malezi. Mifano ya hadithi fupi za kijamii ni: "Uwike Usiwike Kutakucha" (Ruhumbika), na "Siri ya Bwanyenye" (Mulokozi) zote hizi zimo katika Msokile (1992). Nyingine ni "Damu Nyeusi" (Walibora, 2007) na "Kijana Yule" (Mohamed, 2010).

FOR ONLINE READING ONLY

Hadithi fupi za kisiasa ni zile zinazohusu masuala ya kisiasa. Mifano ya hadithi hizo ni "Wali wa Ndevu" (Ruhumbika, 1974), "Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani", "Magwanda Kubilya na Vyama Vingi" na "Mayai Waziri wa Maradhi" (Kezilahabi katika Msokile, 1992).

Hadithi fupi za kiutamaduni zinahusu masuala ya mila na desturi. Mifano ya hadithi fupi za kundi hili ni *Tamaa Mbele* (Banzi, 1970) na "Siku ya Mganga" (Mpilipili, katika Wamitila, 2012).

Hadithi fupi za kifalsafa huzungumzia tafakuri kuhusu masuala mazito yanayomzunguka mwanadamu na ulimwengu wake. Mifano ya hadithi fupi za kifalsafa ni "Wasubiri Kifo" (Kezilahabi, katika Msokile, 1992) na "Mchakamchaka wa Maisha" (katika Komba, 1978).

Hadithi fupi pendwa ni zile ambazo huzungumzia masuala yanayosisimua kama vile mapenzi, matukio yenye uajabu ajabu, mauaji na upelelezi. Mifano ya hadithi hizi ni "Sadiki Ukipenda" (Mohamed, 2002)

Pamoja na uainishaji wa hadithi fupi uliofanywa hapo juu, ni vigumu kuwa na hadithi fupi yenye maudhui ya mwelekeo mmoja. Hivyo, hadithi fupi moja inaweza kubeba maudhui ya aina mbalimbali.

**Shughuli ya 2.11**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, soma hadithi fupi zisizopungua nne (4) kisha, bainisha aina zake na chambua maudhui ya hadithi hizo.

**Shughuli ya 2.12**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, fafanua dhana na historia ya tamthiliya.

### Tamthiliya

Tamthiliya ni mchezo ulioandikwa ili utendwe jukwaani au usomwe, kwa malengo mbalimbali. Tamthiliya hujengwa na wahusika na migogoro iliyomo katika mchezo. Migogoro ndiyo hukuza mwendo wa tamthiliya kwa kutumia visa ambavyo hutendwa na wahusika mbalimbali. Wahusika huzungumza na kutenda matendo mbalimbali kisanii.

### Historia ya tamthiliya

Tamthiliya haikuwapo nchini Tanzania kabla ya ujio wa Waingereza. Ujio wao ulileta drama ambayo ndiyo chanzo cha tamthiliya. Drama iliingizwa shuleni na Waingereza kwa lengo la kuwaburudisha na kuwakumbusha utamaduni wao, hasa

FOR ONLINE READING ONLY

baada ya saa za kazi ambapo wengi wa walimu walikuwa Waingereza. Ilikuwa rahisi kuanzisha vikundi vya drama shuleni kwa sababu shule nyingi zilikuwa za bweni; na hivyo, wanafunzi walipatikana muda wote. Vilevile, wanafunzi hao walifahamu vizuri lugha ya Kiingereza. Tamthiliya nyingi zilizoigizwa ni zile zilizoandikwa na Waingereza. Miongoni mwa tamthiliya hizo ni *The Merchant of Venice* (Shakespeare, 1596) na *Julius Caesar* (Shakespeare, 1599). (Kwa kuwa tamthiliya hizi hazikuwa na uhusiano na mazingira ya Kitanzania, Watanzania walioziigiza waliona ni kiburudisho tu yaani tamthiliya hizo hazikuwa na maana kubwa kwao. Kadiri muda ulivyopita, baadhi ya Watanzania walivutika na sanaa ya tamthiliya. Hata hivyo, hawakuwa na ujuzi wa kuandika tamthiliya kama zile za Waingereza. Miaka ya mwanzo baada ya uhuru, maudhui hayakubadilika mpaka lilipotangazwa Azimio la Arusha mwaka 1967. Maudhui ya tamthiliya ya baada ya Azimio la Arusha yalichukua sura mpya kwa kutangaza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kwa kuunga mkono au kukosoa.

Tamthiliya za mwanzo ziliathiriwa sana na vichekesho. Pia, ziliathiriwa na tamthiliya za Kiingereza. Watunzi walitunga tamthiliya zilizofanana kimaudhui na zile za akina Shakespeare. Kwa mujibu wa Mazrui (2007) na Mulokozi (2017), tamthiliya za mwanzo za Kiswahili zilitungwa nchini Kenya. Mifano ya tamthiliya hizo ni *Mgeni Karibu* (Hyslop, 1957), *Nakupenda Lakini* (Kuria, 1957) na *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (Ngugi, 1961). Kwa upande wa Tanzania, miaka ya 1960, tamthiliya za Kiingereza zilitafsiriwa. Miongoni mwa tamthiliya hizo ni zile za Shakespeare za *Juliasi Kaisari* (Nyerere, 1964), *Mabepari wa Venisi* (Nyerere, 1969), *Tufani* (Mushi, 1969) na tamthiliya ya Kiyunani ya *Mfalme Edipode* (Mushi, 1969). Tamthiliya nyingine ni zile zilizoandikwa na Waafrika. Zilizotafsiriwa ni *Mtawa Mweusi* (wa Thiong'o, 1970), *Masaibu ya Ndugu Jero* (Yahaya, 1974) na *Nitaolewa Nikipenda* (wa Thiong'o na wa Mirii, 1982).

Kuanzia miaka ya 1960, watunzi wa Kitanzania walianza kutunga tamthiliya za Kiswahili kwa ajili ya Watanzania. Miongoni mwa watunzi waliojitokeza ni Ebrahim Husein ambaye tamthiliya yake ya kwanza ni, *Wakati Ukuta* (1967), ilishinda na kupata tuzo katika mashindano. Tamthiliya nyingi zilizotungwa miaka ya 1960 ziliigizwa tu shuleni na katika kumbi za maonesho lakini hazikuchapishwa.

Tamthiliya nyingi za Kiswahili zilichapishwa kama matokeo ya kuhitimu kwa watu wengi katika fani ya sanaa za maonesho katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, yalikuwa ni matokeo ya kuanzishwa kwa mashindano ya uigizaji miaka ya 1970 - 1990. Baadhi ya tamthiliya zilizochapishwa ni *Kinjekitile* (Hussein,

FOR ONLINE READING ONLY

1969), *Mashetani* (Hussein, 1971), *Hatia* (Muhando, 1972), *Tambueni Haki Zetu* (Muhando, 1973), *Aliyeonja Pepo* (Topan, 1973) na *Pambo* (Muhando, 1975). Nyingine ni *Sundiata* (Mbogo, 1975), *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (Hussein, 1976), *Machozi ya Mwanamke* (Ngozi, 1977), *Mukwava wa Uhehe* (Mulokozi, 1979), *Arusi* (Hussein, 1980), *Tendehogo* (Semzaba, 1984), na *Giza Limeingia* (Mbogo, 1980). Vilevile, kulikuwa na *Njia Panda* (Muhanika, 1981) *Tone la Mwisho* (Mbogo, 1981), *Nguzo Mama* (Muhando, 1982), *Lina Ubani* (Muhando, 1984), *Kwenye Ukingo wa Thim* (Hussein, 1988), *Pungwa* (Mohamed 1988), *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* (Semzaba, 1988) *Kivuli Kinaishi* (Mohamed 1990), na *Morani* (Mbogo, 1993).

Tamthiliya zimeendelea kutungwa zikiakisi mabadiliko ya mifumo ya maisha ya jamii ya wakati huo. Mathalani, tamthiliya kama Ushuhuda wa Mifupa (Ngozi, 1990) na *Kilio Chetu* (Medical Aid Foundation, 1995) zimejadili kuhusu maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI katika jamii.

Miaka ya karibuni, tamthiliya ya kihistoria imeanza kushamiri tena baada ya kupotea kwa takribani miongo mitatu tangu enzi za *Kinjekitile* na *Mukwava wa Uhehe*. Mtunzi aliyejipambanua zaidi katika mkondo huu ni Emmanuel Mbogo ambaye ametoa tamthiliya nne katika miaka ya karibuni. Tamthiliya hizi zinaongeza idadi ya tamthiliya zake nyingine mbili za kihistoria alizozichapisha hapo kabla. Nazo ni *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Sundiata* (1994), *Fumo Lyongo* (2009), *Sadaka ya John Okello* (2015), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) na *Shujaa Mirambo* (2021). Tamthiliya hizo, mbali na kupevua mkondo wa tamthiliya ya kihistoria, zinadhihirisha namna historia inavyoweza kutumika kisanaa kusawiri migogoro na masuala yenye umuhimu katika jamii ya leo.

**Aina za tamthiliya**

Tunaweza kuainisha tamthiliya kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile kigezo cha maudhui, kusudio, dhima, muktadha wa utendaji, hadhira lengwa na mbinu za kisanii. Kila kigezo hutupatia aina mahususi za tamthiliya. Mathalani, kigezo cha hadhira lengwa kinapotumika, huweza kutupatia aina zifuatazo: tamthiliya ya watoto, tamthiliya ya vijana, tamthiliya ya watu wazima, tamthiliya ya wanawake, tamthiliya ya wanaume, tamthiliya ya miungu na tamthiliya ya waumini wa dini fulani. Uainishaji uliotumika katika kitabu hiki umetumia kigezo cha mbinu za kisanaa. Kwa kuzingatia kigezo hicho, tunapata aina zifuatazo: tanzia, ramsa, tanzia ramsa, na melodrama.

FOR ONLINE READING ONLY

**(a) Tanzia**

Tanzia ni tamthiliya zenye tukio au matukio ya kuhuzunisha; nayo huhusika na mambo yenye uzito kifikra na kihisia, katika maisha ya binadamu. Mhusika mkuu ambaye kwa kawaida ni mtu maarufu mwenye kupewa sifa nyingi zinazovutia, hukabiliwa na shida au tatizo. Tatizo hilo ni kama lile linaloweza kumkabili mtu yeyote. Ijapokuwa mhusika huyo hujitahidi kulitatua tatizo hilo, hali ya ulimwenguni na tabia ya kibinadamu humfanya asiweze kufaulu, na mwishowe hushindwa. Kwa hiyo, mwisho wa tamthiliya hizi ni masikitiko, maanguko na hasara kwa mhusika mkuu au jamii. Mfano wa tanzia ni tamthiliya ya *Kinjeketile* (Hussein, 1969) na *Kifo Kisimani* (wa Mberia, 2001).

**(b) Ramsa**

Ramsa, ambayo hujulikana pia kama komedia au futuhi, hukusudia kufurahisha au kuchekesha, na huwa na mwisho mwema. Sifa ya kufurahisha na kuchekesha haimaanishi kwamba tamthiliya za aina hii hazina maudhui mazito. Tamthiliya hizi hushughulikia masuala mbalimbali ya msingi kama vile uzembe, uzalishaji mali, siasa, mapenzi na ndoa. Utani, mzaha na kejeli hutumika katika kuchekesha. Kupitia uchekeshaji huo, jamii, watawala na watu binafsi hukosolewa. Mhusika mkuu wa ramsa si lazima awe mtu maarufu. Anaweza kuwa mtu wa kawaida au anaweza kuwa mtu wa nasaba duni, lakini hubeba matendo ya ucheshi yanayobeba maana nzito. Mhusika huyu akifanikiwa, wasomaji au watazamaji hufurahi. Mfano mzuri wa ramsa ni tamthiliya ya *Mfalme Juha* (Topan, 1971) na *Aliyeonja Pepo* (Topan, 1973).

**(c) Tanzia ramsa**

Hii ni tamthiliya yenye mseto wa maudhui ya kuhuzunisha na kufurahisha. Mifano ya tamthiliya hizi ni *Kaptula la Marx* (Kezilahabi, 1999), *Pambo* (Muhando, 1975), *Masaibu ya Ndugu Jero* (Soyinka, [mf.] Yahaya, 1974), *Mabepari wa Venisi* (Shakespeare [mf.] Nyerere, 1969), *Wakati Ukuta* (Hussein, 1967) na *Amezidi* (Mohamed, 1995).

**(d) Melodrama**

Melodrama ni tamthiliya yenye matumizi mengi ya muziki na uimbaji wa nyimbo. Inafanana sana na tanzia ingawa, mara nyingi, nguli wa melodrama huibuka na ushindi. Dhamira za melodrama huzungumzia mvutano kati ya wema na uovu au ubaya. Matukio yake husisimua sana na mwendo wa msuko wake huwa wa harakaharaka. Wahusika wake huvutia lakini hawana sifa za kishujaa. Aghalabu, mwishoni, mhusika mwema huweza kupata ushindi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Tofauti baina ya michezo ya fasihi simulizi na tamthiliya za fasihi andishi**

Michezo ya fasihi simulizi hutofautiana na tamthiliya za fasihi andishi kwa vipengele vifuatavyo:

**(a) Utunzi wa maonesho**

Mara nyingi mtungaji wa mchezo na mwigizaji wa tamthiliya huwa tofauti. Maneno ya mtunzi ni lazima yakaririwe na waigizaji jinsi yalivyo au kama madokezo ya lazima. Kwa upande wa fasihi simulizi, mara kadhaa watunzi wa mchezo ndio wachezaji. Maneno na vitendo ni vyao wenyewe na wakati mwingine hubuniwa papo kwa papo.

**(b) Maandalizi**

Tamthiliya hupitia maandalizi kadhaa kama vile kufanya mazoezi mengi kabla ya kuigizwa jukwaani. Pia, jukwaa na vyombo vitakavyotumika sharti viandaliwe mapema. Kwa ujumla, igizo lolote ili livutie watazamaji linapaswa kufanyiwa maandalizi mazuri. Kwa upande wa maandalizi drama zinazotokana na vitabu na zile zinazotungwa tu kichwani lazima ziandaliwe vizuri.

**(c) Shabaha**

Shabaha kuu katika drama na maigizo ya kawaida ni kuelimisha, kuburudisha na wakati mwingine ni biashara kwa sababu watu hununua tamthiliya au huuza kazi hizo katika vituo vya runinga na redio. Vilevile, maigizo huoneshwa ukumbini ambapo watazamaji hupaswa kulipia.

**Shughuli 2.13**

Kwa kutumia vyanzo vya maktabani, soma tamthiliya mbili au zaidi, kisha bainisha aina ya tamthiliya hizo.

**Shughuli 2.14**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, jadili dhana na aina za riwaya.

**Riwaya**

Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni itumiayo lugha ya kinathari (lugha ya mjazo) yenye uchangamani wa visa, wahusika, mandhari na dhamira. Mara nyingi vipengele hivyo huakisi maisha ya jamii inayohusika. Hivyo, riwaya huweza kutoa picha ya jumla ya maisha ya mtu kutoka nyumbani (mtu binafsi) hadi kiwango cha taifa na hata dunia nzima (Mohamed, 1995; Madumulla, 2009; na Senkoro, 2011).

FOR ONLINE READING ONLY

**Sifa za riwaya**

Kuna sifa mbalimbali za riwaya. Kwa kawaida riwaya huwa:

(a) ndefu ikilinganishwa na tanzu nyingine. Urefu wa riwaya ya *Mungu Hakopeshwi* (Baharoon, 2021) kwa mfano, ni tofauti na ule wa hadithi fupi ya *Uwike Usiwike Kutakucha* (Ruhumbika, 1978);

(b) na visa changamani, yaani huwa na visa zaidi ya kimoja, ambapo kisa kikuu hujengwa na visa vidogo;

(c) na wahusika wengi na waliokuzwa. Kutokana na riwaya kuwa na visa vingi, basi huwa na wahusika wengi ambao humwezesha mwandishi kukidhi haja hii;

(d) na mandhari pana na huendelezwa kikamilifu. Kwa kuwa riwaya hushughulikia mawazo mengi, hujishughulisha na vipengele vingi vya maisha ambavyo hupatikana katika nyakati na mahali tofauti kama vile shuleni, mijini, vijijini, nyumbani na barabarani. Ili kushughulikia mazingira mapana, simulizi hutumia kipindi kirefu cha wakati ikilinganishwa na kazi kama vile za hadithi fupi ambazo huweza kuchukua kipindi kifupi tu kukamilika;

(e) na migogoro iliyokuzwa zaidi kwa sababu mwandishi ana uhuru mkubwa wa kuiibua na kuieleza kwa kina;

(f) Hutumia lugha ya kisanii ya kinathari / lugha ya mjazo; na

(g) Kwa sababu ya urefu na upana wake, riwaya huwa na uwezo wa kubeba au kutomelea tanzu nyingine (kama vile barua, insha, shairi, wimbo au igizo) bila matatizo. Mathalani, katika riwaya ya *Kiu ya Haki* (Mwanga,1983) mwandishi ametumia hadithi ndani ya hadithi. Hadithi mojawapo ni ile ya Mzee Fundisha anayesimulia yaliyompata alipovamiwa na polisi nyumbani kwake na kulazimishwa kutoa rushwa ya Sh. 2,000 ingawa hakuwa na hatia. Vilevile, kuna hadithi ya Sikujua, anayesimulia yaliyompata miaka kumi iliyopita wakati yeye na Pondamali wakifanya biashara ya kubadilisha fedha.

FOR ONLINE READING ONLY

**Historia ya riwaya**

Riwaya ni utanzu wa hivi karibuni zaidi ukilinganishwa na ushairi na tamthiliya. Inadaiwa kwamba riwaya ilipata umbo ililonalo hivi sasa katika karne ya 18 huko Ulaya. Riwaya ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kiutamaduni na viwanda. Ukoloni na "uvumbuzi" viliumba hali zilizohitaji kuelezwa kwa mawanda mapana kuliko ilivyowezekana katika ngano na hadithi fupi. Uchangamani wa maisha katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, utamaduni na uchumi ulihitaji kuwa na utanzu wa fasihi ulio na uchangamani kifani na kimaudhui pia. Kupanuka kwa usomaji, hasa wakati wa mapinduzi ya viwanda huko Uingereza, kuliwafanya waandishi waandike kazi ndefu kwa sababu walikuwapo wasomaji, hasa wanawake, waliokuwa wakibaki majumbani wakati waume zao wakiwa viwandani (Senkoro, 1984; Njogu na Chimerah, 1999; Madumulla, 2009).

Afrika ni miongoni mwa mabara yenye historia fupi zaidi ya riwaya, ambapo maandiko ya riwaya yalianza kujitokeza mwishoni mwa karne ya 19. Katika eneo la Afrika ya Mashariki, kazi za kinathari za kwanza hazikukidhi ubora wa usanii na ubunifu. Baadhi ya maandiko ya awali ni *Habari za Wakilindi* (el Ajjemi, 1885, 1907, 1962), *Tulivyoona na Tulivyofanya Uingereza* (Kayamba, 1933), *Mwaka katika Minyororo* (Sehoza, 1921) na *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1934). Vyote hivi vinaangukia katika kundi linaloendana na tawasifu au masimulizi ya wasafiri. Kwa hakika, kiwango cha usanifu wa vitabu hivi ni cha chini.

Nchini Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazoendelea, nathari andishi ya kibunifu ni fani ambayo ilichelewa kuja. Nathari bunifu simulizi, kama vile hadithi, hekaya na ngano zilizosimuliwa kwa mdomo ndizo ambazo zilizotawala ndani ya jamii.

Kwa upande wa fasihi andishi, kwa kipindi kirefu, maandiko ya fani ya ushairi, hususani tenzi za Kiswahili katika hati ya Kiarabu, ndiyo yaliyotamba katika eneo la Pwani ya Afrika ya Mashariki. Maandiko ya kinathari yalianza baada ya ujio wa wamisionari. Nathari simulizi inayojulikana kuandikwa na wenyeji ni *Habari za Muma* (bin Hemed, 1880), nayo ilichapishwa mwaka 1935 katika *Mambo Leo*, gazeti la Kiswahili lililovuma wakati wa ukoloni wa Waingereza. Nathari nyingine ni ile ya *Habari za Wakilindi* iliyoandikwa na Abdallah bin Hemed bin Ali el Ajjemy mzaliwa wa Zanzibar kwa baba wa Kiarabu na mama wa Kihehe, na ambayo juzuu ya kwanza ilichapishwa mwaka 1894, ya pili mwaka 1904 na ya tatu mwaka 1907. Kitabu hiki kilihusu masimulizi ya Wasambaa. Kumbukumbu nyingine ni zile zilizohusu Lamu na ambazo zinasadikiwa kuwa ziliandikwa

FOR ONLINE READING ONLY

na Shaibu Faraji, na kuchapishwa na William Hichens (1928). Maandiko haya yalitokea wakati wa kipindi cha Wajerumani (Njogu na Chimerah, 1999).

Baada tu ya Vita vya Kwanza vya Dunia, Waingereza walijishughulisha zaidi na kuandika na kufasiri vitabu vya shule vya kiada na ziada. Baadhi ya vitabu hivyo ni: *Hadithi ya Allan Quartermain* (Haggard [mf.] Frederick Johnson, 1934), *Safari za Gulliver* (Swift, [mf.] Frederick Johnson, 1932), *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Haggard, [mf.] Edwin Brenn, 1929), *Alfu Lela Ulela* ([Waf.] Frederick Johnson na Edwin Brenn, 1929), na *Kisiwa Chenye Hazina* (Stevenson [mf.] Frederick Johnson, 1929). Maandiko haya yalikuwa maarufu hadi kufikia mwaka wa 1950 ambapo waandishi wazawa walianza kujitokeza kuandika nathari za kibunifu (bunilizi) kwa mfuatano wa kimikondo (Madumulla, 2009).

Riwaya ya Kiswahili iliendelea kukua na kubadilika sambamba na vipindi mbalimbali vya kihistoria nchini Tanzania. Katika kipindi cha miaka 1940 mpaka 1970, riwaya za aina mbalimbali ziliandikwa, zikiwamo za kitawasifu, kimaadili, kiutamaduni, na za kihalifu au kikachero. Kwa mfano riwaya za kimaadili, zina sifa za kifasihi simulizi ambazo ni matumizi ya dialojia, kutofungwa na wakati pamoja na matumizi ya balagha (chuku), ambayo hukipatia kitu sura, uwezo na nguvu isiyokuwa ya kawaida. Mifano ya riwaya hizi ni *Kusadikika* (Robert, 1991), *Kufikirika* (Robert, 1968) na *Adili na Nduguze* (Robert, 1952).

Riwaya za kiutamaduni zilisheheni maudhui yaliyosawiri tamaduni za jamii mbalimbali. Mfano mmojawapo ni riwaya ya *Kurwa na Doto* (Farsy, 1960) inayosawiri maisha ya watu wa visiwa vya Unguja na Pemba. Halikadhalika, kuna riwaya ya *Mzishi wa Baba ana Radhi* (Nkwera, 1967), inayoelezea maisha ya Wapangwa wa mkoa wa Njombe, wilayani Lubewa. Vilevile, kuna riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka, Ntulanalwo na Bulihwali* (Kitereza, 1980) ambayo inasawiri mila na desturi za jamii ya Wakerewe kabla ya kuja kwa wakoloni.

Riwaya za kihalifu au kikachero zilibeba maudhui ya uhalifu na upelelezi. Mifano mizuri ni riwaya za Muhammed Said Abdulla ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974) na *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976).

Baada ya uhuru, na hatimaye Azimio la Arusha kutangazwa, ziliibuka riwaya zenye maudhui yanayohusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika kipindi hiki, makundi mawili ya waandishi yalijitokeza kuandika riwaya kuelezea Azimio la Arusha. Kundi la kwanza liliuona ujamaa kwa jicho la ujadi. Kundi hili liliandika

FOR ONLINE READING ONLY

kazi zilizosawiri maisha yaliyopita. Mfano wa riwaya za kundi hili ni *Mtu ni Utu* (Mhina, 1971) na *Njozi za Usiku* (Seme, 1976). Kundi la pili ni lile lililouona ujamaa kwa jicho la matarajio kwamba kuna ujenzi wa jamii mpya itakayoishi vizuri kuliko jamii iliyokuwapo. Kwa hiyo, kundi hili liliandika kazi kwa shauku ya kueleza mabadiliko yatakayoletwa na vijiji vya ujamaa. Mfano wa riwaya hizo ni *Shida* (Balisidya, 1975) na *Ndoto ya Ndaria* (Ngomoi, 1976). Riwaya hizi zililenga kuonesha ubora wa maisha ya vijijini. Muundo wa riwaya hizi ni wa moja kwa moja, lugha nyepesi na wahusika wasio na utata.

Pia, katika kipindi hiki, walijitokeza waandishi walioandika riwaya kwa jicho la kiyakinifu. Riwaya za namna hii ziliyasawiri masuala ya kijamii kipembuzi. Mifano ya riwaya hizo ni *Kasri ya Mwinyi Fuad* (Shafi, 1978), *Kuli* (Shafi, 1979) na *Dunia Mti Mkavu* (Mohamed, 1979). Waandishi wa riwaya hizi wanaeleza mapambano dhidi ya umwinyi na ubepari. Katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, kwa mfano, kuna mvutano baina ya mamwinyi, watwana na watumwa. Pande hizi mbili zinakinzana na hatimaye, mikinzano inazaa mapinduzi. Kwa kiasi, waandishi hawa waliathiriwa na fikra za Ki-Marx (Senkoro, 1984).

Katika miaka ya 1980, liliibuka wimbi la uandishi wa riwaya pendwa. Riwaya hizi zilizuka kutokana na sababu za kiuchumi, ambapo uchumi wa Tanzania uliyumba kutokana na Vita vya Kagera, majanga kama ukame, pamoja na masharti magumu ya Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia. Waandishi wengi walianza kuandika riwaya pendwa kwa lengo la kujipatia fedha za haraka. Pia, zilizuka kampuni nyingi za uchapishaji nchini. Kampuni hizo zilirahisisha uchapishaji wa riwaya pendwa kwa haraka na kwa gharama nafuu. Soko la riwaya pendwa lilikuwa kubwa kutokana na maudhui yake kupendwa na watu wa rika zote. Aidha, waandishi ndio walikuwa wachapishaji na wauzaji wakuu wa riwaya hizo. Miongoni mwa riwaya hizo ni *Tutarudi na Roho Zetu* (Mtobwa 1987), *Roho Mkononi* (Rajab,1984), *Dimbwi la Damu* (Mtobwa, 1984), *Kikomo* (Musiba, 1980) na *Njama* (Musiba, 1981). Nyingine ni *Kijasho Chembamba* (Ganzel, 1980), *Ufunguo wa Bandia* (Rajab, 1974), *Jeraha la Moyo* (Kiango, 1974) na *Kwa Sababu ya Fedha* (Simbamwene, 1972).

Pia, katika kipindi hiki waandishi wengi waliandika riwaya zilizohakiki jamii. Riwaya hizi zilitokana na Azimio la Arusha kutokukidhi matarajio ya Watanzania. Wasanii waliandika riwaya kueleza maoni yao kuhusu viongozi walioaminika kuwaongoza wananchi kuyafikia malengo ya vijiji vya ujamaa. Viongozi waligeuka wasaliti, waroho, na wazembe huku wakiendekeza rushwa, uvivu, ulevi na ubadhirifu wa mali ya umma. Mfano wa riwaya za kipindi hicho

ni *Nyota ya Huzuni* (Liwenga, 1978), *Njozi Iliyopotea* (Mung'ong'o, 1979), *Sudi ya Yohana* (Chachage, 1981), *Kivuli* (Chachage, 1981), *Harusi* (Safari, 1984) na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1992).

Riwaya hizo za kihakiki zimeendelea kuandikwa mpaka miaka ya 2000. Riwaya hizi zimejadili upokezi na athari za soko huria lililotokana na sera za ubinafsishaji. Katika mfumo huu, njia kuu za uchumi zinamilikiwa na watu binafsi, wengi wao wakiwa si wazawa. Kwa hiyo, wazawa wameendelea kuishi maisha magumu kinyume na matarajio waliyokuwa nayo, baada ya uhuru, hususani baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Mifano ya riwaya zenye maudhui yanayohusiana na ubinafsishaji na soko huria ni *Almasi za Bandia* (Chachage, 1991) na *Makuadi wa Soko Huria* (Chachage, 2002).

Ikumbukwe kwamba hakuna mpaka bayana katika vipindi vilivyotajwa hapo juu. Kuna kazi za fasihi andishi zenye maudhui yanayohusu vipindi tofauti katika kipindi kimoja. Hivyo, si ajabu kukuta riwaya za kiuhakiki katika kipindi cha Azimio la Arusha; vivyo hivyo, riwaya pendwa zinajitokeza katika vipindi vyote. Pia, hali hii inaweza ikatokana na mhamo wa kutoka kipindi kimoja kwenda kipindi kingine. Katika kipindi cha mpito, kunakuwa na kazi za fasihi zinazozungumzia kipindi ambacho kinaelekea kufikia mwisho na nyingine zinakuwa na maudhui ya kipindi kilichopo au hata kijacho.

**Aina za riwaya**

Riwaya hugawanywa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Vigezo vilivyo maarufu ni vya kutazama fani na maudhui. Kifani, riwaya huainishwa kwa kuzingatia jinsi vipengele vya fani vinavyojitokeza. Kadhalika, kimaudhui, mgawanyo hutazama mambo yanayoongelewa katika riwaya inayohusika. Kigezo hiki cha maudhui ndicho kinachotumika katika kitabu hiki. Kwa kutumia kigezo hiki, kuna makundi makubwa mawili ya riwaya: riwaya dhati na riwaya pendwa.

**1. Riwaya dhati**

Riwaya dhati ni zile zinazochambua matatizo au masuala mazito ya kijamii, kutafuta sababu zake, athari zake na ikiwezekana ufumbuzi wake. Riwaya hizi hukusudiwa kumfikirisha msomaji kuhusu masuala mazito na si kumstarehesha tu. Riwaya dhati zimegawanyika katika aina mbalimbali. Aina hizo ni: riwaya za kijamii, kisaikolojia, sira, kiistiara, kingano, teti, chuku, kihistoria, kimaadili, kimapinduzi na kifalsafa. Pia, kuna riwaya za barua, vitisho na za watoto na vijalunga.

FOR ONLINE READING ONLY

### (a) Riwaya za kijamii

Hizi ni riwaya zinazosawiri maisha na matatizo ya kawaida ya kijamii. Matatizo hayo huweza kuwa ya kifamilia, kimahusiano, kitabaka, kisiasa na kiutamaduni. Maudhui mengine ni mgongano kati ya ukale na usasa, kati ya maisha ya mjini na ya vijijini na migogoro ya kifamilia. Wahusika wake, aghalabu, huwa halisi ambao wanapatikana katika jamii. Hivyo, huifanya riwaya iwe inaishi wakati wote, yaani haichuji. Aina hii ndiyo yenye idadi kubwa ya riwaya. Mifano ya riwaya za aina hii ni *Siku ya Watenzi Wote* (Robert, 1968), *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971), *Titi la Mkwe* (Banzi, 1972) na *Nyota ya Rehema* (Mohamed, 1978).

### (b) Riwaya za kisaikolojia

Hizi ni riwaya zinazosaili nafsi ya mhusika. Hudodosa fikra, hisia, mawazo, imani, hofu, mashaka, matumaini na matamanio ya mhusika binafsi. Vilevile, hudadisi athari za mambo hayo kwa mhusika na labda jamii yake. Hueleza mikinzano ya ndani ya mhusika kinafsi, kiakili na kijinsia. Baadhi ya riwaya za aina hii ni: *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971), *Kiu* (Mohamed, 1972), *Ukiwa* (Mkangi, 1973), *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974), *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990), na *Mhanga Nafsi Yangu* (Mohamed, 2012).

### (c) Riwaya za sira

Hizi ni riwaya ambazo husimulia habari za maisha ya mtu. Riwaya za aina hii zimegawanyika katika makundi mawili: riwaya za kitawasifu na za kiwasifu.

### (d) Riwaya za kitawasifu

Riwaya za kitawasifu ni zile zinazotumia nafsi ya kwanza, yaani mwandishi anaelezea mwenyewe kuhusu maisha yake tangu kuzaliwa kwake hadi muda wa kuandika riwaya husika; au hueleza kipande cha maisha yake ambacho sio lazima kiwe hadi anapoandika. Mwandishi hueleza matukio ambayo huona yanasisimua na huenda hayatokei kwa wengine. Kwa kuyaeleza, anadhani yanaweza kuwasaidia wasomaji. Riwaya ya aina hii huweka kumbukumbu au historia ya maisha ya mtu binafsi. Mifano ya riwaya za aina hizi ni *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (Robert, 1949 na 2003), *Mbali na Nyumbani* (Shafi, 2013) na *Nasikia Sauti ya Mama* (Walibora, 2015).

### (e) Riwaya za kiwasifu

Riwaya za kiwasifu ni zile zinazotumia nafsi ya tatu, yaani mwandishi husimulia maisha ya mtu mwingine. Mfano wa riwaya za wasifu ni *Wasifu wa Siti Binti Saad* (Robert, 1967).

FOR ONLINE READING ONLY

**(f) Riwaya za istiara**

Hizi ni riwaya za mafumbo ambazo umbo lake la nje ni ishara au kiwakilishi tu cha jambo jingine. Mifano mizuri ni riwaya za *Kusadikika* (Robert, 1991) na *Kufikirika* (Robert, 1968) ambazo huenda ni istiara kuhusu utawala wa mabavu wa kikoloni.

**(g) Riwaya za kingano**

Hizi ni riwaya zenye umbo na mtindo wa ngano. Mathalani, huweza kuwa na wahusika wanyama, visa vya ajabuajabu, mandhari ya kubuni na visa vyenye kutendeka nje ya wakati wa kihistoria. Mfano wa riwaya za kingano ni *Adili na Nduguze* (Robert, 1952) na *Lila na Fila* (Kiimbila, 1966).

**(h) Riwaya teti**

Hizi ni riwaya zinazosimulia vituko na masaibu ya maayari (watu wapuuzi, laghai, wajanja, na kadhalika) kwa njia inayosisimua na kuchekesha. Aghalabu maayari hao huwa watu wanaovutia (si wahusika wawi/waovu), wanatokea tabaka la chini, na bapa. Matukio ya riwaya hii hayana msuko ulioshikamana vizuri.

**(i) Riwaya barua**

Hizi ni riwaya ambazo sehemu yake kubwa husimuliwa kwa njia ya barua wanazoandikiana baadhi ya wahusika. Mfano ni riwaya ya *Barua Ndefu kama Hii* (Mariama Bâ, 2009).

**(j) Riwaya za kihistoria**

Riwaya hizi huchanganya historia halisi na ubunifu ili kutoa maudhui fulani. Mara nyingi, riwaya hizi zinajikita kwenye matukio makuu ya kihistoria yaliyoathiri mwenendo na mwelekeo wa jamii au taifa linalohusika. Riwaya ya kihistoria huchanganya wahusika wa historia na wa kubuni, matukio ya kweli na ya kubuni. Hata hivyo, riwaya hizo huzingatia zaidi namna matukio makuu ya kihistoria yalivyomwathiri mtu binafsi aliyeyashiriki. Riwaya ya kihistoria ina dhamira zinazogusa watu wengi, ni muhimu kwa sababu masimulizi yake yanahusu mambo yaliyotokea, na inawezekana yaliwahi kuwapata hata wasomaji. Ni kumbukumbu nzuri ya kipindi kilichopita. Baadhi ya riwaya mashuhuri za kihistoria ni *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1934), *Kuli* (Shafi, 1979), *Zawadi ya Ushindi* (Mtobwa, 1987), *Kwa Heri Iselamagazi* (Mapalala, 1992) na *Pambazuko Gizani* (Mboneko, 2004). Pia, kuna riwaya za Mulokozi za *Ngome ya Mianzi* (1990), *Ngoma ya Mianzi* (1991) na *Moto wa Mianzi* (1996). Nyingine ni *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1992) na *Wachamungu wa Bibi Kilihona* (Ruhumbika, 2014).

FOR ONLINE READING ONLY

**(k) Riwaya za kimaadili**

Hizi ni riwaya zenye nia ya kufundisha maadili fulani yahusuyo mwenendo mwema katika maisha. Ni riwaya zinazowapa watu maadili, na mara nyingi, maadili hayo huwa ya kidini. Wahusika wakuu huwa na sifa na tabia nzuri bila udhaifu. Sifa hizo ni za kudumu; kama ni mwenendo mwema huwa mwema tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mabadiliko yakitokea, huwa ya kimaadili na hutokea ghafla. Mifano ya riwaya za aina hii ni *Adili na Nduguze* (Robert, 1952) *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili* (Mnyampala, 1961) na *Mtu ni Utu* (Mhina, 1971).

**(l) Riwaya za kimapinduzi**

Hizi ni riwaya zinazojadili matatizo yanayosababisha migogoro fulani katika jamii kwa lengo la kuleta mabadiliko. Mabadiliko hayo huweza kuwa ya kisiasa, kiutamaduni au kiuchumi. Aghalabu, lengo la riwaya hizi ni kuuwezesha umma kushika hatamu kwa njia ya mapambano. Mifano ya aina hii ya riwaya ni *Ubeberu Utashindwa* (Kiimbila, 1971), *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (Shafi, 1974), *Kabwela* (Saffari, 1976), *Dunia Mti Mkavu* (Mohamed, 1979) na *Kuli* (Shafi, 1979).

**(m) Riwaya za kifalsafa**

Riwaya za kifalsafa ni zile zinazojadili masuala anuai kuhusu maisha. Aghalabu, masuala hayo ni yale yanayohitaji tafakuri ya kina. Hii inamaanisha kuwa riwaya hizi zinajadili kwa kina na kwa kufanya tafakuri makini kuhusu mambo ambayo hayaonekani kwa urahisi. Muundo wa riwaya hizi ni changamani. Riwaya hizi hujadili maswali kuhusu maana ya ukweli, maisha au kifo kama vile ukweli ni nini? Maisha ni nini? Kifo ni nini? Kuwapo na kutokuwapo ni nini? Mifano ya riwaya za kifalsafa ni *Mzingile*, *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (Kezilahabi, 1978), *Mafuta* (Mkangi, 1984), *Kiza katika Nuru* (Mohamed, 1988), *Nagona* (Kezilahabi, 1989), *Ziraili na Zirani* (Mkufya, 1999), na *Babu Alipofufuka* (Mohammed, 2001).

**(n) Riwaya za vitisho**

Hii ni riwaya yenye visa vya kutisha na kusisimua. Mara nyingi, visa hivyo huambatana na mambo ya ajabu au miujiza. Mambo hayo ni kama vile mauaji ya kishirikina, uchawi, uganga na vita. Mifano ya riwaya hii ni *Mbojo Simba Mtu* (Kuboja, 1971), *Mirathi ya Hatari* (Mung'ong'o, 1977) na *Janga Sugu la Wazawa* (Ruhumbika, 2002). Kwa mfano riwaya ya *Mirathi ya Hatari*, imeeleza visa na mikasa ya kisihiri katika jamii za Njombe. Msanii amemtumia Gusto ambaye anarithishwa mirathi ya hatari (uchawi) kutoka kwa baba yake, Kazembe. Mirathi hiyo inasababisha vifo visivyokuwa vya kawaida. Miongoni

FOR ONLINE READING ONLY

mwa vifo hivyo ni kile cha mama yake Gusto, dada yake (Nandi) na mjomba wake Gusto (Kapedzile). Kuwapo kwa matukio mengi ya kichawi kunaleta hofu kwa wasomaji wa riwaya hii. Zaidi, matendo yanayotendeka wakati Gusto akila kiapo cha uchawi yanatisha mno.

**(o) Riwaya za watoto na vijalunga**

Riwaya za watoto na vijalunga hutofautiana na riwaya za watu wazima kwa sifa kadhaa, zikiwamo za aina za wahusika, muundo, msuko, uchache wa visa, michoro na picha, matumizi ya fantasia na fonti zinazotumika. Vilevile, riwaya za watoto huepuka kusawiri matukio hasi kama vile ya mauaji, masuala ya ngono, na mahusiano ya jinsia moja. Mifano ya riwaya hizo ni *Safari ya Prospa* (Lema, 1995), *Kimbia Helena Kimbia* (Mnyaka, 1995), *Moto wa Mianzi* (Mulokozi, 1996) na *Marimba ya Majaliwa* (Semzaba, 2008).

## 2. Riwaya pendwa

Riwaya pendwa ni zile ambazo hutumia fani inayojichomoza na kusisimua zaidi kiasi cha kuweza kufunika maudhui. Hali hii huifanya riwaya hizi zionekane kuwa na lengo la kustarehesha au kuburudisha wasomaji tu. Mambo yanayosawiriwa sana na waandishi wa riwaya za kundi hili ni mapenzi, upelelezi, ujasusi, ugaidi, ujambazi na mauaji. Waandishi wa riwaya pendwa huyasawiri mambo hayo kwa ufundi mkubwa; na hupangilia visa na vituko kwa namna inayosisimua. Nchini Tanzania, aina hii ya riwaya iliandikwa kwa mara ya kwanza na Muhamed Said Abdulla (MSA) alipoandika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957). Mifano mingine ya riwaya hizi ni *Simu ya Kifo* (Katalambula, 1965), *Kisima cha Giningi* (Abdulla, 1968) na *Njama* (Musiba, 1981). Uandishi wa riwaya za aina hii uliongezeka maradufu katika miaka ya 1980, kutokana na matatizo ya kiuchumi.

**Sifa za riwaya pendwa**

Riwaya pendwa zina sifa zifuatazo:

**(i) Hutumia taharuki kwa kiasi kikubwa**

Taharuki ni hamu kubwa anayokuwa nayo msomaji kutaka kujua mambo yatakayotokea na yatakavyotokea katika hadithi. Taharuki hutumiwa kwa kiasi kikubwa katika riwaya pendwa kupitia matukio ya kusisimua yanayojibainisha kupitia migogoro iliyosukwa kwa ufundi. Taharuki inafikia kilele wakati fumbo linapofumbuliwa kwa kujibiwa maswali kadhaa yaliyojitokeza akilini mwa msomaji. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (Abdulla, 1957) swali linalojitokeza ni: nani amemuua Bwana Ali Bomani? Mbinu za awali za

FOR ONLINE READING ONLY

msanii za kumfanya msomaji awatuhumu watu wasiohusika ndizo zinazojenga maswali akilini mwa msomaji.

**(ii) Hutumia wahusika wa kimwendelezo**

Riwaya pendwa zina sifa ya kutumia wahusika walewale; hivyo, huwa na uwezo wa kujiendeleza katika vitabu kadhaa. Karibu kila mwandishi maarufu wa riwaya pendwa ameandika vitabu zaidi ya kimoja. Sifa hiyo ya kuwatumia wahusika walewale hufanya kitabu kimoja katika mfuatano wa vitabu kadhaa vya mwandishi mmoja kionekane kama tukio linalojitegemea katika mfululizo wa matukio mengi. Mifano ya watunzi waliowatumia wahusika wa jinsi hii ni Aristablus Elvis Musiba. Huyu amemtumia mhusika Willy Gamba katika riwaya zake. Pia, Muhammed Said Abdulla amemtumia mhusika Bwana Msa katika riwaya zake takribani zote. Mwandishi mwingine ni Ben Mtobwa ambaye amemtumia mhusika *Joram Kiango* katika baadhi ya riwaya zake.

**(iii) Huwa na mhusika mkuu mkwezwa**

Mhusika wa riwaya pendwa mara nyingi hupewa sifa zisizo za kawaida kitabia na kiutendaji. Mhusika mkuu wa riwaya pendwa hukwezwa juu ya wahusika wengine; hivyo, anatawala na ana sifa ya ubabe. Wahusika hawa huwa na sifa ya kuwa kielelezo chenye ukamilifu, yaani kutokuwa na dosari. Mifano mizuri ya wahusika wa namna hii ni Bwana Msa, Willy Gamba na Joram Kiango. Mara kwa mara, mhusika mkuu ndiye mshindi hata akipitia katika taabu na mashaka ya aina gani, tunajua, hatimaye ataibuka kuwa mshindi katika mapambano yake. Wahusika hawa wakuu hutenda na kuendesha mambo yao kama miungu wadogo pasi na kukosea. Huwa hodari sana katika kutenda mambo yao. Mambo hayo ni kama vile kuchunguza, kufanya mapenzi, kuwindana, kupigana kwa silaha na kwa mikono mitupu. Kwa hiyo, ufundi wa utendaji unaojitokeza humo huwa unaziteka nafsi za wasomaji na, wakati mwingine, kuwasahaulisha hata maudhui. Mfano mzuri ni mhusika mkuu wa riwaya ya *Njama* (Musiba, 1981). Msomaji anapoendelea kuisoma riwaya hii, anajikuta anamezwa na ufundi wa kupeleleza na kupambana unaooneshwa na Willy na wenzake kiasi cha kupoteza kiini cha simulizi yenyewe, ambacho kinahusu ukombozi wa nchi za Afrika. Hali hii inasababishwa na hali ya kukwezwa kwa wahusika wa riwaya, hususani Willy Gamba, katika tabia na matendo yao.

**(iv) Hupendwa na watu wengi**

Riwaya hizi zina wasomaji na wapenzi wengi, hasa vijana. Hii ni kwa sababu wasanii wake wameupatia vizuri utunzi wa kisasa ambao umeletwa na utamaduni

FOR ONLINE READING ONLY

wa kigeni unaofuatwa kwa makini na vijana na baadhi ya watu wazima. Kwa hiyo, watu wanaposoma riwaya hizi, wanasisimka na kuburudika.

### (v) Hutumia mandhari ya mijini

Wasanii wa riwaya pendwa hutumia mandhari halisi au ya kubuni, hususan katika miji au majiji. Hali hii ndiyo inayoonesha upekee wa mandhari ya riwaya pendwa. Wasanii hutumia mandhari ya namna hii ili kukidhi malengo ya usukaji wa visa na maisha ya wahusika. Mandhari ya namna hii hubeba matukio kama vile ufujaji mkubwa wa fedha kwenye sehemu za starehe, kama vile baa, hoteli kubwa na fukwe za bahari. Kwa mfano, kwenye riwaya ya *Salamu Toka Kuzimu* (Mtobwa, 1987), kuna ufujaji mkubwa wa fedha unaofanywa na mhusika Joram na mpenzi wake. Vilevile, mandhari ya mjini yanaoneshwa kupitia tukio kama la uchezaji wa kamari linalojitokeza kwenye riwaya ya *Simu ya Kifo* (Katalambula, 1965). Aidha, mandhari ya mjini au jijini yanathibitishwa na kuwapo kwa kampuni na mashirika makubwa. Kampuni hizi huajiri watu. Waandishi huumba wahusika wenye vyeo kwa kuhusianisha na kampuni na mashirika hayo. Mfano mzuri ni mhusika *Kalulu* katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* (Mtobwa 1984). Huyu ni kiongozi katika kampuni mojawapo ya kusambaza dawa za Oxton. Mzee Jacobo kwenye *Simu ya Kifo* (Katalambula, 1965) ni mfanyakazi katika shirika la reli.

Mandhari ya mijini pia hudhihirika kupitia matumizi ya vyombo vya mawasiliano kufanikisha matukio ya ujambazi, ujasusi, uporaji na uhusiano wa kimapenzi. Mathalani, katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* (Mtobwa, 1985), mhusika Kwame anatega chombo cha kunasa mawasiliano ofisini kwa Kombora. Chombo hiki kinamsaidia kunasa maongezi yote ya mipango ya kuwasaka wahalifu (Kwame na kundi lake). Kwa njia hii, Kwame na kundi lake wanang'amua mikakati ya kukamatwa, hivyo, wanafanikiwa kuwakimbia askari.

### (vi) Matumizi ya wanawake kama nyenzo ya mafanikio

Kwa ujumla, wahusika wakuu wa kiume wa riwaya pendwa husawiriwa wakifanikiwa katika mambo yao kupitia mbinu ya kuwatumia wanawake warembo. Warembo hao hutumiwa kwa njia za mapenzi, kuwa chambo cha kufanyia uhalifu, au chambo cha kumnasia adui. Mapenzi, kwa upande wake, huonekana kuwa jambo muhimu sana katika riwaya pendwa. Huonekana kwamba, upelelezi au shughuli yoyote inayofanyika haiwezi kusisimua wala kufanikiwa bila mapenzi. Katika riwaya za Musiba, kwa mfano, mhusika Willy Gamba huwa na wasichana warembo ambao ndio wapenzi wake wanaomsaidia kufumbua mafumbo mazito na mitego mikubwa. Baadhi yao ni Zabibu kwenye

FOR ONLINE READING ONLY

riwaya ya *Njama*, (Musiba 1986), Tete na Mwadi kwenye riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*, (Musiba 2018), pamoja na Nyaso kwenye riwaya ya *Hofu* (Musiba 2018).

**(vii) Huiga mawazo na matendo ya filamu za kigeni**

Riwaya pendwa nyingi za Kiswahili, hasa za miaka ya 1980, ni mwigo wa maandishi ya Kimagharibi pamoja na filamu za Kizungu na Kiasia zinazohusu upelelezi, ujasusi, uhalifu na mapenzi. Wasomaji wengi wameifanya riwaya pendwa kama kibadala au kijalizo cha filamu. Kwa mfano, Musiba kwenye riwaya zake amemchora mhusika mkuu, Willy Gamba, kwa kumpa ujuzi wa kupigana kininja katika mapambano dhidi ya majasusi. Kupigana kwa kufuata sheria za kininja, mara nyingi, ni mbinu zinazotumiwa na filamu za Kimagharibi na Kimashariki.

**Shughuli 2.15**

Soma riwaya na hadithi fupi teule, kisha eleza tofauti ya tanzu hizo.

**Zoezi la 2.3**

1. Kwa kutumia mifano, tofautisha dhana zifuatazo:
   (a) melodrama na ramsa
   (b) utao na ukwapi
   (c) riwaya za kihistoria na za sira
   (d) mashairi na tenzi
   (e) riwaya za kifalsafa na za kisaikolojia
2. "Riwaya ni zao la fasihi simulizi." Jadili
3. "Tamthiliya za Kitanzania za sasa ni zao la tamthiliya za Kimagharibi." Jadili.
4. Eleza kwa ufupi namna dhana ya utendaji inavyojitokeza katika tamthiliya.
5. Kwa kutumia mifano, eleza aina za tamthiliya na namna zinavyotofautiana.
6. Kwa kutumia mifano, jadili mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili katika vipindi mbalimbali.

FOR ONLINE READING ONLY

7. "Hadithi fupi ni utanzu usioeleweka" Jadili kauli hii kwa mifano.
8. Jadili maendeleo ya riwaya ya Kiswahili baada ya Uhuru.
9. Eleza mchango wa mapinduzi ya viwanda katika kuzuka na kukua kwa riwaya.
10. Kwa kutumia mifano thabiti, jadili kauli kuwa fasihi simulizi ni malighafi ya fasihi andishi.

## Uhusiano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi

Licha ya kutofautiana, aina za fasihi zina uhusiano wa mwingiliano. Kwa mfano, kazi za fasihi andishi zina vipengele vya kifasihi simulizi kama vile semi, nyimbo na mazungumzo au dayolojia, wahusika wasio wanadamu (kwa mfano wanyama, mazimwi, wadudu na vinginevyo) na mbinu za uwasilishaji (mianzo na miisho ya hadithi, mianzo na miisho ya tenzi na nyinginezo). Mbali na mwingiliano, aina hizi za fasihi hutofautiana, kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi**

| Na. | Kigezo | Fasihi simulizi | Fasihi andishi |
|---|---|---|---|
| 1. | Utunzi | Huweza kutungwa mapema na kukaririwa kabla ya uwasilishaji. Huweza pia kutungwa papo hapo wakati wa utendaji. | Hutungwa kwa kipindi kirefu kabla ya kuwasilishwa kwa hadhira. |
| 2. | Uwasilishaji | Huwasilishwa kwa njia ya mdomo, ishara na vitendo. Uwasilishaji huo hutumia viambato kama vile maleba, miondoko na sauti. | Huwasilishwa kwa njia ya maandishi. |
| 3. | Umri | Ni kongwe kwa sababu ilianza kabla ya ugunduzi wa maandishi. | Ilianza baada ya mwanadamu kugundua maandishi. |
| 4. | Umiliki | Tanzu nyingi za fasihi simulizi ni mali ya jamii nzima. | Ni mali ya mtunzi na mdhamini wake. |

FOR ONLINE READING ONLY

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Uhifadhi | Huhifadhiwa kichwani na kuendelezwa kwa njia ya kupokezana, ijapokuwa kutokana na maendeleo ya teknolojia, huweza kuhifadhiwa katika vinasa sauti, kompyuta na hata maandishi. | Huhifadhiwa katika nyaraka au kwa njia za kidijiti. |
| 6. | Tanzu na vipera | Idadi ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi ni kubwa kuliko ilivyo katika fasihi andishi. Aidha, huwa na mwingiliano mkubwa wa vipera. | Idadi ya tanzu na vipera vya fasihi andishi ni ndogo. Aidha, vipera vyake havina mwingiliano mkubwa. |
| 7. | Mabadiliko | Hubadilika kwa haraka kutegemeana na mahitaji ya hadhira, tukio la kijamii na wakati. | Haibadiliki kwa haraka kwa sababu ipo katika hali ya kudumu. |
| 8. | Hadhira | Hadhira yake ni hai ambayo hushiriki katika utendaji kama kuitikia, kupiga vigelegele na makofi. | Ni wasomaji; hivyo hawashiriki katika utendaji, isipokuwa katika tanzu chache zinazowasilishwa kiutendaji kama vile mashairi na tamthiliya. |
| 9. | Wahusika | Hutumia wahusika mchanganyiko (kwa mfano binadamu, wanyama, mimea na vitu visivyo na uhai). | Hutumia zaidi wahusika binadamu. Wahusika wasio binadamu hutumika mara chache. |
| 10. | Muundo | Huwa na muundo wa moja kwa moja, aghalabu bila utata. | Huweza kuwa na muundo wa moja kwa moja au changamani kutegemeana na utanzu. |

**Shughuli ya 2.16**

Kwa kutumia vyanzo vya maktabani na mtandaoni, eleza namna fasihi simulizi ilivyochangia kupatikana kwa fasihi andishi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Mchango wa fasihi simulizi katika maendeleo ya fasihi andishi

Maendeleo ya fasihi andishi kabla ya uhuru yana uhusiano mkubwa na wamisionari na watawala wa kigeni. Wageni hawa walipofika pwani ya Afrika Mashariki, waliwakuta wenyeji wakiwa na fasihi yao. Kwa mfano, baadhi ya tenzi za zamani kama vile *Fumo Liyongo* zilikuwa zikisimuliwa kabla ya maandishi na ziliwekwa katika maandishi baadaye. Pia, tenzi hizi zilitokana na nyimbo ambazo ndizo fasihi ya awali.

Halikadhalika, kuna athari za mashairi na fani nyinginezo kama tarihi, masimulizi ya wasafiri, ngano na hekaya mbalimbali. Ngano na hekaya hizi ndizo zilitafsiriwa na kuwa msingi wa hadithi za awali za Kiswahili. Miongoni mwa hadithi hizo ni *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870) zilizotafsiriwa na Edward Steere. Ngano nyingine zimechapishwa katika Kitabu cha *Prosa und Poesie der Suaheli* (1907) kilichohaririwa na Carl Velten, *Mazungumzo ya Alfu Lela Ulela* Juzuu (1-4) (1928) kilichotafsiriwa na Edwin Brenn na kuhaririwa na Frederick Johnson na *Hekaya za Abunuwasi* (Chiponde, 1928). *Kisiwa chenye Hazina* (Johnson, 1929), *Safari za Gulliver* (Swift, 1932), *Mashimo ya Mfalme Suleimani* (Haggard, 1937) na *Safari ya Msafiri* (Bunyan, 1925).

Kama ulivyojifunza kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi, fasihi hii inajumuisha hadithi, semi, ushairi na sanaa za maonesho na vipera vyake. Baadhi ya tanzu hizi hujitokeza katika fasihi andishi kwani vipengele mbalimbali vya tanzu hizo huweza kutumika kama mbinu za kisanaa katika kazi za fasihi andishi. Mfano wa vipengele hivyo ni wahusika wasio binadamu kama vile wanyama, mashetani na mazimwi, kama wanavyojitokeza katika riwaya za vitisho na za kingano. (Senkoro, 2011).

Kuanzia miaka ya 1940 hadi 1960, riwaya nyingi za Kiswahili zilifuata mkondo wa hekaya na ngano. Kimaudhui, riwaya hizo zilielezea mambo ya mila na desturi kama njia ya kutunza maadili. Mifano ya riwaya hizo ni *Adili na Nduguze* (Robert, 1952), *Kusadikika* (Robert, 1991) na *Kufikirika* (Robert, 1968).

Kimsingi, fasihi simulizi imekuwa nguzo ya fasihi andishi katika kueneza tamaduni mbalimbali za kijamii. Waandishi mbalimbali wamechota fikra kutoka katika kazi mbalimbali za kifasihi simulizi na kuzitumia katika tungo za fasihi andishi.

**Shughuli ya 2.17**

Chunguza vipindi vya fasihi simulizi vinavyorushwa na vituo vya runinga au sikiliza vipindi kutoka katika vituo viwili vya redio, kisha eleza athari zinazotokana na vipindi hivyo kurushwa kwa njia hizo.

FOR ONLINE READING ONLY

## Athari za sayansi na teknolojia katika maendeleo ya fasihi simulizi na fasihi andishi

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesaidia sana katika uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi. Maendeleo haya yamewezesha kuwapo kwa vyombo mbalimbali vya uwasilishaji kama redio, runinga na simu. Redio na runinga zimekuwa na mchango mkubwa katika uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi. Kwa mfano, *Redio Tanzania* (kwa sasa TBC Taifa) imekuwa na vipindi ambavyo vimesaidia sana fasihi simulizi kuwafikia watu wengi. Kipindi kama vile *Mama na Mwana* kilipendwa na watu wengi, hasa watoto, kwa sababu ya masimulizi ya hadithi mbalimbali. Kipindi kingine ni *Cheichei Shangazi* ambacho kimekuwa na masimulizi ya hadithi, vitendawili na nyimbo. Baadaye, vilianzishwa vituo vingine vya redio na kuongeza mawanda ya uwasilishaji na uenezaji wa kazi za fasihi simulizi. Kwa mfano, *Redio One Stereo* hurusha kipindi cha *Watoto Wetu* ambacho hupambwa na wimbo maarufu wa "Watoto Wasafi Moyoni". Kipindi hiki hurushwa kila Jumamosi, ambapo watoto walioko studio na nyumbani huweza kushiriki katika uwasilishaji wa hadithi, methali, vitendawili, mafumbo na nyimbo.

Pamoja na watoto kutoonana ana kwa ana, wanaweza kushiriki kwa njia ya kusikiliza. Hivyo, hadithi ambazo awali zilisimuliwa kwa watu wachache, zinaweza kujulikana kwa wote wanaosikiliza. Mbali na vipindi vya watoto, redio zimekuwa zikirusha vipindi vingine vya fasihi simulizi. Baadhi ya vipindi hivyo ni *Mkoa kwa Mkoa*, *Malenga Wetu*, *Ngoma Zetu*, *Zilipendwa*, (*TBC Taifa*), *Hizi Nazo* (*Redio One Stereo*), *Kwa Raha Zetu* (*Redio Clouds FM*) na *Mitikisiko ya Pwani* (*Times FM*).

Kwa upande wa runinga, uwasilishaji umekuwa tofauti kidogo. Katika runinga washiriki wana fursa ya kuona matendo yanayotendwa. Kuna vipindi vya watoto ambavyo huwasilisha kazi za fasihi simulizi. Mfano wa vipindi hivyo ni kipindi cha *Watoto kilichoandaliwa na TET* ambacho hurushwa na *TBC1* na *TBC2*. Kipindi hiki kinachorushwa siku za Jumamosi na Jumapili, husimulia hadithi na michezo ya watoto. Pia, kuna kipindi cha *Ubongo Kids* (*TBC1*) ambacho kinahusu somo la hisabati na kusoma. Kipindi hiki huwa na matumizi ya nyimbo, usimulizi wa hadithi, na maigizo mbalimbali. Aidha, kituo cha *ITV* hurusha kipindi cha *Watoto Show* ambacho hujumuisha nyimbo, ngoma, methali, vitendawili na hadithi. Halikadhalika, runinga zimekuwa zikirusha vipindi kama vile, *Mizengwe*, *Sanaa na Msanii*, *Mashamushamu ya Pwani* na *Hawavumi lakini Wamo* (*ITV*). Vipindi vingine ni *Futuhi*, *Bongo Beats* na *Msanii Wetu* (*Star TV*). Aidha, kuna *Fataki*, *Ngoma Zetu*, *Mchikicho wa Pwani Club Raha Leo Show* (*TBC1*), na *Mirindimo ya Pwani* (*Channel Ten*). Vipindi vyote hivyo vimekuwa vikisaidia uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi.

FOR ONLINE READING ONLY

Matumizi ya simu nayo yana mchango mkubwa katika jamii. Watu wengi hutumia simu kwa mawasiliano ya mazungumzo. Kuwapo kwa mawasiliano ya mitandao ya kijamii kwa kutumia simu kumewezesha uwasilishaji na uenezaji wa fasihi simulizi. Baadhi ya simu zina uwezo wa kurekodi na kutuma nyimbo, masimulizi na picha. Pia, zina uwezo wa kunasa vituo mbalimbali vya redio na runinga na, hivyo, kuwawezesha watumiaji wake kusikiliza kazi za kifasihi. Vilevile, vifaa kama vile vishikwambi, na kompyuta vimerahisisha uhifadhi, ubebaji, na usomaji wa kazi za fasihi andishi. Zaidi, teknolojia imesaidia kupatikana kwa majukwaa ya kidijiti kama vile mitandao ya kijamii ambayo watunzi wa kazi za fasihi simulizi na andishi huitumia kuwasilishia au kuuzia kazi zao.

Kadhalika, kutokana na maendeleo ya kiteknolojia, fasihi simulizi pia imekuwa ikiwasilishwa kwa njia ya maandishi. Hii inatokana na kuongezeka kwa viwanda vya uchapaji ambavyo vimerahisisha mchakato wa uzalishaji wa machapisho ya kazi mbalimbali za fasihi, zikiwamo zinazotokana na fasihi simulizi.

**Shughuli ya 2.18**

(a) Kusanya semi kumi (10) za Kiswahili kulingana na makundi yafuatayo:

(i) Methali tano (5) zinazoonya kuhusu utovu wa nidhamu.

(ii) Misemo mitano (5) inayohamasisha umoja na ushirikiano katika jamii.

(b) Jadili mchango wa semi ulizozikusanya na umuhimu wake kwa maendeleo ya jamii.

## Mchango wa fasihi simulizi na fasihi andishi katika maendeleo ya jamii

Fasihi simulizi na andishi zimekuwa na mchango mkubwa kwa jamii ambao umesaidia katika kuigeuza na kuibadilisha jamii. Mchango huo umeweza kujidhihirisha kama ifuatavyo:

### (a) Kuelimisha jamii

Mchango mkubwa wa fasihi simulizi na andishi ni kuelimisha jamii. Fasihi huufumbua macho umma na kupiga vita matatizo ya njaa, maradhi, umaskini na mengineyo. Aidha, fasihi huipa jamii maarifa na stadi za kukabiliana na mazingira ambamo jamii inaishi. Kwa mfano, kuna nyimbo mbalimbali zinazotoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira. Kutokana na nyimbo hizo jamii imeweza kuelimika na kupata maarifa ya namna ya kutunza mazingira pamoja na kuendeleza shughuli za maendeleo binafsi na ya kitaifa. Jamii inasisitiza kuwa mazingira yasipotunzwa husababisha mabadiliko hasi ya tabia nchi.

FOR ONLINE READING ONLY

### (b) Kuburudisha jamii

Mchango mwingine wa fasihi simulizi na andishi ni kuburudisha jamii. Katika kutimiza jukumu hili, fasihi hustarehesha, huliwaza na kutuliza mwili na akili ya hadhira. Kwa mfano, watu wanapotazama vichekesho na maigizo ya "Mizengwe" (katika ITV Tanzania) hufurahia vituko, kejeli na mizaha inayoigizwa.

### (c) Kuutambulisha na kuendeleza utamaduni

Fasihi simulizi na andishi husaidia kuutambulisha, kuutangaza na kuuendeleza utamaduni. Kwa mfano, kazi mbalimbali za fasihi simulizi na fasihi andishi ya Kiswahili huakisi vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Mswahili. Mifano ya vipengele hivyo ni desturi, dini, mavazi, mila, vyakula, na namna ya kuhusiana. Vilevile, mchango mwingine ni kuchangia katika kutunza amali na kumbukumbu nyingine za jamii. Mifano ya amali hizo za kijamii ni mila, desturi, historia na sanaa. Tamthiliya za Kiswahili kama vile *Kinjekitile* (Hussein, 1969) na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Mbogo, 1988) zimebeba vyema jukumu hili la kuhifadhi na kurithisha amali za jamii. Pia, zinafafanua masuala ya kijadi kama vile imani na uganga.

### (d) Kuadibu na kunasihi jamii

Mara nyingi, fasihi hutumika kama nyenzo ya kuasa na kuadibu kuhusu mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Kwa mfano, tamthiliya ya *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* (Semzaba, 1988) inawaadibu na kuwaasa watu kufanya kazi kwa nidhamu. Kwa ufupi, tamthiliya hiyo inatoa funzo kwamba mtaka yote kwa pupa, hukosa yote. Katika fasihi simulizi, nyimbo hutumika kukamilisha jukumu hili. Kwa mfano, baadhi ya nyimbo za bongo fleva zina wasihi watu kupambana na harakati za maisha kwa kutafuta fursa za kiuchumi, bila kujali umbali unaoweza kusababisha utengano wa kifamilia.

### (e) Kukuza na kuhifadhi lugha

Fasihi simulizi na andishi ina mchango mkubwa katika kuikuza lugha. Lugha haiwezi kudumaa kwa sababu inakuwa kwenye matumizi. Mwanafasihi hutumia maneno kuibua na kueleza dhana mbalimbali katika utunzi wa kazi zake. Uandishi na usimulizi wa kazi za fasihi huibua misemo mipya mara kwa mara; kwa njia hii lugha huweza kukua. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika* (Robert, 1991) kuna uibuaji wa msamiati kama vile 'ali ali' (tukufu) 'azali' (asili au kiini) 'kitali' (mapigano) na 'mlizamu' (chemchem).

### (f) Kutia hamasa jamii

Fasihi hutia hamasa kuhusiana na mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii. Mathalani, riwaya ya *Pepo ya Mabwege* (Mwakyembe, 1980) inatia hamasa

FOR ONLINE READING ONLY

kwa vijana kusimamia kile wanachokiamini. Mhusika Kalenga alisimama kidete kufichua uozo uliomo kwenye jamii, na hatimaye alipandishwa cheo kutokana na kazi nzuri aliyoifanya. Vilevile, kazi nyingine za fasihi kama nyimbo zimekuwa zikitumika kutia hamasa ya wanawake kufanya kazi ili kujiletea maendeleo bila kuwa wategemezi katika jamii.

### (g) Kukosoa jamii

Fasihi ina mchango katika kukosoa jamii kuhusiana na mambo mbalimbali ya maisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufikirika* (Robert, 1968), mwandishi anakosoa tabaka tawala linalotumia rasilimali nyingi kwa manufaa ya watu wachache ilihali wanajamii wengine wanateseka. Halikadhalika, methali katika fasihi hutumika kukosoa au kuonya jamii. Methali kama vile "Mkataa pema, pabaya panamwita" inakosoa mtu anayekataa wosia mzuri kwani kuna madhara yanaweza kumpata. Aidha, methali kama "Tamaa mbele, mauti nyuma" imekusudiwa kuwaonya wanajamii kuepuka tamaa kwani mtu mwenye tamaa anaweza kukabiliwa na madhara.

### (h) Kukomboa jamii

Fasihi simulizi na fasihi andishi imechangia sana kupiga vita masuala mbalimbali yanayokwamisha maendeleo ya jamii kama vile ujinga, maradhi na umaskini. Tamthiliya ya *Hawala ya Fedha* (Lihamba, 1985), kwa mfano, inaeleza mambo yanayosababisha umasikini ambayo ni ujinga na uvivu. Aidha, wakati wa harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika, baadhi ya bendi za muziki wa dansi zilipiga nyimbo za kuwaunganisha watu kwa ajili ya ukombozi. Mfano mzuri wa wimbo wa "Mwenyekiti Mwalimu Nyerere" ulioimbwa na bendi ya *Urafiki Jazz miaka ya 1970* wimbo huo ulikuwa ukimsihi mwenyekiti wa nchi tano zilizo mstari wa mbele kupigania ukombozi wa Kusini mwa Afrika azidishe mapambano kwani maadui wa Afrika walilisumbua sana Bara la Afrika.

**Shughuli ya 2.19**

(a) Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, jadili mchango wa fasihi andishi ya Kiswahili katika jamii.

(b) Jadili uhusiano uliopo baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

**Tamrini**

1. Kwa kutumia mifano, eleza namna sayansi na teknolojia zinavyochangia katika kukuza fasihi simulizi na andishi.
2. Fafanua tofauti kati ya maigizo na tamthiliya andishi ya Kiswahili.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Jadili jinsi utanzu wa semi unavyosaidia kuimarisha tanzu nyingine za fasihi simulizi.
4. Kwa kutumia mifano, eleza namna fasihi simulizi na fasihi andishi zinavyochangia kukuza maendeleo ya kijamii.
5. Eleza namna ushairi simulizi ulivyochangia katika kukua kwa ushairi andishi.
6. Kwa kutumia mifano, eleza namna sayansi na teknolojia inavyokuza fasihi simulizi na andishi.
7. Jadili maendeleo ya ushairi kwa kuzingatia vipindi mbalimbali.
8. "Bila fasihi simulizi hakuna fasihi andishi". Jadili kauli.
9. Katika orodha uliyopewa, chagua waandishi wawili wa tanzu tofauti kisha ueleze mchango wa kila mmoja wao katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.
   (a) Shaaban Robert
   (b) Euphrase Kezilahabi
   (c) Mugyabuso Mulokozi
   (d) Mohammed Said Abdulla
   (e) Eric Shigongo
   (f) Gabriel Ruhumbika
   (g) Zainabu Mwanga
   (h) Penina Muhando
   (i) Muhammed Seif Khatib
10. "Michezo ya watoto haina umuhimu wowote katika makuzi yao". Jadili kauli hii kwa kutumia mifano maridhawa.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tatu — Kutathmini kazi za fasihi

## Utangulizi

*Kutathmini kazi za fasihi ni muhimu kwa sababu kunajenga uwezo wa kiakili na kihisia, kukuza stadi za uchambuzi na uandishi, kuchochea mawazo na kuelewa muktadha wa kihistoria na kijamii. Katika sura hii utajifunza, mitazamo, uhusiano na dhima ya vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi. Pia, utajifunza nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi pamoja na kuzitumia katika kuchambua kazi mbalimbali za kifasihi. Umahiri utakaoujenga katika sura hii utakuwezesha kukuza stadi za uchambuzi na uandishi wa kazi za kifasihi.*

*Fani bila maudhui*

**Shughuli ya 3.1**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni au maktabani na vinginevyo, soma matini zinazohusu mitazamo mbalimbali ya dhana za fani na maudhui.

## Mitazamo kuhusu fani na maudhui

Kuna mitazamo miwili inayoeleza fani na maudhui nayo ni: mtazamo wa kidhanifu na wa kiyakinifu. Sehemu inayofuata inafafanua mitazamo hiyo.

### Mtazamo wa Kidhanifu

Mtazamo wa kidhanifu ni ule unaochukulia fani na maudhui kama vipengele ambavyo havina uhusiano, yaani kila kimoja kinajitegemea. Kwa mtazamo huu, katika kazi za fasihi, fani na maudhui huweza kutenganishwa na kila kimoja kikajitegemea. Hivyo, mtunzi anaweza kufikisha ujumbe wake kwa hadhira aliyokusudia bila kutilia maanani fani. Sengo na Kiango (1973) na Nkwera (1978) wametumia mtazamo wa kidhanifu katika kufasili dhana za fani na maudhui.

FOR ONLINE READING ONLY

Wataalamu hawa huitazama fani na maudhui kama chungwa na ganda lake au kikombe na chai.

Zifutazo ni hoja za mtazamo wa kidhanifu:

(a) **Fani na maudhui ni kama chungwa na ganda lake:** Mtazamo huu unayaona maudhui kama nyama ya ndani ya chungwa na fani ni ganda lake la nje ambalo huifunika nyama hiyo. Mtu anapotaka kula chungwa huliondoa ganda lake na kulitupa, kwani lengo huwa ni kuipata nyama ya ndani. Kwa mtazamo huu, fani na maudhui huweza kutenganishwa. Hivyo, mtunzi anapotunga kazi yake huwa hana haja na fani kwani kusudi lake ni maudhui ambayo hulengwa kwa hadhira husika. Maudhui lengwa huweza kuifikia jamii hata kama hayajafumbatwa na fani. Hadhira inaposoma kazi hiyo hutafuta maudhui na si fani iliyoifunika kazi hiyo.

(b) **Fani na maudhui kama kikombe na chai:** Mtazamo huu umejitokeza katika kazi za baadhi ya watalaamu wa fasihi. Miongoni mwao ni Nkwera (1978) ambaye anashadidia kuwa fani na maudhui vinaweza kutenganishwa na kwamba kila kimoja kinajitegemea kama ilivyo kikombe na chai. Kikombe hutumika kubeba chai ili mnywaji aweze kuinywa. Chai ikinyweka kikombe huwa hakina kazi tena. Hapa kikombe kinawakilisha fani na chai ni maudhui katika kazi za fasihi. Hii ina maana kuwa mtunzi wa kazi ya fasihi hulenga kufikisha maudhui kwa jamii na fani huwa ni kibebeo chake tu. Mtazamo huu unaona kuwa mtunzi anaweza kufikisha maudhui kwa hadhira yake bila kutumia fani.

**Mtazamo wa kiyakinifu**

Mtazamo wa kiyakinifu huitazama fani na maudhui kama vipengele vinavyotegemeana na ambavyo haviwezi kutenganishwa. Hii ni kwa sababu fani na maudhui hutegemeana, huathiriana na kujengana. Mtazamo huu hulinganisha fani na maudhui kama pande mbili za sarafu. Ifuatayo ni hoja kuu ya mtazamo wa kiyakinifu:

**Fani na maudhui kama pande mbili za sarafu moja**: Mtazamo huu unaungwa mkono na Senkoro (1982 na 2011) unafananisha fani na upande wa kwanza wa sarafu, ilhali maudhui ni upande wa pili. Hii ina maana kwamba pande mbili za sarafu ndizo huikamilisha sarafu hiyo; hivyo, haziwezi kutenganishwa.

FOR ONLINE READING ONLY

Fani hufumbata maudhui; na maudhui ndiyo huitengeneza au kuipa umbo fani. Inamaanisha kuwa ili kazi ya fasihi ikamilike na iwe bora, lazima iwe na vipengele vya fani na maudhui ambavyo huhitajiana, hushirikiana, hutegemeana, huwiana na hukamilishana. Uwiano na ushirikiano wa fani na maudhui ndio unaokamilisha kazi ya fasihi.

**Shughuli ya 3.2**

(a) Chambua vipengele vya fani na maudhui katika hadithi teule moja uliyosoma kisha jibu maswali yafuatayo.

  (i) Ni kwa namna gani wahusika wa hadithi hiyo wanahusiana na migogoro iliyojitokeza?

  (ii) Kwa nini mwandishi ametumia muundo alioutumia katika kufikisha ujumbe wake?

  (iii) Ni kwa namna gani lugha iliyotumika inachangia kuibua maudhui katika hadithi hiyo?

  (iv) Taswira alizozitumia mwandishi zina mchango gani katika kuelewa dhamira za hadithi hii?

  (v) Mtindo wa uandishi wa hadithi hiyo umechangiaje katika kuwasilisha maudhui?

(b) Chambua uhusiano wa fani na maudhui katika kazi yoyote ya fasihi ya Kiswahili.

## Uhusiano wa fani na maudhui katika kazi za fasihi

Mwandishi na mhakiki wa kazi za fasihi anapaswa/hupaswa kuzingatia uhusiano wa vipengele vya fani na maudhui katika kubuni na kuchambua kazi. Endapo mwandishi na mhakiki huyo hatazingatia na kuhusianisha ipasavyo vipengele hivyo, vya fasihi uhakiki wake utakuwa chapwa.

**Shughuli ya 3.3**

Kwa kutumia mifano, jadili umuhimu wa fani na maudhui katika kazi za fasihi.

## Dhima za vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi

Vipengele vya fani na maudhui vina dhima kubwa katika kazi ya fasihi. Dhima hizo muhimu zinaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

FOR ONLINE READING ONLY

**(a) Kuwavutia wasomaji**

Kazi iliyopambwa kwa sanaa huwavutia wasomaji kutamani kuisoma na kuielewa. Wasomaji hupenda kazi za fasihi ambazo huwafanya wasichoke kusoma na wauishi ulimwengu wa kazi hiyo. Kwa mfano, kutumia mbinu nzuri za kisanaa huwezesha kufikisha ujumbe husika, kuielewa na kuifurahia kazi ya fasihi.

**(b) Kuchochea mawazo na hisia kwa wasomaji**

Uandishi wenye mifano ya kina na uumbaji wa wahusika na mandhari kiubunifu huwafanya wasomaji kuhisi na kufikiri zaidi. Kazi za fasihi zinazochochea mawazo na kuibua hisia husaidia kuleta mabadiliko ya kifikra, kuongeza ubunifu na maarifa, na kuwapa wasomaji mtazamo tofauti kuhusu maisha na duniani wanamoishi.

**(c) Kuipa maana kazi ya fasihi**

Wasomaji wengi hupenda kufuatilia hadithi au tukio fulani na hutamani kulijua zaidi, yamkini kutokana na mafunzo ama ujumbe uliomo ndani yake. Maudhui yaliyomo ndani ya kazi ya fasihi huwafanya wasomaji kuutazama ulimwengu kwa jicho la tofauti na kuwafikirisha kuhusu masuala muhimu katika jamii. Hivyo, maudhui husaidia kubaini mafunzo yatokanayo na kazi za fasihi.

**(d) Kuongeza ubora na upekee wa kazi ya fasihi**

Mwandishi anayetumia ubunifu mkubwa uliojaa mbinu za kifasihi katika mtindo wake wa uandishi huongeza ubora wa kazi na kutofautisha kazi hiyo na nyingine. Matumizi ya tamathali za semi na taswira mbalimbali husaidia kuumba ulimwengu mbadala ambao unaakisi ukweli na uongo, hali ambayo huzidisha ubunifu wa kazi za fasihi.

**(e) Kukuza stadi za uandishi wa kazi za fasihi**

Ufahamu wa kina wa vipengele vya fani na maudhui huwasaidia waandishi kuandika kwa umahiri mkubwa.

**Zoezi la 3.1**

1. "Fani na maudhui havina umuhimu katika kazi za fasihi". Jadili hoja hii kwa mifano thabiti kutoka katika kazi teule za fasihi.
2. Fafanua kauli kwamba "uhusiano wa fani na maudhuii ni kama chai na kikombe".

FOR ONLINE READING ONLY

3. "Fani na maudhui ni kama pande mbili za sarafu." Jadili kauli hii.
4. Eleza ubora na udhaifu wa mitazamo ya kidhanifu na kiyakinifu katika kutoa maana ya fani na maudhui.

## Nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi

**Shughuli ya 3.4**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, eleza maana, sifa na umuhimu wa nadharia za uhakiki.

### Dhana ya nadharia na nadharia ya uhakiki

Wataalamu mbalimbali kama vile Massamba na wenzake (2009) na Mulokozi (2017) wanakubaliana kuwa nadharia ni utaratibu au mwongozo unaosaidia kueleza jambo fulani. Kwa msingi wa fasili hii, nadharia ya uhakiki ni mwongozo unaoelekeza namna ya kufafanua vipengele vya fani na maudhui ya kazi za fasihi.

Kwa muktadha wa kifasihi, Wafula na Njogu (2013) wanasema kwamba nadharia za uhakiki ni miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu kazi hiyo na vipengele vyake. Hivyo, nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi ni mawazo, maelezo au miongozo iliyopangwa ili kusaidia kufafanua vipengele mbalimbali vya kazi hizo.

### Sifa za nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi

Nadharia za uhakiki huwa na sifa zifuatazo:

(i) kuwa na malengo mahususi yanayokusudiwa kutimizwa;

(ii) kuwa na misingi mikuu ambayo ni mwongozo wa uchambuzi au uhakiki; na

(iii) kuwa na mpangilio inayojengana na kukamilishana katika kufafanua mambo yanayopatikana katika kazi husika.

### Umuhimu wa nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi

Nadharia za uhakiki zina umuhimu ufuatao:

(i) kumwongoza mhakiki katika uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi kupitia misingi na maudhui yake makuu;

(ii) kumsaidia mhakiki kuzielewa na kuzitumia nadharia mbalimbali za fasihi; na

FOR ONLINE READING ONLY

(iii) kumsaidia mhakiki kugundua jambo jipya au kuliboresha lililokuwapo awali.

## Uchambuzi wa nadharia teule za uhakiki wa kazi za fasihi

**Shughuli ya 3.5**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni au maktabani, taja nadharia nne (4) za uhakiki wa kazi za fasihi.

**Shughuli ya 3.6**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni au maktabani, fafanua maana na misingi ya nadharia ya umuundo katika kuhakiki kazi za fasihi.

### Nadharia ya umuundo

Umuundo ni nadharia ya uhakiki wa fasihi iliyojikita kwenye taratibu zilizopo katika uundwaji wa kazi ya kifasihi. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Ferdinand de Saussure (1857-1913) aliyeanzisha umuundo wa kiisimu. Wanamuundo wanaeleza kuwa lugha ni mfumo wa ishara nasibu, na kwamba kila kipengele kinahusiana na vipengele vingine katika mfumo huo. Kama ilivyo katika mfumo wa lugha, fasihi nayo imeundwa na vipengele vinavyotegemeana. Katika kazi ya fasihi kuna vipengele vya kisanaa vinavyojidhihirisha katika fani na maudhui. Vipengele hivyo huelezwa kwa kutegemeana, kwani hakuna kipengele kinachoweza kusimama peke yake bila kuhusishwa na kingine. Nadharia ya umuundo huonesha namna vipengele vya kazi ya fasihi vinavyohusiana na kufungamana hadi kuikamilisha kazi husika. Kwa jumla, wanaumuundo wanaeleza kuwa kazi ya fasihi haina urejelezi wa nje bali huonwa kama mfumo unaojitosheleza.

### Misingi ya nadharia ya umuundo

Misingi mikuu ya nadharia ya umuundo ni:

(i) lugha hutawaliwa na mfumo wa ishara, ambapo vipengele vinavyounda mfumo huo huweza kueleweka tu kwa kuangalia uhusiano wake na vipengele vingine katika mfumo huo wa lugha badala ya kuangalia nje ya mfumo wa lugha husika;

(ii) maana ya fasihi imejificha ndani ya mfumo wa lugha;

(iii) ishara haielezi wala haitoi uhusiano baina ya neno na kitu, bali ni muunganiko changamani kati ya dhana iliyopo akilini na ruwaza za sauti zinazoendana na dhana hiyo; na

FOR ONLINE READING ONLY

Katika kuchambua kazi ya fasihi kwa kutumia nadharia ya umuundo, unatakiwa kuchunguza matumizi ya lugha, na uhusiano wa vipengele vya lugha katika kutoa maana ya kazi hiyo. Pia, chunguza namna wahusika wanavyoitumia lugha kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Vilevile, chunguza jinsi taswira na ishara mbalimbali zilivyotumika kujenga maana ya kazi hiyo ya fasihi. Kadhalika, fafanua mpangilio wa vipengele vya kazi hiyo. Mathalani, iwapo unachambua shairi zingatia namna vina, mizani, vibwagizo, beti, na mpangilio kwa jumla vinavyosaidia kupatikana kwa maana ya shairi.

**Shughuli ya 3.7**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni au maktabani, fafanua maana na misingi ya nadharia ya umaksi katika kuhakiki kazi za fasihi.

### Nadharia ya umaksi

Umaksi ni nadharia inayozungumzia harakati za mwanadamu katika kupambana na utabaka uliomo katika jamii yake. Harakati hizo huhusiana na masuala ya uchumi, historia, siasa, jamii na mapinduzi, ambapo tabaka linalodhibiti njia kuu za uzalishaji mali huitawala na kuidhibiti jamii. Nadharia hii iliasisiwa na Karl Marx (1818 - 1883) na Friedrich Engels (1820 - 1895) kupitia kazi zao za *Das Kapital* (1867) na *Communist Manifesto* (1848). Jambo kubwa katika nadharia hii siyo kuufasili ulimwengu tu, bali kuubadilisha. Kwa mujibu wa Karl Marx, tabaka moja hutoweka na lingine huchipuka kwa sababu ya mgongano unaotokea kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Mgongano huo hutokea kwa sababu kila mara kuna tabaka la wanyonyaji na wanyonywaji.

Kwa jumla, nadharia ya umaksi huhusisha kazi za fasihi na uhalisi wa kijamii wa wakati kazi hizo zilipotungwa. Vilevile, nadharia hii huzingatia zaidi maudhui katika uhakiki wa kazi za kifasihi huku ikijikita katika kuhakiki maadili na njia za kuyaboresha maisha.

### Misingi ya nadharia ya umaksi

Nadharia ya umaksi ina misingi mbalimbali inayotumika katika uhakiki wa kazi za kifasihi. Misingi hiyo ni:

(i) kutumia historia ya binadamu kuakisi harakati za kitabaka zinazoendelea katika jamii;

(ii) kuvunjiliwa mbali kwa ubepari kama njia ya uzalishaji mali kutokana na jitihada mbalimbali za kitabaka za kuuangamiza;

FOR ONLINE READING ONLY

(iii) watunzi wa kazi za fasihi kuwa na jukumu la kufichua, kudadisi na kukosoa mifumo ya kibwanyenye;

(iv) kuwapo kwa kupigania haki za mtu/jamii; na

(v) kubainisha vipengele kama vile maadili, itikadi, dini na utamaduni na namna vinavyoathiri maisha ya jamii.

Unapochambua kazi ya kifasihi kwa kutumia nadharia ya umaksi, unatakiwa kuchunguza namna mwandishi anavyoibua harakati za kitabaka katika kazi hiyo, mifumo ya uzalishaji mali, namna kazi hiyo inavyodadisi mambo mbalimbali katika jamii, na kupigania haki za mtu/jamii. Pia, unatakiwa kuhakiki vipengele mbalimbali vya maisha (maadili, itikadi, dini na utamaduni), migongano ya kijamii, na muundo wa jamii kwa kuangalia hali ya uchumi wao. Zaidi, unatakiwa kubainisha msimamo wa mwandishi wa kazi hiyo katika kuleta mabadiliko kwa jamii. Iwapo unachambua tamthiliya kama vile *Kwenye Ukingo wa Thim* (Hussein 1988), *Nguzo Mama* (Muhando 1982), *Kivuli Kinaishi* (Mohamed 1990), *na Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Mbogo 1988), zingatia namna vipengele kama vile migogoro ya kitabaka inavyosawiriwa hadi kupatikana kwa haki ya wanyonge.

**Shughuli ya 3.8**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, fafanua maana na misingi ya nadharia ya ufeministi katika kuhakiki kazi za fasihi.

**Nadharia ya ufeministi**

Ufeministi ni nadharia iliyojikita kwenye harakati za kupigania ukombozi wa mwanamke dhidi ya mifumo kandamizi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mifumo hii imelenga kumkandamiza, kumnyonya na kumbagua mwanamke. Lengo la nadharia ya ufeministi ni kubainisha vipengele vya mifumo hii ili kupata suluhu ya matatizo yanayomkabili mwanamke katika hali mbalimbali.

Baadhi ya waasisi wa nadharia hii ni Mary Wollstonecraft (1759 - 1797), Virginia Woolf (1882 - 1941) na Simeon de Beauvoir (1908 - 1986). Awali ufeminisiti uliibuka kama vuguvugu la kisiasa, ambapo lengo lake lilikuwa kuwainua wanawake kutoka katika hali ya kukandamizwa, kunyanyaswa, na kutengwa; na hivyo, kuwawezesha kupata haki ya kujieleza. Wanafeministi wa mwanzo walizungumzia matatizo yao kwa njia ya maandishi au machapisho na wakati mwingine mihadhara. Walikosoa na kuzipiga vita asasi kama vile za dini, ndoa na utamaduni zinazomdhalilisha au kumdunisha mwanamke.

FOR ONLINE READING ONLY

Steady (1981) ni miongoni mwa waasisi wa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Huyu alitumia nadharia hii kubainisha dhuluma zilizokuwa zikimkandamiza mwanamke wa Kiafrika kama vile kutokuwa na uhuru wa kuchagua kuwa mzazi kwa wakati gani au kujichagulia mume; ukeketaji wa mwanamke, unyamavu wa kulazimishwa, urithi wa mali, mila za kurithiwa, rangi yake mwenyewe na kubaguliwa kwa mwamwake tasa.

Katika kutahadharisha kuhusu ufeministi, Badru (2019) anaeleza kuwa tangu kuanza kwa mawazo ya ufeministi ulimwenguni msisitizo mkubwa umekuwa ni namna gani wanawake wanaweza kujikomboa kwa kubadilisha mfumo-dume na kupata haki na wajibu sawa. Pamoja na hatua kubwa iliyopigwa, mapigano haya hayawezi kufanikiwa iwapo yatakuwa mapigano ya wanawake dhidi ya wanaume. Iwapo mwanaume ataachwa nyuma na asikombolewe kutoka katika ufungwa wa kifikra, kiutamaduni na kiuchumi alimofungwa hakuna namna ambavyo mapambano haya yatafanikiwa.

Ni vizuri kujua kuwa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika hainuii kuleta mgogoro na mvutano wa nafasi mbalimbali baina ya mwanamume na mwanamke katika jamii; bali unalenga kuamsha uelewa na usawa baina yao.

**Misingi ya nadharia ya ufeministi**

Ifuatayo ni misingi ya nadharia ya ufeministi ni:

(i) kukuza na kuendeleza umoja wa wanawake kupitia majukwaa mbalimbali;

(ii) kuleta usawa wa kijinsia katika maeneo mbalimbali kama malezi na mgawanyo wa majukumu;

(iii) kumpa mwanamke uhuru na nguvu ya kufanya maamuzi katika jamii;

(iv) kuelezea kwa undani hali ya mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo;

(v) kumpa mwanamke haki ya kushirikishwa na kushiriki katika masuala mbalimbali ya jamii;

(vi) kuhimiza mhusika wa kike katika kazi za fasihi awe mfano mzuri wa kuigwa katika jamii;

(vii) kutambua na kuthamini kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake; na

(viii) kuepuka usaguzi wa kimapokeo uliojengewa misingi ya kiimani na wenye mawazo hasi kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

Kwa hiyo, unapohakiki kazi ya fasihi kwa kutumia nadharia ya ufeministi, unatakiwa kuchambua masuala yanayohusiana na usawa wa kijinsia kati ya mwanamke na mwanamume katika nyanja za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa, na kiuchumi.

**Shughuli ya 3.9**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, fafanua maana na misingi ya nadharia ya uhalisia katika kuhakiki kazi za fasihi.

### Nadharia ya uhalisia

Nadharia ya uhalisia inahusu kusawiri na kuakisi maisha ya mwanadamu na mazingira. Nadharia hii inaepuka masuala ya unjozi na huyaelezea maisha kwa uyakinifu kama yalivyo katika jamii. Waasisi wa nadharia hii ni: George Wilhelm Hegel (1770-1831), Friedrich Schiller (1759-1805), na Gustave Flaubert (1821-1880). Nadharia hii husisitiza kuwa kazi ya sanaa ioneshe maisha ya binadamu jinsi yalivyo. Kimsingi, nadharia hii inaichukulia kazi ya fasihi kama kioo kinachoonesha masuala mbalimbali yanayohusiana na maisha ya binadamu.

### Misingi ya nadharia ya uhalisia

Ifuatayo ni misingi ya nadharia ya uhalisia ni:

(i) uwasilishaji wa maudhui ya kazi ya fasihi uzingatie hali halisi ya jamii;

(ii) mandhari ya kazi ya fasihi yaakisi mazingira halisi;

(iii) wahusika wasawiriwe kiyakinifu ili kuakisi maisha ya kila siku;

(iv) matukio katika kazi ya fasihi yaakisi mambo kama yalivyo kisiasa, kiuchumi, na kutamaduni na kijamii;

(v) changamoto za kijamii zitatuliwe kwa njia zinazothibitika kisayansi; na

(vi) lugha inayotumika kwenye kazi za fasihi iwe ile inayoeleweka kwa msomaji/hadhira lengwa.

Unapohakiki kazi ya fasihi kwa kutumia nadharia ya uhalisia, unatakiwa kuchunguza namna mwandishi alivyowaumba na kuwasawiri wahusika, matumizi ya lugha ya kawaida, namna matukio yanavyoakisi hali halisi, na jinsi mandhari ilivyochorwa. Vilevile, hakiki namna maudhui ya kazi hiyo yanavyoakisi hali halisi na ukweli wa maisha ya jamii husika.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 3.10**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, fafanua maana na misingi ya nadharia ya mwitiko wa msomaji katika kuhakiki kazi za fasihi.

**Nadharia ya mwitiko wa msomaji**

Nadharia ya mwitiko wa msomaji huhusu namna msomaji anavyoikabili, anavyoifasili na kuipa kazi ya fasihi maana kutokana na tajriba yake.

Mmoja wa waasisi wa nadharia hii ni Wolfgang Iser (1926 - 2007) ambaye anajulikana kama baba wa nadharia hii.

Kwa kawaida, mwandishi anapoandika kazi yake hutawaliwa na mambo kama vile mazingira, historia au muktadha wa jamii yake. Kwa upande mwingine, msomaji wa matini naye huathiriwa na mambo kama vile uelewa binafsi, aina ya matini anayosoma, utamaduni, mtindo wa usomaji, uzoefu wake juu ya jambo analolisoma, mazingira, historia, na matarajio yake. Mambo haya ndiyo husababisha tofauti ya uelewekaji wa matini baina ya msomaji mmoja na mwingine. Kwa hiyo basi, nadharia hii huhusisha mambo matatu: mtunzi wa kazi ya fasihi, kazi husika ya fasihi, na hadhira. Pia, husisitiza kuwa hadhira hukamilisha maana kwa sababu msomaji ndiye anayelengwa na mwandishi; pia maana ya matini inategemea namna msomaji atakavyoelewa.

**Misingi ya nadharia ya mwitiko wa msomaji**

Ifuatayo ni misingi ya nadharia ya mwitiko wa msomaji:

(i) kazi ya fasihi haina maana moja;

(ii) maana ya kazi ya fasihi hukamilishwa na miktadha mbalimbali inayotokana na tajriba ya msomaji;

(iii) mchakato wa usomaji na uelewaji wa kazi ya fasihi huhusisha matarajio ya msomaji; na

(iv) tofauti za kitamaduni, kielimu, kisiasa, na kiuchumi husababisha tofauti za maana ya kazi ya fasihi kati ya msomaji mmoja na mwingine.

Unapohakiki kazi ya fasihi kwa kutumia nadharia ya mwitiko wa msomaji unatakiwa kuzingatia misingi iliyobainishwa.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 3.11**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, fafanua maana na misingi ya nadharia ya mwingilianomatini katika kuhakiki kazi za fasihi.

**Nadharia ya mwingilianomatini**

Nadharia ya mwingilianomatini inahusu namna matini moja inavyohusiana na matini nyingine. Kwa jumla, nadharia hii husisitiza kwamba kila kazi ya kifasihi kwa namna moja au nyingine inahusiana na kazi iliyoandikwa kabla au kazi nyingine mbalimbali. Katika uhusiano huo, vipengele vya kifani na kimaudhui vya kazi moja ya mwanzo huathiri kazi mpya kwa namna ambayo huonesha kufanana kwa vipengele vya kazi hizo.

Nadharia ya mwingilianomatini iliasisiwa na Julia Kristeva (1941 hadi sasa) kutokana na mawazo aliyoyapata katika nadharia ya usemezano iliyoasisiwa na Mikhail Bakhtin (1895-1975). Kristeva anaitazama dhana ya mwingilianomatini kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya maana ya matini moja kueleweka kwa kuhusisha na matini nyingine.

**Misingi ya nadharia ya mwingilianomatini**

Ifuatayo ni misingi ya nadharia ya mwingilianomatini:

(i) hakuna matini inayoweza kuchunguzwa peke yake kwa kujitegemea, bali lazima pawe na matini nyingine iliyotangulia inayohusiana na matini hiyo mpya;

(ii) matini za kifasihi huchota, hunukuu, hugeuza, na kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine; na

(iii) kazi za kifasihi huundwa kutokana na tamaduni mbalimbali zinazopatikana katika matini mbalimbali za kifasihi na zisizo za kifasihi.

Kwa hiyo, unapohakiki kazi ya fasihi kwa kutumia nadharia ya mwingilianomatini unatakiwa kuangalia uhusiano wa matini moja na matini nyingine kwa kutumia ulinganishi wa vipengele vya kifani na kimaudhui katika kazi mpya na zile za awali. Kwa mfano, unaweza kuchunguza namna wahusika walivyochorwa, jinsi mandhari yanavyoathiri tabia na matukio katika kazi ya fasihi, matukio mbalimbali ya kihistoria, mtindo na mbinu za uandishi, mwingiliano wa kiutamaduni, na uwasilishwaji wa maudhui. Pia, unaweza kuchunguza mwingiliano wa fasihi simulizi na andishi, mwingiliano wa tanzu, na mwingiliano wa vipera.

FOR ONLINE READING ONLY

Mpaka hapa umejifunza baadhi ya nadharia muhimu zinazotumika katika uhakiki wa kazi za fasihi. Nadharia hizi zitakupa mwongozo katika kuchambua kazi mbalimbali za kifasihi.

**Shughuli ya 3.12**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, eleza sifa na dhima za mhakiki wa kazi za kifasihi.

## Kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia nadharia za kifasihi

Taaluma ya uhakiki ilianza zamani, tangu enzi za mwanafalsafa wa zamani wa Kiyunani, Plato, (takribani miaka ya 428 - 348 K.K). Nchini Tanzania, taaluma hii ilianza kutumika zaidi miaka ya 1970 baada ya baadhi ya Watanzania kusoma taaluma ya fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongoni mwao walikuwa John Ramadhani, May Balisidya, Saifu Kiango, Euphrase Kezilahabi, na Mbunda Msokile. Wengine ni pamoja na Farouk Topan, Tigiti Sengo, Fikeni Senkoro na Mugyabuso Mulokozi.

Unapohakiki kazi ya fasihi unachambua na kutathmini mawazo au masuala mbalimbali yaliyomo katika kazi hiyo. Mbali na kuwa na maarifa ya nadharia zinazoongoza katika kuchambua kazi za fasihi, unapaswa kufahamu historia na siasa ya jamii inayohusika ili uweze kuelewa masuala muhimu katika jamii husika. Halikadhalika, inakulazimu kusoma kazi nyingine za fasihi tofauti na ile unayoihakiki ili uwe na ujuzi zaidi katika uwanja wa uhakiki. Vilevile, unapohakiki kazi za fasihi ni muhimu kujua historia na mazingira yaliyomkuza mwandishi au msanii; na mwisho kueleza bayana ubora na upungufu wa kazi husika.

Ukiwa na ufahamu wa kutosha kuhusu nadharia, itakuwia rahisi kuamua ni nadharia gani uitumie katika kuhakiki kazi fulani ya fasihi. Uteuzi wa nadharia ya kutumika hutegemea mwelekeo wa jumla wa kazi inayohakikiwa pamoja na kipengele au vipengele mahususi unavyotaka kuvifanyia uhakiki.

Kumekuwa na mjadala kuhusu nafasi ya mhakiki wa kazi za fasihi. Mjadala huu umetokana na kuwapo kwa mitazamo miwili inayopingana kuhusu nafasi ya mhakiki huyo. Mtazamo wa kwanza unaona kwamba msanii na mhakiki ni watu ambao wanahitajiana kwa sababu mhakiki ndiye anayeieleza na kuitambulisha kazi ya msanii kwa hadhira. Vilevile, mhakiki ndiye anayemtahadharisha mwandishi kuhusu makosa aliyoyafanya ndani ya kazi yake na kumfanya awe makini zaidi katika kushughulikia kazi nyingine. Aidha, mhakiki ni kiungo muhimu kati ya jamii na msanii kwa sababu hutumia ujuzi wake wa kuchambua



FOR ONLINE READING ONLY

kazi ya sanaa ili kubainisha maadili, ujumbe, msimamo na falsafa ya kazi hiyo kwa wanajamii. Kwa mujibu wa mtazamo huu, mhakiki ni mwalimu wa jamii kwa kuwa humfundisha msomaji kuhusu yale yaliyomo katika kazi ya fasihi. Aidha, mhakiki humweleza mwandishi kuhusu mambo yaliyomo katika kazi yake ambayo yanakubalika au hayakubaliki kwa jamii (Senkoro, 1973).

Mtazamo wa pili haumchukulii mhakiki kama mtu muhimu katika fasihi. Hii ni kwa sababu, mwandishi ndiye mhakiki mwenyewe. Hivyo, huweza kujikosoa na kurekebisha kazi yake mpaka anaporidhika nayo. Mtazamo huu pia huona kuwa mhakiki anajipachika vyeo ambavyo hastahili kwa kusema kuwa ni mwalimu wa msanii na msomaji kwa sababu wasomaji wa kazi za fasihi wana uwezo wa kusoma na kuelewa; na hawahitaji watu wa kuwafafanulia. Kila msomaji anaaminika kuwa na uwezo wa kuchambua kazi inayohusika; uchambuzi hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Kwa mantiki hiyo, haitakiwi kumtegemea mhakiki ambaye naye ana mawazo yake kulingana na uwezo wake wa kuchambua na kufafanua kazi inayohusika (Mbele, 1993).

Kwa mtazamo wa kwanza, mhakiki wa kazi za fasihi ana dhima zifuatazo:

(i) Kuchambua kila kipengele cha fani na maudhui.

(ii) Kubainisha dhamira zinazotolewa katika kazi za fasihi.

(iii) Kuhimiza na kushirikisha fikra za kihakiki kwa wanataaluma wengine.

(iv) Kukuza kiwango cha usomaji wa kazi za fasihi.

(v) Kumwelekeza msomaji ili apate maarifa zaidi.

(vi) Kufafanua nadharia zilizotumika katika kuhakiki kazi husika.

(vii) Kubainisha misingi bora ya uandishi wa kazi za fasihi.

(viii) Kuonesha uzuri na upungufu wa kazi iliyohakikiwa kwa lengo la kuelimisha jamii na waandishi wa kazi za fasihi.

## Zoezi la 3.2

1. Eleza tofauti kati ya nadharia na nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi.
2. Jadili kwa kutumia mifano umuhimu wa nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Linganisha nadharia za umuundo na umaksi zinavyotumika katika uchambuzi wa kazi za fasihi.
4. Fafanua tofauti zilizopo kati ya nadharia ya mwingilianomatini na mwitiko wa msomaji.
5. Eleza tofauti zilizopo kati ya nadharia ya ufeministi na uhalisia.
6. Mhakiki hana nafasi katika kazi za fasihi. Jadili.
7. Kwa kutumia mifano, fafanua mitazamo kuhusu mhakiki wa kazi ya fasihi kisha toa maoni yako.

**Kuhakiki maigizo, mashairi, na tamthiliya kwa kutumia nadharia za kifasihi**

Uchambuzi wa kazi za fasihi kwa kutumia nadharia za kifasihi huzingatia misingi ya uhakiki ya nadharia husika. Hivyo, mhakiki anapaswa kuzingatia misingi ya kila nadharia katika kuhakiki kazi za kifasihi. Ufuatao ni ufafanuzi wa namna ya kuhakiki maigizo, mashairi na tamthiliya kwa kutumia nadharia za kifasihi.

**Kuhakiki maigizo kwa kutumia nadharia za kifasihi**

**Shughuli ya 3.13**

(a) Tazama igizo katika runinga au vifaa vingine vya TEHAMA, kisha hakiki igizo hilo kwa kutumia nadharia ya uhalisia, huku ukiongozwa na maswali yafuatayo:
  (i) Ni kwa namna gani maudhui yaliyowasilishwa na wahusika katika maigizo hayo yanaakisi hali halisi katika jamii?
  (ii) Ni kwa namna gani uumbaji wa wahusika katika maigizo hayo unaakisi hali halisi?
  (iii) Maudhui yanayowasilishwa katika maigizo hayo yana athari gani kwa jamii?
  (iv) Je, lugha ya wahusika katika maigizo hayo ina uhalisi?
  (v) Ni kwa namna gani mandhari ya maigizo hayo yanasawiri mazingira halisi?

FOR ONLINE READING ONLY

(b) Tazama maigizo katika runinga au vifaa vingine vya TEHAMA, kisha chambua maigizo matatu kwa kutumia nadharia ya mwitiko wa msomaji, huku ukiongozwa na maswali yafuatayo:

(i) Ni maana zipi zinaweza kupatikana katika maigizo hayo?

(ii) Kwa maoni yako, ni miktadha gani imetumika katika utunzi wa maigizo hayo?

(iii) Je, msomaji anaweza kupata athari zipi kutokana na maigizo hayo?

(iv) Maigizo hayo yana uhusiano gani na mazingira yako?

(v) Una maoni gani kuhusu usahihi wa maigizo hayo?

Kutokana na kufanya shughuli ulizopewa, na kujibu maswali uliyoulizwa, utakuwa umejifunza namna ya kuzitumia nadharia za uhalisia na mwitiko wa msomaji katika kuhakiki kazi za fasihi.

**Kuhakiki mashairi kwa kutumia nadharia za kifasihi**

**Shughuli ya 3.14**

Soma na hakiki shairi lifuatalo kwa kutumia nadharia ya umuundo.

**Hutaniacha Morogoro**

1. *Ninapotazama saa, ni saa saba mchana,*
*Watu wengi wamekaa, stendi wasukumana,*
*Nasikia "Daa! Daa! Basi lenu mwaliona!"*
*Kondakta kwa kupaaa, sauti hiyo anena,*
*Ndipo ninapoutwaa, mfuko naingizana,*
*John ananiambia, "hutan'acha Morogoro!"*

2. *Niingiapo basini, kuna mtu anikuna,*
*Anipapasa begani, kama vile twajuana,*
*Najifanya simuoni, pilika zimenibana,*
*Ghafula aja usoni, namwona ana kwa ana,*
*Kumbe ni kijana John, ni mwanangu wa ujana,*
*John ananiambia, "hutan'acha Morogoro!"*

FOR ONLINE READING ONLY

3. *Macho yamtoka pima, John amekasirika,*
*Namuona anasema, "Baba ananitoroka?"*
*Ninabaki najiuma, nini kimempeleka,*
*"Sikiliza John Chema", ninamtoa mashaka,*
*"Nakwenda Moro tazama, wazazi wananitaka",*
*John ananiambia,* "hutan'acha Morogoro!"

4. *Kwa dakika kumi nzima, John hasemi na mie,*
*Mgongoni aniuma, nusura nyama ang'oe,*
*Hapo nasogea nyuma, namvua an'achie,*
*Siwi tena na huruma, namshika nimtoe,*
*"Nakufa mwenzenu jama", aita wamsa'die,*
*John ananiambia, "hutan'acha Morogoro!"*

5. *Nje ninapomtoa, namfungia mlango,*
*Hapo John analia, ajitupa kwenye dongo,*
*Gari anang'ang'ania, kama mchwa na udongo,*
*Mara anaiachia, imgusapo mgongo,*
*Huku anitamkia, atakamilisha lengo,*
*John ananiambia, "hutan'acha Morogoro!"*

6. *Sikose kuendelea, sehemu yake ya pili,*
*Ni nini kitatokea, Moro nitapowasili,*
*John ameshapania, kunif'ata kila hali,*
*Moro kanitamkia, atafika hatojali,*
*Tena kasisitizia, yeye mwanangu halali,*
*John ananiambia, "hutan'acha Morogoro!"*

*Diwani ya Mloka* (Mloka, 2002: 28 - 29).

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 3.15**

(a) Hakiki mashairi mawili kutoka katika diwani teule kwa kutumia nadharia ya umuundo.

(b) Soma shairi lifuatalo, kisha hakiki kwa kutumia nadharia ya ufeministi kwa kujibu maswali yafuatayo.

**Maisha ya Ndoa**

**Mume**

*Nimeagiza chakula, wanisogezea uji,*
*Nikiangalia saa, ni mwanana adhuhuri,*
*Ni ya msosi majira, umenitengea nini?*
*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

**Mke**

*Mboga unga na mkaa, mwenzangu mi' sivioni,*
*Nimechoka kulalama, mapenzio siyaoni?*
*Unazicheza karata, pesa zako sizioni,*
*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

**Mume**

*Wewe mke sikiliza, tena usiwe shubiri,*
*Makonzi nitakutia, mke gani we bilisi!*
*Umepuya huna uja, hatari bora ya chui,*
*Haya maisha ya ndoa, mwenzangu mnaishije?*

**Mke**

*Mume tega masikia, nisikize kwa makini,*
*Majukumu nayajua, jikoni hadi chumbani,*
*Kuchapana zilipendwa, ndoa sio utumwani,*
*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

FOR ONLINE READING ONLY

**Mume**

*Mshahara unapewa, wako hauparuliwi,*

*Majukumu kugawana, napalangania denti,*

*Bado pango nalipia, umeme na maji ni mimi,*

*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

**Mke**

*Mke si wa kuteseka, wangu sema asilani,*

*Zipunguze zako nongwa, kulalama hakufai,*

*Kucha nywele nasetia, kusaidia nyumbani,*

*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

**Mume**

*Mke msomi ni shida, wanaume tuna kazi,*

*Ya wahenga nikapuza, nikijua ni kejeli,*

*Viuno wajishikia, wanawaza ofisini,*

*Haya maisha ya ndoa, mwenzangu mnaishije?*

**Mke**

*Vyombo maji saidia, dawa tosha ya mapenzi,*

*Mke hawezi kutoka, atajituliza ndani,*

*Atakiandaa chanda, kando yatatengwa maji,*

*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

*Mwanamke ndege njiwa, apetiwe peti peti,*

*Asiguswe kwa mabaya, atapeperuka mbali,*

*Haloo wangu kibamba, toa maneno laini,*

*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

FOR ONLINE READING ONLY

**Mume**

*Aaa! nimetambua, tumtafute Uledi,*
*Ili apike chakula, afue nguo nyumbani,*
*Akitandike kitanda, adeki na sebule,*
*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*
*Nguo zetu kunyoosha, anifunge yangu tai,*
*Viatu vyako kuvaa, afunge yangu lesani,*
*Mke wangu pumzika, kwa uchovu wa kazini*
*Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?*

*Kurunzi (Mbijima, 2019: 17 – 20)*

(i) Shairi hili lina nafasi gani katika kuleta usawa wa kijinsia katika jamii?

(ii) Mshororo usemao "mke msomi ni shida, wanaume tuna kazi" unaibua hisia gani?

(iii) Ni kwa namna gani shairi hili linaipambanua hali ya mwanamke kiuyakinifu?

(iv) Jadili uumbaji wa wahusika katika shairi hilo?

(v) Ni kwa namna gani shairi hili linaakisi maisha halisi ya jamii?

(c) Hakiki mashairi mawili kutoka katika diwani teule kwa kutumia nadharia ya ufeministi.

Kutokana na kufanya shughuli ulizopewa, na kujibu maswali uliyoulizwa, utakuwa umejifunza namna ya kuzitumia nadharia za umuundo na ufeministi katika kuhakiki kazi za fasihi.

**Shughuli ya 3.16**

(a) Hakiki kipande cha tamthiliya kifuatacho kwa kutumia nadharia ya umaksi ukiongozwa na maswali yanayofuata.

*(Mahali ni palepale kama kwenye onesho la kwanza. Mapambo yameondolewa. Martha amekaa kwenye kiti cha marehemu. Chris ameweka kichwa chake katika mikono yake. Martha anajishughulisha kuandaa chakula cha mchana)*

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| **Chris:** | Ma! Mimi nani? |
| **Martha:** | Wewe? (*Kimya*) Wewe Chris. |
| **Chris:** | Chris! Chris! (*Ana uchungu*) Haunielewi. Na maana: Mimi hasa ni nani? Bado haujaelewa. |
| **Martha:** | Naelewa. Unatoka kusikiliza maneno ya wahuni barabarani.<br>(*Baada ya muda*)<br>Mimi Martha. Wewe Chris. |
| **Chris:** | Kila ukiniandikia barua, ukizungumza kwenye simu, unanieleza habari ya familia. Iko wapi familia? Mbona… |
| **Martha:** | Sitaki maneno hayo.<br>(*Kimya*) |
| **Chris:** | (*Anasikitika*)<br>Baba, maskini, baba! |
| **Martha:** | Mwisho… Jambo la mwisho kabisa baba yako angependa kusikia… ni huku kuomboleza, kuomboleza. |
| **Chris:** | Baba yangu? Kwani kweli baba yangu?<br>(Kibao) |
| **Martha:** | Sijui huko Amerika wanafundisha nini? Ukitoka nje, ukirudi mara hili. Sasa hujui mimi nani, wewe nani? Umechanganyikiwa. Unalialia na kupenga makamasi tu hapa. Lakini utakua kweli wewe, ukawa mtu hasa wa kukutegemea? Baba zima. Litazame. Utaweza kushika madaraka ya aina yoyote wewe? Utaweza kusimama mahali pa baba yako? |
| **Chris:** | Kushika mahali pa baba? Nani atanisikiliza? Nitaanzaje? Huku siko… siko kokote!<br>(*Analia*) |
| **Martha:** | Msikilize, hana hata haya. Unajua maana ya kuachiwa kichwa cha tembo? Haujui. |

FOR ONLINE READING ONLY

Basi baba yako katuachia kichwa cha tembo. Tumewinda pamoja. Jamaa zake amewapa meno na usinga. Na sisi ametuachia kichwa cha tembo. Sasa naelewa kwa nini hakutia saini hati. Mwenyekiti sasa hivi anatayarisha mazishi ya Herbert.

Anataka kumzika Herbert Kikiristo. Hiyo ni dhima yetu. Ni dhima yangu. Anataka kumzika Herbert na kuandikisha kila kitu katika jina la Umma Klan.

Kila kitu. Nyumba, viwanja, gari, fanicha kila kitu.

Unavyotuona hapa, sisi ni maskini. Ndiyo maisha ya mwanamke. Unapoteza mume. Unapoteza maisha. Unapoteza kila kitu.

(*Kimya*)

Na wewe unafanya nini? Unalialia tu hapa. Utaniona mimi kulia? Unaniona mimi kujiuliza maswali ya kijinga? Hapana! Kwa sababu najuwa mimi nani? Na wajibu wangu ni nini?

(*Kimya*)

Kweli, kuna wakati hata mimi natamani ningekuwa maiti, simo katika maisha, nikaepukana na ujinga huu.

(*Anabadilisha sauti. Anakumbuka*)

Ingekuwa uzuri ningekufa siku ile nilipokuwa msituni. Ilikuwa siku za Mau Mau. Nilikuwa naumwa malaria kali sana. *Scouts* walikuwa wanatutafuta. Walipata habari wapi tumejificha. Wenzangu wote walikimbia. Wapiganaji wawili, Njiru na mwenziwe, walipigwa risasi wakafa palepale msituni. Mimi nikajikokota. Nikajificha kwenye kichaka, kwenye majani.

*Scouts* wakaja mpaka pale nilipokuwa. Ajabu! Sikuogopa. Nilikuwa tayari mimi kufa.

(*Kimya*)

Ingekuwa uzuri ningekufa! Ningekufa peke yangu kuliko hivi. Watu chungu nzima! Rafiki tele! Bure tu. Jamaa zangu damu moja. Wamenitenga siku ya ndoa.

FOR ONLINE READING ONLY

Ben peke yake ndiye aliyekuwa na mimi. Jamaa za mume wangu vilevile, walimtenga siku hiyohiyo ya ndoa. Lakini nikaona si kitu tutaishi. Mimi, wewe, Herbert. Kwa nini isiwezekane ikiwa pendo lipo? Kwa nini tusiweze? Lakini hata hi…

Chris: Ma!

*(Kimya, Mtu anagonga mlango)*

Martha: Mtazame nani.

*(Ingia George)*

George: Habari Martha.

*(Martha hajibu)*

A-a! Chris

*(Chris hajibu. Baada ya muda)*

George: Nimekuja kuchukua hati.

Martha: Hati?

George: Tunataka kuchukua maiti kutoka hospitali.

(Kimya)

Martha: Sina hati. Sisi tutamzika hapa. Nimeshamwomba Pasta atatusaidia kumzika. Tumewaambia marafiki zetu watakuja. Na wewe…

George: Utamzika wapi?

Martha: Hapa! Pale.

(Anaonesha nje ya dirisha)

George:: Ndivyo alivyousia marehemu?

Martha: Ndiyo.

George: Hakikisha.

Martha: Usinifokee. Kama unataka kufoka nenda nyumbani kwako.

FOR ONLINE READING ONLY

George: Bado haujaelewa. Ninyi mko ndani ya madaraka yangu.

Martha: Nini?

George: Mko chini…

Martha: Katika nyumba hii wewe huna madaraka yoyote! Tena tafadhali ondoka.

George: Ond …

(Hakudhani kuwa Martha atasema hivyo)

Unajua unasema nini?

Martha: Nasema nini?

George: Labda huelewi. Herbert hakukueleza. Kimila, mimi ni mkubwa wa Herbert. Mama yangu aliolewa, halafu mama aliyemzaa Herbert.

*Kwenye Ukingo wa Thim* (Hussein, 2004: 24 - 28)

**Maswali**

(i) Mgogoro kati ya Martha na George unatokana na nini?

(ii) Kuna uhusiano gani kati ya mambo yanayosawiriwa katika kipande hiki cha tamthiliya na jamii yako?

(iii) Kutokana na matini hii, ni kwa namna gani mwandishi anasawiri matabaka na mifumo mbalimbali ya maisha katika jamii yako?

(iv) Jamii inapaswa kufanya nini ili kuepusha migogoro kama inavyosawiriwa katika matini hii?

(v) Kwa namna gani matini hii imesawiri upiganiaji wa haki na suluhu yake?

(vi) Utamaduni umeathirije maisha ya familia ya Herbert na Martha katika matini hii?

(b) Hakiki tamthiliya moja teule kwa kutumia nadharia ya umaksi.

(c) Hakiki tamthiliya moja teule kwa kutumia nadharia ya mwingilianomatini.

FOR ONLINE READING ONLY

Kutokana na kufanya shughuli ulizopewa, na kujibu maswali uliyoulizwa, utakuwa umejifunza namna ya kuzitumia nadharia za umaksi na mwingilianomatini katika kuhakiki kazi za fasihi.

**Shughuli ya 3.17**

Kwa kutumia kazi za ushairi au tamthiliya teule, eleza mchango wa nadharia ya mwingilianomatini katika maendeleo na uhakiki wa tanzu hizo.

## Kutathmini mchango wa nadharia teule za uhakiki wa kazi za fasihi katika maendeleo ya ushairi na tamthiliya

Kila utanzu wa fasihi hupitia mabadiliko yanayotokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo huweza kuwa za kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi, na kitaaluma. Yote haya huathiri pia maendeleo na kukua kwa taaluma ya uhakiki ambapo wahakiki huwa na wigo mpana wa kuibua na kutumia nadharia mbalimbali za kihakiki. Mathalani, katika utanzu wa ushairi mabadiliko yaliyotokea hadi kuibua mvutano baina ya washairi wa kijadi/kimapokeo na wa kisasa ulichangia katika kuibua mawazo na aina mpya ya ushairi. Kutokana na hali hii maana ya ushairi wa Kiswahili ilibadilika. Halikadhalika, utanzu wa tamthiliya ulipitia mabadiliko yaliyotokana na udadisi na ubunifu wa wanatamthiliya na wahakiki waliosaili utunzi unaofuata kanuni za Kiaristotle. Utanzu wa tamthiliya za Kiswahili ukaanza kutumia kanuni za kijadi za fasihi simulizi, sanaa za maonesho za Kiafrika, pamoja na kuakisi mazingira ya Kiafrika. Mchakato huo uliibua tamthiliya za Kiswahili zenye ladha ya Kiafrika.

Mabadiliko na maendeleo ya tanzu za ushairi na tamthiliya yaliathiri na kuibua nadharia mbalimbali za uhakiki zilizochangia maendeleo ya tanzu hizi. Nadharia hizi zimeendelea kutumika kama mwongozo wa jumla katika kujenga hoja wakati wa kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi. Vilevile, nadharia hizi humsaidia mhakiki kuibua na kuchochea udadisi katika kubaini changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii. Halikadhalika, nadharia humsaidia mhakiki kuchunguza na kuifahamu jamii katika nyanja mbalimbali, kama vile za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Aidha, nadharia humsaidia mhakiki kujenga hoja na kumwezesha kuweka bayana changamoto au matatizo yanayoikumba jamii. Pia, humwezesha mhakiki kugundua au kuboresha jambo jipya. Kwa msingi huo, nadharia ni muhimu sana katika maendeleo ya kazi mbalimbali za fasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la 3.3

1. "Katika kuhakiki kazi za kifasihi, mhakiki hujiegemeza katika vipengele mbalimbali vya nadharia". Jadili kauli hii kwa kutumia mifano ya nadharia mbili unazozipenda.
2. Jadili namna vipengele vya kifani katika shairi vinavyotofautiana na vipengele vya kifani katika tamthiliya.
3. Jadili vipengele vya maudhui vinavyopatikana katika mashairi mawili kutoka diwani teule ulizosoma.

## Tamrini

1. Kwa kutumia mifano, tofautisha dhana zifuatazo:
   (a) fani na maudhui
   (b) nadharia na uhakiki
   (c) mtindo na muundo
   (d) tamathali za usemi na mbinu nyingine za kisanaa
2. Fafanua kwa kina nadharia zifuatazo ukizingatia maana, misingi na matumizi yake katika uchambuzi wa kazi za kifasihi:
   (a) uhalisia
   (b) umuundo
   (c) mwingilianomatini
   (d) umaksi
   (e) mwitiko wa msomaji
   (f) ufeministi

FOR ONLINE READING ONLY

3. Kwa kutumia mifano ya kutosha, tofautisha mitazamo ya kidhanifu na kiyakinifu kuhusu fani na maudhui.

4. "Nadharia za kifasihi humlemaza mhakiki". Jadili.

5. "Usomaji na uelewa wa kazi fulani ya fasihi hutofautiana baina ya mtu mmoja na mwingine". Thibitisha kauli hii kwa kuchambua tamthiliya teule moja huku ukitumia nadharia ya mwitiko wa msomaji.

6. Chagua nadharia mbili za kihakiki kisha uzitumie kuchambua tamthiliya mbili teule.

7. "Suala la ukandamizaji na unyanyasaji wa wanawake katika jamii linapigiwa kelele na waandishi mbalimbali wa kazi za fasihi". Tumia nadharia ya ufeministi kuthibitisha kauli hiyo kwa kuhakiki tamthiliya teule mbili.

8. Hakiki tamthiliya teule mbili za waandishi chipukizi kwa kutumia nadharia ya mwingilianomatini.

9. "Hakuna jamii isiyokuwa na matabaka". Tumia nadharia ya umaksi kuhakiki kauli hiyo katika tamthiliya teule mbili.

10. "Kwa kuwa kila msanii na msomaji wa kazi za fasihi ni mhakiki, hakuna haja ya kuwa na mtu anayejiita mhakiki". Kubali au kanusha dai hili kwa hoja maridhawa.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nne

# Maadili katika fasihi

## Utangulizi

*Maadili katika kazi za fasihi ni muhimu kwani husaidia kujenga mwenendo na tabia inayokubalika katika jamii. Hivyo, kazi za fasihi zimekuwa chachu ya kubadilisha jamii kupitia ujumbe unaopatikana katika kazi hizo. Katika sura hii, utajifunza maadili yaliyomo katika nyimbo za bongo fleva, mashairi, na tamthiliya. Pia, utajifunza misingi ya maadili, umuhimu wa maadili katika jamii na maadili yaliyosawiriwa katika kazi za fasihi. Vilevile, utajifunza namna ya kueleza na kuhusianisha mitazamo iliyomo katika kazi hizo za fasihi na matendo ya jamii na athari za kiimani na kimtazamo zinavyodhihirika katika jamii. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutunga kazi za fasihi zenye kujenga maadili kulingana na mtazamo na imani ya jamii husika.*

*Kazi za fasihi zinavyochochea ujenzi wa maadili katika jamii*

## Maadili katika nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya

**Shughuli ya 4.1**

Sikiliza au tazama nyimbo za bongo fleva kisha bainisha wimbo mmoja unaodhani una maadili na wimbo mwingine unaodhani hauna maadili na eleza kwa nini unasema wimbo fulani umezingatia maadili au la.

### Maadili ni nini?

Maadili ni kanuni, miongozo na taratibu zilizowekwa na jamii ili kusimamia mienendo na tabia za watu zinazokubalika katika jamii husika. Maadili huathiri

FOR ONLINE READING ONLY

maamuzi, tabia na uhusiano wa watu katika maisha ya kila siku. Baadhi ya watunzi na waandishi wa kazi za sanaa huyapa kipaumbele maadili katika kazi zao. Kutokuzingatia misingi ya maadili katika utunzi wa kazi za kifasihi huchangia kumomonyoka kwa maadili katika jamii. Hivyo basi, misingi hiyo inapaswa kuzingatiwa katika utunzi wa kazi mbalimbali za kifasihi, zikiwamo nyimbo za bongo fleva mashairi na tamthiliya.

**Misingi ya maadili katika jamii**

Misingi ya maadili huweza kutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Hata hivyo, kuna misingi ya jumla ambayo hutawala katika jamii mbalimbali. Baadhi ya mifano ya misingi hiyo ni heshima, utii, haki na usawa, uwajibikaji, uaminifu na uwazi:

(i) Heshima: ni hali ya kujithamini na kuwathamini wengine, mali na mazingira yao. Heshima huweza kujengwa kwa ukarimu, uvumilivu, uelewa na kuthaminiana miongoni mwa watu. Aidha, heshima hudumisha umoja, amani, maelewano, nidhamu na maendeleo ya jamii.

(ii) Utii: kipengele cha maadili ambacho huhusiana na nidhamu na kukubali maagizo au majukumu ambayo mtu hupewa, aghalabu na mtu aliye juu yake kiumri au kimamlaka. Pia, utii huendana na kuafiki au kutekeleza sheria au miongozo ya kijamii. Msingi huu wa uadilifu huleta maendeleo katika jamii na huchochea kuwapo kwa umoja na ushirikiano.

(iii) Haki na usawa: katika jamii yenye haki na usawa, watu wanapaswa kuwa salama, wenye uhuru kamili, na wasio na hofu ya kudhulumiwa wala kutengwa. Haki na usawa hulinda watu dhidi ya ubaguzi wowote, kwa misingi ya rangi, jinsi, dini, au utaifa. Kila mmoja ana thamani na mchango katika kuleta maendeleo ya jamii yake. Hivyo, jamii inayotambua haki na usawa hutoa elimu bora, huduma za afya na fursa za kiuchumi kwa usawa ili kujenga maisha bora kwa mtu mmojammoja na wanaomzunguka.

(iv) Uwajibikaji: unahusu kutimiza majukumu kikamilifu na kwa wakati. Kila mtu anapaswa kutekeleza majukumu yake ili kuleta tija na maendeleo katika jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

(v) Uaminifu ni hali ya mtu kuwa mnyoofu mwenye tabia njema inayosababisha akubalike na watu na jamii inayomzunguka. Uaminifu huzingatia msimamo alionao mtu bila kuathiriwa na ushawishi wa mtu mwingine. Uaminifu hujenga imani na heshima. Pia, huimarisha uhusiano mwema kuanzia ngazi ya familia na maeneo mengine kama vile kazini, kwenye nyumba za ibada, na kwenye asasi na taasisi mbalimbali.

(vi) Uwazi: unahusu fursa ya kila mwanajamii kujua mambo ya kimaendeleo yanayotokea au kufanyika katika jamii yake. Uwazi pia hutakiwa kudhihirishwa na kila mmoja kuanzia katika ngazi ya familia.

**Umuhimu wa maadili katika jamii**

Maadili hujenga amani na utulivu na huleta umoja, ushirikiano na kuheshimiana miongoni mwa wanajamii. Hali hii huondoa vitendo vya ukatili na uonevu ambavyo huweza kusababisha migogoro au machafuko katika jamii.

Zaidi ya kuleta maendeleo katika jamii, maadili huwafanya watu wawe wawazi, wakweli, na waaminifu katika kutunza mali au rasilimali za umma. Mathalani, viongozi waadilifu huweza kuchangia maendeleo kwa kusimamia vizuri rasilimaliwatu na rasilimalifedha zilizoko katika maeneo yao ya kazi. Vilevile, maadili hujenga uzalendo na kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maendeleo binafsi na ya jamii kwa ujumla. Maadili huwafanya watu watambue umuhimu wa kushiriki katika miradi ya kijamii na kuchangia katika maendeleo ya sekta mbalimbali kama vile elimu na afya. Zaidi ya hayo, maadili hupunguza ufisadi, uhalifu na migogoro katika jamii. Kwa hiyo, maadili huchangia katika kuboresha maisha ya watu na kujenga ustawi. Umuhimu wa maadili umeweza kudhihirika katika kazi za fasihi kama vile bongo fleva, mashairi na tamthiliya kama inavyofafanuliwa hapa chini:

**Maadili katika nyimbo za bongo fleva**

Nyimbo za bongo fleva zilianza kuimbwa kuanzia miaka ya 1990 hadi sasa na zimekuwa zikiimbwa na kupendwa sana na watu ndani na nje ya bara la Afrika. Nyimbo hizi zimekuwa zikiwavutia watu kwa sababu mbalimbali kama vile mahadhi yake na matumizi ya lugha ya kisanaa. Baadhi ya nyimbo zimetumia lugha ya picha katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Mbali na kutumia lugha ya kisanaa, nyimbo hizi zimekuwa zikielimisha na kuburudisha kwa namna mbalimbali. Licha ya baadhi ya nyimbo hizi kukiuka misingi ya kimaadili kutokana na kutumia lugha zisizo na staha. Hata hivyo, nyingine zimekuwa zikizingatia maadili yanayofundisha na kujenga jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 4.2**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mkondoni na vinginevyo, sikiliza wimbo wowote wa bongo fleva unaosawiri umuhimu wa wazazi, au kusisitiza kazi au utu wema kisha jibu maswali yafuatayo.

(i) Ni dhamira zipi zinazopatikana katika wimbo huo?

(ii) Ni maadili gani yanayopatikana katika wimbo huo? (toa mifano)

(iii) Una mtazamo gani kuhusu wimbo huo?

(iv) Lugha iliyotumika katika wimbo huo inasawiri vipi suala la maadili?

(v) Wimbo huo una mchango gani katika kuhamasisha maadili ya jamii ya Tanzania?

(b) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na vinginevyo, sikiliza nyimbo mbili za bongo fleva, kisha chambua maadili yaliyomo katika nyimbo hizo.

**Maadili katika mashairi**

Waandishi wengi wamekuwa wakitunga mashairi yenye maudhui mbalimbali yanayoshughulikia masuala ya kijamii. Mashairi yana mchango mkubwa katika kutoa maadili mbalimbali yanayoelimisha na kuburudisha jamii.

**Shughuli ya 4.3**

(a) Chambua maadili yaliyomo katika shairi hili huku ukiongozwa na maswali yanayofuata.

**Shujaa haogopi kitu kilicho halali yake**

*Nisemayo muyashike, hili ni shairi letu,*
*Akuitae muitike, tuendeshe mambo yetu,*
*Shujaa na kitu chake, hadhulumiwi na mtu.*
*Shujaa hahofu kitu, kilicho halali yake.*

*Hodari kwa haki yake, hapendi ipate kutu,*
*Tena hageuki ike, japokuwa mwana kwetu,*
*Japo mtoto mshike, atafanya utukutu,*
*Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake.*

FOR ONLINE READING ONLY

*Hupendezwa kiongoke, cha kwake au cha kwetu,*
*Hupendezwa moyo wake, usitekwe mji wetu,*
*Japokuwa muudhike, yeye haogopi kitu,*
*Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake.*

*Hodari nyumbani kwake, huwakaribisha watu,*
*Hutetea nchi yake, asiichafue mtu,*
*Yu tayari peke yake, kuutembelea mwitu,*
*Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake.*

*Mashairi ya Saadani* (Kandoro, 1972:66)

**Maswali**

(i) Ni dhamira gani zinazopatikana katika shairi hili?

(ii) Kutokana na shairi ulilolisoma, unafikiri ni kwa namna gani maadili yaliyomo yanaakisi jamii yako?

(iii) Ni kwa namna gani jina la shairi linaakisi maadili?

(iv) Unafikiri lugha iliyotumika inasawiri maadili ya jamii? Kwa nini?

(v) Mwandishi anamaanisha nini anaposema "Hodari kwa haki yake, hapendi ipate kutu"?

(vi) Ni kwa namna gani mbinu za kisanaa zinaibua maadili katika shairi hili?

(vii) Una mtazamo gani kuhusu maadili yanayoelezwa katika shairi hili?

(b) Chambua maadili yaliyomo katika mashairi mawili uliyosoma katika diwani teule.

**Maadili katika tamthiliya**

Kutokana na kusoma au kutazama tamthiliya katika runinga, watu wamekuwa wakijifunza mambo mengi yanayotokea au ambayo hayajapata kutokea katika jamii zetu. Haya yote yanatoa mafundisho yenye kuadilisha kutoka katika tamthiliya hizo na kuyaendeleza kwa manufaa ya jamii nzima.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 4.4**

(a) Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Huka:** *(anaanza kulia.)*

**Ngahinyana:** Eeh! Ukweli unauma sasa...

**Mama Huka:** Aaa, Baba Huka, usimfikirie mtoto mambo mabaya.

**Ngahinyana:** Hapana. Huyu mtoto amekwishaanza kuharibika. Mara nyingi, nimeandikiwa barua na babake mdogo kusema Huka hatulii, na wewe hukuamini ukasema wanaanza kumsingizia mtoto wako, mpaka tukagombana na aliyekuwa akitusomea barua zetu. (*Mara hodi inasikika*). Ehee! Sasa utaniona; nitamnyosha barabara. (*Anachukua fimbo yake iliyokuwa ikiegemea ukutani na anakwenda karibu na mlango na anainua fimbo kungojea ishuke mara tu apigaye hodi atakapoingia.*) Karibu. Fungua mlango.

**Mama Huka:** Hapana baba Huka! (*Anamshika lakini anasukumwa*). Si vizuri.

**Ngahinyana:** Sogea huko! (*Mgeni anaingia na fimbo ya mzee inashuka na kutua begani mwake*). Wewe ndiye ...

**Pata:** (*Anaanguka kwa uchungu na barua alizozishika zinatapakaa chini.*) Oehehehch! Mzee vipi? Nimekukosea nini? Ahaa (*Anainuka na kushika bega lake. Ndipo Ngahinyana anapogundua kosa lake. Huka baada ya kuona barua anatoka*).

**Ngahinyana:** Oh! Pole sana mwanangu, sikujua kama ni wewe. Tulikuwa tunamtegemea mpumbavu mmoja. Lakini bahati yake. Pole sana mwanangu! (*Anasaidia kuokota barua*).

**Pata:** Loo! Pameuma. Pole tu haisaidii kitu. Mzee siku nyingine uwe na uhakika au la tutaogopa kukuletea barua zako. Unaonesha kuwa ni mkali sana!

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| Ngahinyana: | (*Huku akicheka*): Ehe ... Ehee ... Wazee wakati mwingine huwa tuna hasira. Kuna barua yetu? Kutoka Dalisalaam? |
| Pata: | Nadhani inatoka Dar es Salaam. (*Anapekuapekua barua hatimaye anaipata*). Hii hapa. Haya mzee nakwenda. |
| Ngahinyana: | Asante sana. Pole sana kwa kukupiga; nisamehe mwanangu. |
| Pata: | Si kitu mzee. (*Anatoka*) Siku nyingine usinivizie nyuma ya mlango. Ningoje tuonane macho kwa macho. (*Anatoka*) |
| Mama Huka: | (*Anacheka*): Hee ... he ... he ... Ooiii! Unaona sasa, nilikuambia mimi. Umempiga mtoto wa watu bure. Atapita kusema kila mahali. |
| Ngahinyana: | Basi na wewe ... (*Anachana barua na kuisoma.*) |
| Mama Huka: | Inatoka kwa shemeji? |
| Ngahinyana: | Ee! *Anashtuka na kutoa macho*). Mh! |
| Mama Huka: | Nini (*Anamsogelea.*) |
| Ngahinyana: | Mh, (*Huku akitikisa kichwa*). Sikiliza. (*Anasoma.*) Kwa kaka mpenzi,<br><br>Natum... ma... ininy... temu wa... zi... makusu...dihasa...<br><br>la...ku...waa... ndi... kiani... kuwa... aa... ri...fuma.. mbo.. fu.. lani... kuhu.. Huka. (*Anaendelea kusoma hivyo akikwamakwama*). Kwanza hakuchaguliwa kuendelea na shule. Pia, Huka, nasikitika, kuwaeleza, kuwa amebomoa nyumba ya watu. Nina maana amewagombanisha Bi. na Bwana Kambanga hata wameachana. (*Anaachia hapo. Anamwelekea Mama Huka*). Unaona jinsi mwanao anavyofanya. Tulikuwa tukisema sasa hivi. (*Anageuka kumwita Huka*). Unaona, alipofika yule |

FOR ONLINE READING ONLY

kijana tu akatoweka. Alifahamu kuwa baba yake mdogo atatuandikia. (*Anaita tena*). Huka...Nikija huko, kweli nitakuchapa. Afadhali uje mwenyewe.

*Huka (Ngahyoma, 1973)*

**Maswali**

(i) Ni dhamira zipi zinazopatikana katika matini hii?

(ii) Ni kwa namna gani matukio katika matini hii yanafumbata maadili?

(iii) Matendo ya wahusika yanasawiri maadili? Kwa nini?

(iv) Ni kwa namna gani lugha iliyotumiwa na wahusika inaakisi maadili? (toa sababu)

(v) Ni matukio gani katika matini hii hayaakisi maadili ya jamii yako?

(b) Chambua maadili yanayopatikana katika tamthiliya mbili teule ulizosoma.

(c) Angalia au sikiliza tamthiliya mbili zinazorushwa katika vituo vya runinga au redio, kisha chambua maadili yanayopatikana katika tamthiliya hizo.

**Shughuli ya 4.5**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, chambua kazi nne za ushairi na nne za tamthiliya, kisha bainisha masuala ya kiimani yaliyomo katika kazi hizo.

## Ulinganisho wa maadili yaliyomo katika kazi za fasihi na imani za jamii

Imani ni hali ya mtu kukubali jambo fulani kuwa ni kweli na anapaswa kuliheshimu. Aghalabu, imani hujielekeza katika masuala ya dini. Miongoni mwa maudhui yanayowasilishwa kwenye kazi za fasihi hutokana na imani iliyomo katika jamii. Hivyo kuna uhusiano mkubwa baina ya maadili na imani. Dhana hizi hujengana na kuathiriana kiasi kwamba wakati mwingine ni vigumu kuvitenganisha. Ieleweke kuwa wakati mwingine kuna imani ambazo huweza kumsukuma au kumwelekeza mtu kufanya matendo yasiyo na maadili. Kutokana na uwasilishwaji wa masuala mbalimbali, ni muhimu kuzingatia imani za jamii husika katika uchambuzi wa maadili yanayojitokeza katika kazi za kifasihi. Ulinganisho wa maadili katika imani unaweza kuangaliwa katika kazi za kifasihi kama vile bongo fleva, mashairi na tamthiliya.

FOR ONLINE READING ONLY

**Ulinganisho wa maadili na imani katika bongo fleva**

Kwa upande wa fasihi, nyimbo nyingi za bongo fleva zimetumika kubeba maadili yanayoendana na imani zilizopo katika jamii ya Watanzania ijapokuwa baadhi ya nyimbo hizo zimekuwa zikikiuka maadili hayo na kusababisha kufungiwa.

**Shughuli ya 4.6**

(a) Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, sikiliza wimbo wa bongo fleva unaosawiri umuhimu wa elimu, kisha jibu maswali yafuatayo:

(i) Ni dhamira zipi zinazopatikana katika wimbo huu?

(ii) Ni maadili gani unayoyapata kutokana na wimbo huu?

(iii) Ni imani zipi zinazodhihirika katika wimbo huu?

(iv) Kuna uhusiano gani kati ya maadili yaliyoelezwa na imani za jamii yako?

(b) Tumia vyanzo vya mtandaoni au vinginevyo kusikiliza wimbo wa bongo fleva, kisha linganisha maadili yaliyomo na imani za jamii.

**Ulinganisho wa maadili na imani katika ushairi**

Ushairi ni utanzu muhimu katika jamii kwani waandishi wengi wamekuwa wakitunga mashairi yenye malengo ya kufunza, kuonya na kuadibu. Ushairi hupata uhai wake kutokana na hali halisi za kijamii, ikiwa ni pamoja na imani na maadili ya jamii husika. Hii inamaanisha kwamba utanzu huu hubeba maadili yanayoendana na imani zilizomo katika jamii.

**Shughuli ya 4.7**

(a) Soma shairi lifuatalo, kisha linganisha maadili yaliyomo na imani za jamii kwa kujibu maswali yanayofuata.

**Mchwa na Kumbikumbi**

*Nchi yetu kichuguu, ndani yake tunaishi,*
*Tumbo letu na miguu, vyote ndani vinaishi,*
*Mawazo yetu kwa Mungu, aliyeweka utashi,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

FOR ONLINE READING ONLY

*Mate silaha ya kwetu, nyenzo yetu kuitunza,*
*Hatuna hata viatu, kutembea kwanzo funza,*
*Kwetu sisi ni matatu, maagizo twajifunza,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

*Kumbikumbi nakutaja, kwa jina lako heshima,*
*Sina sifa kulitaja, hata kwa liyesimama,*
*Ufanyayo si ya tija, kuishi kama mnyama,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

*Muanzapo ota mbawa, nguvu mwajitangazia,*
*Mwatishia na vipawa, Mungu alo wajalia,*
*Mwaondoka kama njiwa, bila hata chungulia,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

*Mwajifunza nyenyekevu, pindi tuko wote hapa,*
*Mwonesha wenu welevu, kumbe ziro tena kapa,*
*Hamna wenu welevu, ninyi kama hilo pipa,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

*Leo ngoja tuyaseme, yenu haya ni maovu,*
*Tusije kuwa na shibe, kumbe ngozi ni makovu,*
*Badilika usisite, usije juta makovu,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

FOR ONLINE READING ONLY

*Tumaini twaliweka, kwenu nafasi maisha,*
*Hatuna hata mkeka, sema utakuja kwisha,*
*Leo kumbe mwasikika, ipo siku mtakwisha,*
*Kwa nini mwatunyanyasa, wakati wote twaishi?*

*Kurunzi (Mbijima 2019: 33 - 34)*

**Maswali**

(i) Ni dhamira zipi za kimaadili zinazopatikana katika shairi hili?

(ii) Ni maadili gani unayoyapata kutokana na shairi hili?

(iii) Ni imani zipi unazozipata kutoka katika shairi hili?

(iv) Kuna uhusiano gani kati ya maadili yaliyoelezwa katika shairi hili na maadili ya jamii yako?

(v) Ni kwa namna gani maudhui ya shairi hili hayaendani na maadili ya jamii yako?

(b) Chagua mashairi mawili kutoka katika diwani mbili teule, kisha husianisha maadili yaliyomo na imani za jamii.

**Ulinganisho wa maadili na imani katika tamthiliya**

Tamthiliya husawiri mambo halisi yanayotokea katika jamii, aghalabu utanzu huu umeweza kuonesha uhusiano uliopo kati ya maadili na imani za jamii husika. Kupitia utanzu huu, wanajamii huweza kujifunza namna ya kuishi na watu wa hali mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya kiimani na kimaadili.

**Shughuli ya 4.8**

(a) Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Megno: Habari za asubuhi Mtendaji

Mtendaji kata: (*Kwa hasira*) hatutoi misaada hapa, ondoka!

Megno: Aliyekwambia nimekuja kuomba msaada ni nani?

Mtendaji kata: Kilichokuleta nini?

Megno: Msidharau watu jamani. Hatukupenda kuwa hivi.

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| Mtendaji kata: | Ondoka! Unaniwekea kiwingu, nina kazi nyingi za kufanya. |
| Megno: | Nimekuja kuchukua fomu, nataka kugombea |
| Mtendaji kata: | Wala usijisumbue kunieleza, ondoka. Wewe ni kilema. Utamwongoza nani? |
| Megno: | Tafadhali mzee sikuja kudhalilishwa utu wangu. |
| Mtendaji kata: | Nimesema hakuna fomu. (*Akisema kwa ukali*) Ondoka nisikuone! |
| Megno: | Nashukuru sana mzee. (Megno anaondoka wakati mtendaji anaendelea kupekua mafaili yake). |

*Changamoto* (Mahenge, 2010: 5 - 6)

**Maswali**

(i) Mhusika Mtendaji ana imani gani kuhusu Megno?

(ii) Ni kwa namna gani maadili ya tamthiliya hii yanahusiana na imani za jamii?

(iii) Jamii inaamini nini kuhusu tukio la kumfukuza Megno?

(iv) Una mtazamo gani juu ya mhusika Megno ukizingatia suala la imani za jamii yako?

(v) Mhusika Megno anaamini nini kuhusu hali yake?

(b) Chambua uhusiano uliopo kati ya maadili na imani katika tamthiliya mbili teule.

## Mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya

Watunzi wa kazi za kifasihi husawiri mitazamo mbalimbali waliyonayo au iliyomo katika jamii. Hivyo, utunzi wa kazi zao huzingatia mitazamo hiyo na hukusudia kuishirikisha jamii. Mitazamo hiyo imeweza kujidhihirisha katika baadhi ya kazi za kifasihi kama vile nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya.

### Mitazamo iliyomo katika bongo fleva

Bongo fleva ni utanzu pendwa zaidi kwa watoto, vijalunga na watu wazima. Huu ni miongoni mwa tanzu zinazosambaa kwa haraka zaidi ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi simulizi. Kutokana na hali hii, ni wazi kwamba mitazamo

FOR ONLINE READING ONLY

inayojitokeza katika nyimbo za bongo fleva husambaa haraka katika jamii kupitia majukwaa mbalimbali, yakiwamo yale ya mitandao ya kijamii. Ijapokuwa mingi ya mitazamo hiyo ni chanya, bado kuna baadhi ya nyimbo zenye mitazamo hasi inayosababisha zifungiwe na mamlaka husika.

**Shughuli ya 4.9**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na vinginevyo, sikiliza wimbo wa bongo fleva wa msanii yeyote unaosawiri athari za starehe, kisha jibu maswali yafuatayo:

**Maswali**

(i) Wimbo huo una dhamira zipi?

(ii) Mtunzi ana mtazamo gani kuhusu starehe?

(iii) Jamii yako ina mitazamo gani kuhusiana na starehe zinazofanywa katika jamii?

(iv) Mitazamo ya mtunzi wa wimbo huo inahusianaje na ile ya jamii yako? Fafanua

(v) Una mtazamo gani kuhusu wimbo huo?

(b) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni au vinginevyo, sikiliza nyimbo mbili za bongo fleva, kisha chambua mitazamo inayopatikana katika nyimbo hizo.

**Mitazamo iliyomo katika mashairi**

Watunzi wa mashairi ya Kiswahili wameibua mitazamo mbalimbali kupitia kazi zao. Baadhi ya mitazamo hiyo inasawiri maisha halisi, na inawataka wanajamii kubadilika ili kuwa na jamii yenye ustawi na uwajibikaji. Kupitia utanzu huu, wanajamii hujifunza kuhusiana na mitazamo iliyomo katika jamii.

**Shughuli ya 4.10**

(a) Ghani au soma shairi lifuatalo, kisha chambua mitazamo iliyomo.

**Natamka Tanzania**

*Nimejaliwa mabonde natamka Tanzania,*
*Kama Rufiji upande, wa Mashariki sikia,*
*Mazao mengi ja kunde, kumbe mngejilimia,*
*Lakini Watanzania, bado masikini mno.*

FOR ONLINE READING ONLY

*Nimepewa na ardhi, natamka Tanzania,*
*Mola kwenu ameridhi, muweze kuitumia,*
*Wanafaidi baadhi, wengine wagugumia,*
*Lakini Watanzania, wengi wenu ni wavivu.*

*Nimejaliwa asali, natamka Tanzania,*
*Afrika ni ya pili, kwa ubora mizania,*
*Hamfaidi kwa hili, nashangaa mnalia!*
*Lakini Watanzania, mnasikitisha mno.*

*Nimepewa na madini, natamka Tanzania,*
*Almasi na urani, dhahabu imetulia,*
*"Tanzanaiti" kundini, kwa faida yenu pia,*
*Lakini Watanzania, mmelala usingizi.*

*Nimejaliwa matunda, natamka Tanzania,*
*Mngeitafta tenda, kulisha Dunia,*
*Lakini mengi yavunda, huku mwayaangalia,*
*Lakini Watanzania kwa nini hamzinduki?*

*Nimejaliwa maji, natamka Tanzania,*
*Si ya kupikia uji, bali ya kumwagilia,*
*Maziwa, mito, "ulaji" kanitunuku Jalia,*
*Lakini Watanzania, bado mnalia njaa!*

*Nimepewa vivutio, natamka Tanzania,*
*Mbuga, Bahari patio, watu waifurahia,*
*Mngefanya kimbilio, leo mngeshangilia,*
*Lakini Watanzania, mwanikatisha tamaa.*

FOR ONLINE READING ONLY

*Nimejaliwa misitu natamka Tanzania,*
*Mngepata vingi vitu, siyo kama natania,*
*Lakini hamthubutu, wanyonge nasimulia,*
*Lakini Watanzania, mbona hamuendelei?*

*Kwa kweli nimemaizi, mama yenu Tanzania,*
*Pamoja na mali hizi, nyuma mnajirudia,*
*Wakiotesha mizizi, "weupe" mtajutia,*
*Lakini Watanzania, aliyewaroga nani?*

*Sibanduki* (Hancha, 2015:16 - 17)

(b) Kwa kutumia mashairi mawili kutoka katika diwani teule, chambua mitazamo inayopatikana katika mashairi hayo.

**Mitazamo iliyomo katika tamthiliya**

Katika kusawiri mambo halisi ya kijamii, tamthiliya, kama tanzu nyingine za fasihi andishi, hudhihirisha mitazamo mbalimbali iliyomo katika jamii. Mitazamo hiyo huwa na athari chanya au hasi katika jamii husika. Mitazamo chanya ikisawiriwa vyema katika tamthiliya, hadhira hujifunza na kupata maarifa mapya yanayowasaidia katika harakati zao za kuboresha maisha. Kinyume chake, mitazamo hasi hurudisha nyuma maendeleo ya kijamii.

**Shughuli ya 4.11**

(a) Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Cheja: (*kwa hamaki*) Juma! Huwezi kwenda namna hii hata kidogo. Huwezi kunikana na hali ulisema unanipenda. Nilikueleza siku ile hatari yake hukutaka kunisikia. Ukajisingizia mapenzi. Sasa leo unataka kunikana hivi. Hata kidogo!

Juma: Hata kikubwa. Usinishikilie hivyo. Tena nakueleza wazi usije ukalogwa kumwambia mtu kuwa mzigo huo ni wangu. Walahi utajuta.

Cheja: Utafanya nini?

FOR ONLINE READING ONLY

**Juma:** (*Anacheka*). Eti "utanifanya nini" kwanza utaniona wapi? Kwanza nani shahidi?

**Cheja:** (*kwa uchungu*). Yaani kweli, Juma imekuwa si kitu kwako litakalonipata baadaye. Hunifikirii nitamfanyaje mtoto. (*Anashindwa kusema kwa muda.*) Kumbe yote yalikuwa ulaghai mtupu. Siamini! Siamini!

**Juma:** Amini! Amini tu! Wewe sikiliza. Jiendee zako kwa wazazi wako ukajitunze kama unaogopa kuendelea kukaa kwa mwajiri wako. Nenda tu.

**Cheja:** Sikuweza kuvumilia kukaa tena nyumbani kwao. (*Anatazama chini.*) Hapana sikuweza.

**Bw. Chowe:** Kwa nini?

**Cheja:** (*Kwa kusita hali akiwa bado anatazama chini.*) Bwana Se … Bwana Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi ni mjamzito…

**Cheja:** Bwana Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi ni mjamzito. (*Wote wanapigwa bumbuazi*).

**Bw. Chowe:** Eti nini? (*Cheja anaanza kulia*).

**Bi. Chowe:** Uuuuuui, Uuuuuuuuuui Mungu wangu! (*kwa wanawake wenzie*) Jamani nieleezeni labda sikusikia vizuri. Uuuuuuuuuuuui! (*Anamkimbilia Cheja*). Cheja mwanangu Uuuuuuuuuui!

**Bw. Chowe:** (*kwa Bi. Chowe*) Aaa! Acha kelele wewe. Sema vizuri Cheja sema acha kulia! Ati kweli au unatania?

**Cheja:** Kweli baba.

**Bi. Chowe:** Uuuuuuuui! Uuuuuuuuui! (*Anakwenda kwa wanawake wenziwe*). Uuuuuui!

*Hatia* (Muhando, 1974: 9-15).

FOR ONLINE READING ONLY

**Maswali**

(i) Ni maudhui gani unayapata kupitia mazungumzo ya wahusika wa matini hii?

(ii) Wahusika wana mitazamo gani katika matini hii?

(iii) Unapata mtazamo gani kuhusiana na Cheja anaposema "Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi ni mjamzito"

(iv) Una maoni gani kuhusiana na matendo ya wahusika Cheja na Juma? Je, yanapaswa kuigwa katika jamii? Kwa nini?

(v) Mitazamo gani inajengwa na matukio ya mhusika Juma?

(vi) Mbali na mitazamo iliyomo katika tamthiliya hii, una mitazamo gani mingine kuhusiana na matini hii?

(vii) Unafikiri kuna uhusiano wowote kati ya mitazamo ya wahusika wa tamthiliya hii na matendo ya jamii?

(b) Chambua mitazamo inayopatikana katika tamthiliya mbili teule ulizosoma.

## Uhusiano wa mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya na matendo ya jamii

Kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi za kifasihi na matendo ya jamii kwani watunzi hutunga kutokana na matendo yanayofanywa na wanajamii. Uhusiano wa mitazamo na imani ya jamii unaweza kuonekana katika baadhi ya kazi za kifashi kama vile nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya.

### Uhusiano wa mitazamo iliyomo katika nyimbo za bongo fleva na matendo ya jamii

Nyimbo za bongo fleva zimeonesha mitazamo mbalimbali inayosawiri matendo ya jamii. Kwa kupitia usawiri wa matendo hayo wasanii wamekuwa wakitoa mafunzo na maadili kwa jamii katika maeneo mbalimbali ya maisha. Wakati matendo hasi yana athari mbaya kimaisha, matendo chanya yanaposawiriwa vyema, wanajamii hupata maarifa yanayowasaidia kuleta mabadiliko chanya, hivyo kuchangia kwenye ustawi na maendeleo ya jamii.

**Shughuli ya 4.12**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mkondoni au vinginevyo, sikiliza wimbo wowote wa bongo fleva ulioimbwa na mtoto chini ya miaka kumi na minane (18), kisha jibu maswali yafuatayo:



FOR ONLINE READING ONLY

(i) Unapata mitazamo gani unaposikiliza wimbo huo?

(ii) Ni matendo gani katika jamii yanaakisi mtazamo alionao mtunzi wa wimbo huo?

(iii) Je, mitazamo ya wimbo huo inaathiri vipi jamii yako?

(iv) Ni mitazamo gani katika wimbo huo unafikiri haisawiri matendo yaliyomo katika jamii?

(v) Kuna funzo lolote unalipata kutokana na mitazamo inayoibuliwa na mtunzi wa wimbo huo? Kwa nini?

(b) Tumia vifaa vya TEHAMA, sikiliza nyimbo za bongo fleva zisizopungua mbili (2), kisha husianisha mitazamo iliyomo kwenye nyimbo hizo na matendo ya jamii.

**Uhusiano wa mitazamo iliyomo katika mashairi na matendo ya jamii**

Mashairi mengi husawiri matendo ya jamii ambayo kwayo mafunzo na maadili hujitokeza. Watunzi wengi wanaposana kazi zao hulenga jamii ibadilike kimatendo ili kuleta mabadiliko, mafanikio na ufanisi unaohitajika. Endapo jamii itazingatia matendo mazuri na kuondokana na hali ya mazoea mabaya, itachangia katika ustawi wa mtu binafsi na jamii kwa jumla.

**Shughuli ya 4.13**

(a) Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Edita usinihini, naomba kusema haya
Yanishangaza machoni, kuyaficha jambo baya
*Hadi naona huzuni, amefanya kwa kinaya*
*Mtesi mtu mbaya, hatari kuwa kundini*

*Hatari kuwa kundini, mtesi mtu mbaya*
*Muongo hawezekani, sifa yake ni ubaya*
*Hata akiwa jirani, kamata huu wasiya*
*Mtesi mtu mbaya, hatari kuwa kundini*

FOR ONLINE READING ONLY

*Jamani muogopeni, huyu si wa kutaniya*
*Usifanye ya utani, atakutia pabaya*
*Kidhabu toka zamani, hana kheri nakwambiya*
*Mtesi mtu mbaya, hatari kuwa kundini*

*Ujiondowe kundini, makazi yako hawiya*
*Humo hutoonekani, pokea yako hidaya*
*Kama ukifanywa kuni, hiyari yake Jaliya*
*Mtesi mtu mbaya, hatari kuwa kundini*

*Umejitia shimoni, sasa unapayapaya*
*Kazi hiyo kwa yakini, umetafuta javiya*
*Japo upo walakini, jiepushe na hatiya*
*Mtesi mtu mbaya, hatari kuwa kundini*

*Adili za Nyembe 1: Tungo za Ustadh Mohamed Ally Nyembe (Akhery)* (Ndossa na Wenzake, 2019:5)

**Maswali**

(i) Mshairi anaibua mitazamo gani katika shairi hili?

(ii) Je, mitazamo iliyotolewa katika shairi hili inahusiana vipi na matendo ya jamii?

(iii) Je, shairi lina mtazamo gani kuhusu madhara ya utesi?

(iv) Je mstari unaosema "Kama ukifanywa kuni hiyari yake Jaliya" unawakilisha mtazamo gani?

(v) Je, mitazamo ipi katika shairi hili haiendani na matendo yaliyomo katika jamii? Kwa nini?

FOR ONLINE READING ONLY

(b) Chambua mitazamo iliyomo kwenye mashairi mawili katika diwani teule, kisha eleza namna inavyohusiana na matendo ya jamii.

**Uhusiano wa mitazamo iliyomo katika tamthiliya na matendo ya jamii**

Kama ilivyo kwa bongo fleva na mashairi, tamthiliya husawiri mitazamo na matendo ya wanajamii kama njia ya kujenga maudhui. Malengo ya maudhui hayo ni kuleta mabadiliko katika jamii kwa kuonesha matendo na mitazamo chanya kupitia wahusika wake. Hivyo, mazungumzo huwa ni malighafi ya msanii katika kusana kazi yake.

**Shughuli ya 4.14**

(a) Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Bi Somoe: Mata mwanangu, sisi wazazi wako ni masikini. Lakini hata siku moja hujasikia tumeiba mali ya ntu. Tusameheni wanetu kwa kushindwa kuwasomesha. Ni sababu ya umasikini wetu. Ingawa unajua kusoma mawili matatu. Lakini huko njini uendako kama kuna uwezakano wa kujiendeleza fanya hivyo. Kwani elimu haina mwisho.

Mata: Sawa mama.

Bi Somoe: Kila siku tunasikia kwenye maredio. Urithi wa ntoto ni elimu. Zamani tuliona heri watoto wetu tuwatumikishe tu kwenye mashamba ya mikorosho. Tulijua kuwa tungepata faida kubwa. Kumbe ulikuwa ni ujinga. Ungekuwa na elimu wala usingekwenda njini kwa mashaka. Ungekwenda njini kwa kazi yako.

Che Munndu: Mama Mata unaongea nini? Wangapi wana elimu na wanaishi kwa mashaka?

Bi Somoe: Kwani kuoa ni ujanja? Au kuoa wake wengi kila kukicha na kuwa na watoto wengi kama bata ndo ujanja?

Che Munndu: Sasa hiyo unaona ni ujinga? Ndo maana kila mwananke ninayemwoa nampa talaka sababu ya ulozi wako.

Bi Somoe: Nlozi we mwenyewe. Unaoa kila ukipata hela za korosho. Wanawake wanajua una pesa. Pesa zikikuishia wanakukimbia. Mbona mi uliyenioa na umaskini sikukimbii?

FOR ONLINE READING ONLY

**Che Munndu:** Wasomeshe basi hao watoto wako. Nani anataka hasara? Unapeleka watoto shule siku mbili wamepata mimba.

**Bi Somoe:** Lakini si nyie wenyewe ndo mwawapa mimba? We mwenyewe mbona mwaka juzi ulioa binti ndogo wa shule. Lakini sharia zipo, iko siku zitachukua nkondo wake.

**Che Munndu:** Sheria sheria ndo kitu gani? Wangapi hapa kijijini wamewapa watoto wa shule mimba. Na hatuoni kufungwa? Si mnawafundisha watoto wenu wenyewe (*huku akibana pua*) 'bwana aliyenipa mimba sinjui'. Sasa hiyo akili kweli? Hela yangu si afadhali nkaoe nke mwingine. Kuliko kupeleka ntoto shule anayeishia kupata mimba na kuniongezea nzigo?

*Safari ya Chinga* (Omari, 2012: 18 – 20)

**Maswali**

(i) Mwandishi anabainisha mitazamo gani katika kipande hiki cha tamthiliya?

(ii) Una maoni gani kuhusu mitazamo iliyomo katika kipande hiki cha tamthiliya? (Toa sababu)

(iii) Unafikiri mtazamo wa mhusika Bi. Somoe una uhalisi katika jamii? Kwa nini?

(iv) Je, unadhani mtazamo wa Che Mundu wa kujitenga na jukumu la kumuelimisha mtoto unasawiri matendo ya jamii yako?

(v) Ni kwa namna gani mitazamo ya mhusika Che Mundu inaathiri matendo ya jamii?

(vi) Je, jamii yako ina mitazamo gani kuhusu mimba za utotoni?

(vii) Unafikiri kuna uhusiano wowote kati ya mitazamo ya wahusika wa tamthiliya hii na matendo ya jamii? Toa sababu.

(b) Kwa kutumia tamthiliya mbili teule ulizosoma, husianisha mitazamo iliyomo katika tamthiliya hizo na matendo ya jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

**Athari za kiimani na kimtazamo katika bongo fleva zinavyojidhihirisha katika jamii**

Kuna athari nyingi za kiimani na za kimtazamo zinazotokana na maudhui ya nyimbo za bongo fleva. Kwa kuwa utanzu huu hutumia zaidi redio, runinga na mitandao ya kijamii, inakuwa rahisi kwa athari za imani na mitazamo hiyo kuifikia hadhira kwa haraka. Athari hizo huweza kujenga ama kubomoa jamii zisipopokelewa kwa tahadhari na uchambuzi faafu.

**Shughuli ya 4.15**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mkondoni na vinginevyo, sikiliza wimbo wa msanii yeyote wa kike unaohamasisha mapambano ya maisha, kisha jibu maswali yafuatayo:

(i) Ni mitazamo na imani ipi inapatikana katika wimbo huo?

(ii) Wimbo huo unatoa taswira gani kuhusiana na changamoto za kiuchumi na maisha ya kila siku katika jamii?

(iii) Wimbo huo una athari zipi za kiimani na kimtazamo katika jamii?

(iv) Wimbo huo una athari zipi za kiimani na kimtazamo kwa vijana?

(v) Ni mitazamo ipi iliyomo katika wimbo huo haiendani na jamii? Kwa nini?

(vi) Ni mafunzo gani jamii inaweza kuyapata kutokana na wimbo huo?

(vii) Una mtazamo gani kuhusu wimbo huo ukilinganisha na maisha ya kila siku?

(b) Jadili namna athari za kiimani na mitazamo katika nyimbo mbili za bongo fleva (kongwe na za sasa) zinavyojitokeza katika jamii.

**Athari za kiimani na kimtazamo katika mashairi zinavyojitokeza katika jamii**

Fasihi andishi, ukiwamo utanzu wa ushairi, husawiri imani na mitazamo ya jamii katika kutoa maudhui. Maudhui hayo huchagiza ufanisi na mabadiliko yanayohitajika. Kwa njia hii, mashairi huibua mitazamo na imani ambazo huweza kuchangia ustawi wa jamii husika.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 4.16**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mkondoni au vinginevyo, sikiliza wimbo wowote wa bongo fleva kisha jibu maswali yafuatayo:

(i) Chambua dhamira za wimbo huo.

(ii) Je, ni athari zipi za kiimani na kimtazamo zinazopatikana katika wimbo huo?

(iii) Ni mitazamo gani inasawiriwa katika wimbo huo na ina athari zipi katika jamii?

(iv) Ni mitazamo ipi katika wimbo huo inasawiri au haisawiri jamii yako?

(v) Una mtazamo upi wa jumla kuhusu wimbo huo?

(b) Chambua athari za kiimani na kimitazamo zilizomo katika mashairi mawili ya diwani teule, kisha thibitisha namna zinavyojitokeza katika jamii.

**Athari za kiimani na kimtazamo katika tamthiliya zinavyojitokeza kwenye jamii**

Maudhui ya tamthiliya huwa na athari za kiimani na za kimtazamo ambazo hujitokeza kwenye jamii husika. Maudhui hayo husambaa kupitia runinga, redio, na mitandao ya kijamii. Njia hizi zinarahisisha kusambaa kwa athari hizo na kuifikia hadhira kwa haraka.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 4.17**

(a) Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Avita: Nina wengine, siyo mwingine. Kwa uzuri huu wanaonitaka ni wengi, lazima nibadili ladha.

Vera: Hayo ndiyo maneno, unanipa raha *best*. Hahahaaaa!

Avita: Tena siku hizi nina yule aliyekuwa wako ukamwacha ulipokwenda chuo. Vipi na wewe huko chuoni umeshaopoa madaktari wangapi?

Vera: Siyo madaktari tu, na maprofesa.

Avita: Maprofesa? Sikuwezi. Unawapataje na madigrii yao vichwani?

Vera: Uzuri best, uzuri, chema chajiuza.

**Avita:** Usiniambie!

**Vera:** Ndo nakwambia sasa. Isitoshe, wasomi wengi wana migogoro isiyo na suluhu ya ndoa. Wake zao wasomi wana mambo hamsini kidogo. Mara wanaandika *paper*, mara vikao, mara *appointment* za mheshimiwa. Kwa kupenda au kutokupenda, kujua au kutokujua, wanajikuta wanawaacha wanaume zao wakiwa na njaa, hapo ndo wanatuachia njia nyeupeee. Kufa kufaana.

**Avita:** [*Anaangua kicheko cha nguvu*]. Yaani wewe umepinda, hapo ndo nakupendea mtu wangu.

**Beti:** Yaani mnavunja ndoa za watu halafu mnapongezana? Mh! *Wonders will never end*

[*Anapiga makofi na kubetua mdomo kuonesha mshangao*]

**Vera:** *Point of correction*, hatuvunji, kimsingi tunawasaidia kuondoa stress zao.

Wakiingia kwenye mihadhara wapoleee. Fikiria wangekuja na stress kwenye kumbi za mihadhara, si ingekuwa kimbembe. Yaani, watu kama sisi ni wa muhimu kwa maendeleo ya taifa.

**Beti:** Nawahurumia, hamjui mlifanyalo, halafu mnaongea kwa sauti na kujiamini. Akina mama wakitokea hapa, hamwogopi?

*Halahala* (Mbijima, 2019: 52 - 53)

**Maswali**

(i) Imani na mitazamo gani inajitokeza katika matini hii?

(ii) Mitazamo ya mwandishi kuhusu mwanamke ina athari gani katika jamii?

(iii) "*Nina wengine, siyo mwingine. Kwa uzuri huu wanaonitaka ni wengi, lazima nibadili ladha.*" Kauli hii inaweza kuleta athari gani kwa vijana?

(iv) Unafikiri mitazamo iliyomo katika matini hii ina uhalisi wowote katika jamii? Kwa nini?

FOR ONLINE READING ONLY

(v) Ni kwa namna gani matendo ya wahusika Vera na Avita yanasawiri matendo yanayofanywa na watu katika jamii?

(vi) Kiimani na kimtazamo mhusika Beti anawakilisha kundi lipi la vijana katika jamii?

(vii) Una mtazamo gani wa jumla kuhusu matini hii?

(b) Jadili athari za kiimani na kimitazamo zilizomo katika tamthiliya mbili teule, zinavyojitokeza katika jamii.

**Tamrini**

1. Jadili namna athari za mitazamo ya wahusika wawili katika tamthiliya teule mbili ulizosoma zinavyojitokeza katika jamii.
2. Jadili uhusiano uliopo baina ya mitazamo iliyomo katika nyimbo mbili za bongo fleva na matendo ya jamii.
3. Linganisha masuala ya mitazamo ya kijamii kama yanavyosawiriwa katika tamthiliya mbili teule.
4. Jadili kauli kwamba "Nyimbo za bongo fleva hazina maadili kwa jamii".
5. Chambua maadili na mitazamo inayojitokeza katika mashairi mawili ya diwani teule.
6. Tumia nyimbo mbili za bongo fleva kulinganisha mitazamo iliyomo katika nyimbo hizo na imani za jamii.
7. Huku ukilinganisha na imani za jamii, jadili maadili yanayopatikana katika tamthiliya mbili teule.
8. Maadili na imani za jamii zinachangia katika utunzi wa kazi za fasihi hususani nyimbo na tamthiliya. Jadili kauli hii kwa kutumia mashairi mawili (2) kutoka katika diwani teule.
9. Sikiliza nyimbo mbili za bongo fleva uzipendazo, kisha chambua maadili yaliyomo katika nyimbo hizo.
10. Athari za kiimani na kimtazamo huweza kuimarisha au kudumaza kazi za kifasihi. Jadili kauli hii kwa mifano kuntu.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tano

# Ujumi katika kazi za fasihi

## Utangulizi

*Ujumi ni dhana inayotumika duniani kote japo wananadharia na wanajamii hutofautiana kimtazamo kuhusu dhana hii. Mijadala kuhusu ujumi hujitokeza katika nyanja tofauti, miongoni mwa nyanja hizo ni fasihi andishi na simulizi. Katika sura hii, utajifunza kueleza na kuchambua mbinu za kiujumi katika kazi za fasihi za majigambo, mashairi na tamthiliya teule. Aidha, utajifunza jinsi mbinu za kifasihi zinavyoathiri kupatikana kwa maana katika kazi hizo. Kadhalika, utajifunza namna ya kutumia fasihi katika kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi. Umahiri utaoujenga utakuwezesha kutambua na kueleza ujumi katika miktadha mbalimbali.*

*Namna uchambuzi wa ujumi unavyoboresha utunzi wa kazi za fasihi*

**Shughuli ya 5.1**

Kusanya nyimbo tano (5) za bongo fleva ambazo, kwa maoni yako, ni nzuri na nyimbo tano (5) ambazo, kwa maoni yako, ni mbaya; kisha, kwa kila wimbo eleza kwa nini unaona ni mzuri au mbaya.

## Ujenzi wa ujumi katika kazi za fasihi

Dhana ya ujumi imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa mfano Zirimu na Gurr (1971), Nyirenda na Ishumi (2002), Ponera (2014), na Habwe na Zaja (2019) ambao wanaeleza kuwa ujumi ni hisia za akilini au ni misingi ya kifalsafa kuhusu uzuri wa sanaa. Wanaongeza kuwa ujumi sharti uendane na jamii mahsusi kwa lengo mahsusi la kazi ya kisanaa inayobuniwa. Nyirenda na Ishumi (2002) wote

FOR ONLINE READING ONLY

wanakubaliana kwamba ujumi ni utambuzi wa uzuri au ubaya katika maumbile asilia, vitu aundavyo mtu na sanaa. Tajiriba za kiujumi zinazoibuliwa katika akili au hisia za mtu hujumuisha kuajabia au kufurahisha au kupendezewa au kuvutiwa kwa uzuri wake. Kipimo cha uzuri wa kitu hujengeka katika utambuzi (kiakili na kihisia) wa mtu katika makuzi au malezi yake. Kipimo hiki hakihusu uzuri tu bali pia ubaya wa kitu; na ubaya huu hujumuisha upungufu katika umbile au sanaa.

Kama ilivyo kwa jambo au kitu chochote, kazi ya fasihi pia huweza kuonwa kama nzuri au mbaya. Watunzi huhakikisha kuwa kazi zao zinakuwa na thamani ya kiujumi, yaani hadhi na mvuto kwa hadhira. Watunzi hao huujenga ujumi kwa kutumia mbinu mbalimbali za kibunifu. Mifano ya mbinu hizo ni: taharuki, ufutuhi, utanzia, utomeleaji, ujenzi wa wahusika, usawiri wa mandhari pamoja na uteuzi na mpangilio mzuri wa maneno. Matumizi ya mbinu hizi huifanya kazi ivutie na iwe na upekee. Mbinu nyingine ya kujenga ujumi katika kazi ya fasihi ni kuzingatia vipengele vya kijadi. Watunzi hutumia ujadi katika vipengele kama vile majina au mandhari yanayojulikana na hadhira. Ujadi vilevile hutokana na uzoefu na tajriba ya hadhira. Mathalani, uzuri wa hadithi au ngano zenye mhusika sungura unatokana na kukidhiwa kwa matarajio ya hadhira kwamba lazima mhusika huyu atafanya ujanja fulani. Ikiwa mhusika huyu atatumika vinginevyo, hadhira inaweza isiuone uzuri wa hadithi au ngano uliozoeleka kijadi kuhusu ujanja wa sungura. Kufanya hivi kunaifanya hadhira ijione iko karibu sana na kazi. Mbinu nyingine ni kuzingatia uhalisi. Mtunzi anapotunga kazi inayoakisi mambo ya kweli yanayotokea katika jamii ya hadhira yake huifanya kazi iwe na thamani kwa hadhira hiyo. Zaidi, kazi hutakiwa kuzingatia maadili ya hadhira inayolengwa. Kazi inayoheshimu miiko au inayoepuka mambo yanayokatazwa na jamii huwa na thamani zaidi kwa hadhira kuliko inayokiuka maadili.

Mbinu nyingine inayoweza kutumika ni ile ya mtazamo wa Kiafrika kuhusu ujumi. Katika kulishughulikia suala la ujumi wa Kiafrika, Wafula na Njogu (2007) wamebainisha misingi kadhaa ya ujumi huo. Baadhi ya misingi hiyo ni:

(i) Fasihi ya Kiafrika isifu Uafrika na kutilia mkazo utamaduni wa Kiafrika na usawa wa watu wote.

(ii) Mashujaa wa Kiafrika na ushujaa wao vioneshwe katika kazi za kisanaa na fasihi ya Kiafrika kwa jumla.

(iii) Lugha za Kiafrika zitumike katika uandishi wa fasihi ya Kiafrika.

(iv) Mbinu za utunzi zifungamane na mazingira ya Kiafrika. Mbinu hizo zihusishe matumizi ya vitu kama vile matumizi ya mibuyu, mikuyu,

FOR ONLINE READING ONLY

masimulizi, mavazi, vyakula, maudhui ya Kiafrika, pamoja na mienendo mbalimbali ya Kiafrika.

## Uchambuzi wa mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika kazi za fasihi

Mbinu zinazotumika katika kujenga ujumi huweza kuchambuliwa katika kazi za kifasihi kama vile mashairi, tamthiliya na majigambo. Mbinu hizi za kifasihi huipa kazi husika ujumi ambao humfanya msomaji au mtazamaji kuvutiwa au kutokuvutiwa nao. Mbinu hizo hujitokeza katika kazi za kifasihi kama inavyodhihirika katika shughuli zifuatazo:

### Mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika mashairi

**Shughuli ya 5.2**

(a) Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata:

**Kiswahili**

*Titi la mama li tamu, hata likiwa la mbwa,*
*Kiswahili naazimu, sifayo inayofumbwa,*
*Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,*
*Toka kama chemchemu, furika palipozibwa,*
*Titi la mama li tamu, jingine halishi hamu.*

*Lugha kama Kiarabu, Kirumi na Kiingereza,*
*Kwa wingi zimeratibu, mambo ya kupendeza,*
*Na mimi nimejaribu, kila hali kujifunza,*
*Lakini sawa na bubu, nikizisema nabezwa,*
*Titi la mama li tamu, jingine halishi hamu.*

FOR ONLINE READING ONLY

*Kila mtu lugha yake, ndiye mtumishi mwema,*
*Lugha nyingine makeke, mviringo kuzisema,*
*Kila mkuu na pake, hana hadhi akihama,*
*Kiswahili nivike, joho lako la heshima,*
*Titi la mama li tamu, jingine halishi hamu.*

*Lugha yangu ya utoto, hata leo nimekua,*
*Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,*
*Sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,*
*Pori, bahari na mto, napita nikitumia,*
*Titi la mama li tamu, jingine halishi hamu.*

*Kiswahili kikikopa, lugha nyingine pia,*
*Ambazo zimenenepa, jambo hili hutumia,*
*Au sivyo zingetupwa, kwa kukosa manufaa,*
*Kiswahili kikikopa, si ila ndiyo tabia,*
*Titi la mama li tamu, jingine halishi hamu.*

*Pambo la Lugha* (Robert, 1973:27-29)

FOR ONLINE READING ONLY

**Maswali**

(i) Unafikiri kwa nini mwandishi amefananisha Kiswahili na titi la mama?

(ii) Ni mbinu zipi za kiujumi zilizotumika katika shairi hili?

(iii) Ni kipengele kipi cha ujumi wa kijadi kinachojitokeza katika shairi hili?

(iv) Katika ubeti wa pili, mwandishi anakusudia nini anapotaja lugha za Kiarabu, Kirumi na Kiingereza?

(v) Ni dhana zipi zinazodhihirisha uzuri na ubaya wa shairi hili?

(b) Chambua mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika shairi lifuatalo.

**Ukurasa wa Mwisho**

*Nimesoma visa vya mazonge ya vituko, mazinge ya njia;*
*Visa vya ndoto zenye matundu, macho mia yanayougua;*
*Visa vya pesa kuzidi kujaa kwenye mifuko is'ojaa;*
*Na ukata kustakimu ubavuni pa ukwasi dawamu;*
*Nimevisoma na kusaili;*
*Ukurasa wa mwisho haupo?*

*Nimesoma visa vya wakata misitu ya majoka yatishayo;*
*Visa vya mazimwi yalayo watu, na vifisi na vibweha vyayo;*
*Visa vya kina Masalakulangwa - adui wa mazimwi hayo;*
*Visa vya wajenzi nyumba mpya, na walimaji mashamba mapya;*
*Nimevisoma na kung'amua:*
*Ukurasa wa mwisho haupo.*

*Nimesoma ngano isiyokuwa na mwisho - ya maendeleo*
*Ya mnyonge katika mazonge ya mawimbi ya bahari leo;*
*Ngano ngumu ya sanaa ya harakati iwashayo mifuo*
*Ya jasho na nyundo na risasi, - tabaka kuasi kwa visasi*
*Nimesoma, na sasa nakiri:*
*Ukurasa wa mwisho haupo.*

*Nimezisoma pia ngano za kale zisizosahaulika*
*Za matamanio yasiyokauka, na ari is'ovunjika;*
*Nimesoma jinsi ya kufumbua ishara zilizofumbika;*
*Nazidi kufunua kurasa, nazidi kufasiri mikasa:*
*Nimesoma, na sasa nasema:*
*Ukurasa wa mwisho haupo.*

*Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Kahigi na Mulokozi, 1979:118-119)

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Chambua mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika mashairi mawili ya diwani teule ulizozisoma.

**Mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika majigambo**

**Shughuli ya 5.3**

(a) Tamba au soma jigambo lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Jabali**

Mimi ni jabali

Naangamiza kama umeme unavyopasua anga

Wenye shari wote huniogopa

Mafedhuli na mahayawani hufichama wakiniona

Kila dhalimu hunigwaya na kunikimbia

Mimi ni kama jahazi linalopambana na mawimbi baharini

Gharika ikishavuma hurudi kuwa wima

Yote yenye mawaa hukimbia kutokomea

Wengi kushangaa jabali kuwayumbisha

Madhalimu wote udhalimu hukoma

Matendo mema hutenda kuisalimisha dunia

Mimi ni jabali

kamwe sitetereki kwa lolote.

**Maswali**

(i) Ni kwa namna gani taswira zimetumika kujenga ujumi katika jigambo hili?

(ii) Mbinu ya taharuki imetumikaje kujenga ujumi katika jigambo hili?

(iii) Ni vifungu vipi vya maneno katika jigambo hili vinaakisi mbinu ya uteuzi na mpangilio wa maneno?

(iv) Ni mbinu zipi nyingine zilizotumika kujenga ujumi katika jigambo hili?

FOR ONLINE READING ONLY

(b) Kwa kutumia maktaba au kifaa chochote cha kidijiti, pakua kazi yoyote ya majigambo, kisha chambua mbinu ambazo mtunzi amezitumia kujenga ujumi katika kazi hiyo.

**Mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika tamthiliya**

**Shughuli ya 5.4**

(a) Soma matini ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Miguu ya Bi. Kirembwe: Na mimi pia nilichukuwa kwenye miendo yako ya kichawi ya kuhusudu na kuangamiza…

Bi. Kirembwe: Na miguu pia? (Anaishika miguu) Nisaidieni! (Anaiendea hadhira, lakini zile sauti za nje zinajongea karibu)

Sauti Nyingi: (Kutoka nje ambako zinajongea ndani) Sisi ni vizazi vipya vya Gininigi,

Vizazi vya walioangamia …

Vizazi vya waliodidimia …

Sisi sasa tuna kinywa kipana …

Tuna uwezo wa kuamua tunavyotaka,

Kuamua wenyewe … kwa maslahi ya sote …

Hatutachagizwa tena na uchawi,

Tunakuja … tunakuja …

Bi. Kirembwe: Jamani wazuieni … (*Anaiambia hadhira*), jamani wazuieni wasije kuni …

(*Anatetemeka*)

Sauti: Ah, hata wewe Bi. Kirembwe leo unagwaya?

Unatetemeka kama unjukuti unaopeperushwa na upepo? Unalia kama mtoto mchanga au mwanamke aliyefiwa na mumewe? Unahofu matokeo ya matendo yako mwenyewe …

Huu, kama ulivyokwisha sema, ni mchezo wa wakati:

FOR ONLINE READING ONLY

Wakati unaojibadilisha kama kinyonga,

Wakati unaofuata mahitaji ya wavunja-sheria

Na wafuata-sheria wakati mmoja, sawia;

Kufuata mahitaji na himaya ya nafsi moja dhidi ya nyingine …

Wakati unaowaridhi wawamba-ngoma …

Wakati wenye moyo wa kusubiri mpaka nukta ya mwisho ifike …

Hata ikiwa miaka, karne kwa karne …

Kungojea mwisho wa mwanzo, utakaposema:

"Ho! Sasa basi tena … hatesi mtesi na kufululiza …"

Wakati, mhodhi wa matatizo

Na unaoona leo na kesho

Na hatimaye kulipa baina ya wagomvi wawili

Baina ya nguvu mbili zinazovutana …

**Bi. Kirembwe:** Hakika wakati si wangu tena … (Anapiga kelele na kulia huku akijibanza kipembeni …)

*Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990:128-129)

**Maswali**

(i) Ni kwa namna gani mbinu ya utanzia imetumika kujenga ujumi katika matini hii?

(ii) Mbinu ya taharuki imetumikaje kujenga ujumi katika matini hii?

(iii) Ni kwa namna gani mbinu ya ujadi imetumika kujenga ujumi katika matini hii?

FOR ONLINE READING ONLY

(iv) Ni vifungu vipi vya maneno katika tamthiliya hii vinaakisi mbinu ya uteuzi na mpangilio wa maneno?

(v) Ni mbinu zipi nyingine za kiujumi zimetumika katika matini hii?

(b) Chambua mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika tamthiliya teule mbili ulizosoma.

## Maana na matumizi ya lugha katika matini za fasihi

Kazi yoyote ya fasihi huwa na maana. Mtunzi hukusudia kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira anayoilenga. Matini ya kifasihi hutofautiana na matini isiyo ya kifasihi (kama vile taarifa ya habari iwasilishwayo katika chombo cha habari) kutokana na matumizi ya lugha ya kifasihi. Lugha hiyo ya kifasihi hupatikana kutokana na matumizi ya mbinu za kifasihi. Baadhi ya mbinu hizo ni: semi (kama vile methali na nahau), tamathali za semi (kama vile sitiari, majazi, tashibiha, na tashihisi), mafumbo, lugha ya ishara na alama, na uteuzi na mpangilio maalumu wa maneno. Kutokana na matumizi ya mbinu hizi, matini ya kifasihi huwa na sifa ya kufikirisha kuliko matini isiyo ya kifasihi. Pia, mbinu hizo huifanya kazi ya fasihi iwe na mvuto kwa hadhira yake.

Hali ya hadhira kuwa na uwezo tofauti pamoja na kuwapo kwa lugha ya kifasihi katika matini husababisha hadhira kuibua maana tofauti katika matini moja. Hivyo, ili hadhira ipate maana iliyokusudiwa, hutakiwa kuwa na uwezo wa kung'amua maana mbalimbali ambazo zimefumbatwa katika mbinu hizo. Maana huweza kujitokeza katika kazi za kifasihi kama vile insha za kifasihi, mashairi na tamthiliya kama ifuatavyo:

### Maana zinazopatikana katika insha za kifasihi

**Shughuli ya 5.5**

(a) Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Uongo**

Uongo ni kinyume cha hakika ya mambo yaliyokuwa au yalivyo. Ni watu wachache ambao si waongo katika dunia. Watakaokudanganya au kukupunja hutumia uongo. Huweza kumsaidia mtu kujiokoa pengine, lakini ni mamoja yote kuwa uongo ni tabia mbaya na si kitu cha kupendelea katika maisha. Uongo hautazamiwi kwa watu waovu na wajinga peke yao, hata watu wema na wataalamu huutumia. Bahari moja ya hatari katika dunia ni uongo. Mwongo mmoja huweza kuangamiza watu kadha wa kadha. Uongo wa wajinga hugunduliwa upesi sana kuliko ule wa wataalamu. Baadhi ya

FOR ONLINE READING ONLY

madhara hutokea duniani kutokana na uongo wa watu wakubwa kuliko ule wa watu wadogo. Ukitaka kuwa mwongo lazima usiwe msahaulifu. Kutosahau ni jambo lifikirikalo lakini haliwezekani. Kwa hivi, njia ya mwongo fupi. Uongo ni kama giza, hukimbia mbele ya cheche ndogo ya nuru ya kweli. "Uongo hukimbia kweli ikidhihiri" ni methali ya Kiswahili ikumbushayo watu udhaifu wa uongo. Uovu mkubwa wa uongo ni mtu kujidanganya mwenyewe. Jambo kama hili hutokea mara kwa mara kwa waongo. Muongo humcha mno mtu kuliko Mungu.

*Insha na Mashairi* (Robert, 1967:1)

**Maswali**

(i) Ni maana zipi zinapatikana katika sentensi isemayo "Bahari moja ya hatari katika dunia ni uongo"?

(ii) Msemo wa "Ukitaka kuwa mwongo lazima usiwe msahaulifu" una maana zipi?

(iii) "Tashibiha" iliyotumika katika insha hii ina maana gani?

(iv) Ni maana zipi unaweza kuzipata katika sentensi ya "Baadhi ya madhara hutokea duniani kutokana na uongo wa watu wakubwa kuliko ule wa watu wadogo"?

(v) Ni taswira zipi unaweza kuziibua kutoka katika insha hii?

(vi) Ni maana zipi unaweza kuziibua kutokana na insha hii? Kwa nini?

(b) Soma insha ifuatayo, kisha chambua maana mbalimbali zinazopatikana katika insha hiyo.

### URAFIKI WA PAKA

Wanyama katika kuimarisha maisha yao, hujenga mahusiano wao kwa wao na kwa binadamu. Binadamu huwatumia wanyama hawa kwa shughuli kadha wa kadha. Wanyama wengine wana jukumu la kuleta burudani kwa binadamu kama vile gwaride, nyimbo, ngoma na vichekesho. Paka ni mmoja wa wanyama wenye urafiki na binadamu kutokana na mwenendo wake. Binadamu amekuwa akimwamini na kumpa kiti cha kushughulikia mambo mengi ofisini mwake.

Sauti isikikayo mithili ya kinanda humpatia paka upekee wa ajabu. Akimwona mgeni huimba kwa sauti nyororo! Nyau! Nyaau! Nyaaau! Nyaaaau! Mlio wake

FOR ONLINE READING ONLY

hupendwa na kila mtu ndani ya familia. Sauti yake ni ulinzi tosha dhidi ya wapangaji wanaochungulia na kudokoa mali ya binadamu.

Rangi nzuri inayovutia pamoja na macho yake mithili ya gololi ni baadhi ya vitu vinavyompa upekee. Paka ni doli la watoto na kitulizo murua cha watoto dhidi ya adui zao. Kiumbe huyu hukunja kucha zake vizuri ili zisimdhuru mtoto aliyembeba. Adabu hii amefundishwa na mama yake, ndio maana wahenga wanasema samaki mkunje angali mbichi.

Paka wetu ni mwaminifu na mlinzi bora, kwake udokozi ni mwiko. Hana tabia ya kula chakula isipokuwa amewekewa kwenye chombo maalumu. Chakula chake ni maziwa, michuzi na mifupa ya samaki.

Weledi wa kijasusi, paka amekirimiwa. Huweza kuwapigisha kwata maadui aliowateka. Hawa ni wale wenye mipango ya kumpora binadamu. Paka huwaona, kisha hutembea kwa kunyata taa! Taa! Taa! Taa! Kisha kuwarukia na kuwakamata.

Paka awapo vitani, hapati ngeu kichogoni. Ni jasiri ajabu! Asikiapo mlio wa nyoka siii! iiii! iiii! Hujipanga haraka kwa ajili ya kumdaka nyoka mithili ya golikipa. Siku moja, tulisikia vurugu kali juu ya dari, kumbe alikuwa nyoka aliyekuwa akipambana na paka. Paka alifanikiwa kumuua nyoka mkubwa na kushuka naye kutoka darini.

Usalama wa mali zetu upo mikononi mwa paka. Paka ana mbinu kabambe za kumdhibiti rafiki yake aitwaye Panya. Wakati mwingine humwimbia nyimbo kama:

> "Njoo tule nyama, njoo ×2
>
> Nyama hiyooo!
>
> Kimbiaaa!
>
> Njoo tufurahi."

Paka hutumia mbinu hizi kuwarubuni panya na hatimaye kuwakamata. Mali zetu ambazo ni nguo, vitabu, daftari na viatu vina usalama wa kutosha kutokana na kuwapo kwa paka.

Paka hukwea miti kwa maringo mithili ya kinyonga afukuzaye mawindo. Hapa

FOR ONLINE READING ONLY

hunoa mikuki yake tayari kwa mawindo na maadui. Wakati wa burudani hufanya mazoezi ya kupanda juu ya miti mirefu.

Ninawashauri watu wasiwapige paka kwa mawe; badala yake, wawajali na kuwapatia mahitaji yao kama vile: chakula, maziwa, nyama na maji. Paka ni mfalme kwa watu wenye busara ya kujali viumbe. Urafiki wa binadamu na paka unapaswa kuwa wa kudumu. Wanyama wengine hawana budi kuiga matendo ya paka ili kudumisha urafiki na binadamu.

**Shughuli ya 5.6**

(a) Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Kifo cha Mende Wekundu**

*Na ujenge yako nyumba, jingi jasho likuoshe,*
*Ufyeke, upime na uweke nguzo,*
*Kisha paa na uweke na ukandike,*
*Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.*
*Wataanza kutalii mipaka mende usiku,*
*Nje na ndani ya nyumba watazunguka,*
*Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,*
*Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.*
*Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,*
*Ukae nje nzima siku usubiri,*
*Wazima wamelala ukirudi usiku,*
*Vichwa ngumu hawafi mende rahisi.*
*Kifo cha mende sharti miguu juu,*
*Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,*
*Na kisha wengine usiku mchana uwasake,*
*Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.*

*Karibu Ndani* (Kezilahabi, 1988:33)

FOR ONLINE READING ONLY

**Maswali**

(i) Ni maana zipi unaweza kuzipata katika mstari usemao "Wataanza kutalii mipaka mende usiku"?

(ii) Ni taswira zipi unaweza kuzijenga kutokana na jina la shairi hili?

(iii) Mstari usemao "Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula" una maana zipi?

(iv) Mstari usemao "Kifo cha mende sharti miguu juu" unamaanisha nini?

(v) Ni njia zipi umezitumia katika kupata maana za mistari iliyodondolewa katika maswali namba i, iii na iv?

(vi) Ni maana zipi unaweza kuibua kutokana na shairi hili? Kwa nini?

(c) Soma mashairi mawili kutoka katika diwani teule, kisha, kwa uthibitisho wa mifano, chambua maana na mbinu mbalimbali za kiujumi zinazopatikana katika mashairi hayo.

**Maana zinazopatikana katika tamthiliya**

**Shughuli ya 5.7**

(a) Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Bi Moja: Vipi habari ya safari. Mbona umerudi na vitambaa vyote?

Bi Tano: Hakuna wanunuzi.

Wote: Aah hata! Haiwezekani!

Bi Moja: Hata haiwezekani! Sema tu hukwenda.

Bi Tano: [*Amekasirika*]: Yaani mnasema mimi mvivu siyo?

Nimezunguka mji mzima na zigo hilo halafu mnaniambia mimi mvivu? Nawaambia watu hawataki kununua. Au mlitaka niwagawie bure.

Bi Nne: Lakini kwa nini wakatae kununua hivi, mbona vile vya mwanzo walinunua?

Bi Moja: Tena walikuwa wanavigombania.

FOR ONLINE READING ONLY

Bi Tano: [*Amekasirika zaidi*]: Kila nilipokwenda wananiambia wameshanunua vya kutosha. Sasa mimi ningewalazimisha?

Bi Moja: Biashara inataka bembeleza eti.

Bi Nne: Eee. Unasema maneno matamu matamu. Basi hivihivi tu watu watanunua?

Bi Tano: Basi chukueni muende mkauze wenyewe

[*Anaondoka amekasirika*]

Bi Moja: Huyo Bi Tano mwacheni. Kichwa chake kibovu.

Jamani saa imekwisha. Hebu tugawane hivi vitambaa kila mtu akauze katika eneo lake.

[*Wote wanagawana vitambaa*]

Bi Nne: Haya maarifa mazuri. Jamani tujitahidi tukikutana wiki ijayo kila mtu awe ameshauza vya kwake.

*Nguzo Mama* (Muhando, 2007: 16–17)

**Maswali**

(i) Ni maana zipi zinazopatikana katika sentensi isemayo "Biashara inataka kubembeleza eti."

(ii) Mvutano baina ya Bi Tano na wenzake unaibua maana zipi?

(iii) Mitazamo ya wahusika katika kipande hiki cha tamthiliya inaibua maana zipi za kiujumi?

(iv) Ni mbinu gani zimetumika kupata maana kutoka katika kipande hiki cha tamthiliya?

(v) Ni maana zipi nyingine unazoweza kuibua kutokana na kipande hiki cha tamthiliya?

(b) Chambua maana mbalimbali zinazopatikana katika tamthiliya mbili teule.

FOR ONLINE READING ONLY

## Mbinu za kifasihi zinavyoathiri kupatikana kwa maana katika kazi za fasihi

Katika machakato wa usomaji, huweza kuibuka maana tofauti kwa kila msomaji. Jambo, hili huweza kutokana na jinsi msomaji anavyofasili taswira mbalimbali zilizotumiwa. Kuwapo kwa uwezekano wa kupatikana kwa maana mbalimbali kunatokana na mtunzi kutumia mbinu ya kifasihi ya ufumbaji. Hii inamaanisha kuwa, kama mtunzi asingefumba, maana ingekuwa ya wazi na ya moja kwa moja. Hivyo, kuwapo kwa maana tofauti kunatokana na mbinu za uandishi na utungaji ambao hufasiliwa kwa njia tofauti kwenye sehemu au kazi nzima ya kifasihi. Mbinu za kifasihi hutumika katika kazi mbalimbali za kifasihi kulingana na nini mtunzi anapenda kuandikia. Mbinu hizo zinabainika katika shughuli ifuatayo.

### Mbinu za kifasihi zinavyoathiri kupatikana kwa maana katika mashairi

**Shughuli ya 5.8**

(a) Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata:

**Shetani, Rangi Rangile**

*Aa, awali sisi twanena, sisi sisi wananchi,*
*Ama kiza twakiona, ni kiza hiki hakuchi,*
*Mbaya wetu karudi, karudi tena mbichi,*
*Huu ukweli nanena, kweli siyo pirikichi,*
*Mbaya wetu karudi, shetani rangi rangile.*

*Ba, bahari tunaiona, bado haina shuwari,*
*Mawimbi yatatizana, mkondoni menawiri,*
*Tufani ni nana nana, katu hatuoni heri,*
*Roho atuminya sana, ka jeuri na kiburi,*
*Mbaya wetu karudi, shetani rangi rangile.*

*Diwani ya Tunzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein* (Rashid, 2016:166)

**Maswali**

(i) Ni mbinu zipi za kifasihi zimetumika kupata maana katika shairi hili?

FOR ONLINE READING ONLY

(ii) Ni mbinu zipi za kifasihi zimekutatiza kupata maana katika shairi hili?

(iii) Una maoni gani kuhusu kufaa au kutofaa kwa mbinu za kifasihi zilizotumika katika shairi hili ili kuleta maana?

(iv) Mstari unaosema 'Mbaya wetu karudi, shetani rangi rangile' una maana gani?

(b) Kwa kutumia diwani teule, chambua shairi moja, kisha onesha namna mbinu za kifasihi zilivyochangia au kutatiza kupatikana kwa maana.

**Mbinu za kifasihi zinavyoathiri kupatikana kwa maana katika tamthiliya**

**Shughuli ya 5.9**

Soma matini fupi ya tamthiliya ifuatayo, kisha chambua namna mbinu za kifasihi zinavyoathiri maana.

Moyo: [*Anaitazama hali iliyowazunguka*]

Nani wa kulaumiwa? Kati ya mpunga uliosababisha viroboto au mwenye mguu anayeshindwa kutoa funza?

[*Anazama kwa tafakuri nzito*].

Macho: wote.

Moyo: Ikiwa wote, tupe sababu kuntu. Kwa nini?

Macho: Wote wanaonekana. Mimi ninalaumu kila anayeonekana.

Ndani joto ni kali sana, nasema na nje baridi ni kali sana sitakaa kimya.

Akili: Hahahah! [*Kicheko*], wanadunga wa kwetu, wao wanauza.

Masomo yao moshi ni sumu ya kwetu moshi ni chakula, twala na hatushibi.

Moyo: Nani alaumiwe? Someni pale "Ni hatari kwa mustakabali wako." Haya niambieni, nani alaumiwe? Anayetoa ujumbe ule ndiye anayekusanya kodi kutoka palepale.

[*Anaonesha kwa kidole*].

FOR ONLINE READING ONLY

**Macho:** Kweli sio wote. Mimi nimekuwa nikishuhudia wa kwetu tu ndo hukamatwa. Wasanii wetu, wachezaji wetu na … naa … [*Anakatishwa*].

**Akili:** Na viongozi ni wetu.

**Macho:** Na watoto wa viongozi.

**Moyo:** Watoto wa viongozi?

**Macho:** Watoto wetu jamani wana mambo.

**Moyo:** Watoto wetu au wa viongozi?

**Akili:** Ninakariri, wetu. [*Amekaza macho*]

**Macho:** [*Anatahamaki, apiga kalele*].

Nyie nyie … mnafanya ajizi na mnahisi ni madogo ingawa yana ukubwa wake.

[*Kama mtu alipandwa na mchera*].

**Moyo:** Madogo?

**Akili:** Kama haya ni madogo, makubwa ni yapi?

**Macho:** Unataka kujua makubwa, ebu geuka kuleee. Mi naona ndoa,

Ninyi mnaona pia. Geuka huku. Ndoa yenu yawa yao

[*Wote wanageukageuka huku na huku kama mazuzu*].

*Nje-ndani* (Mswahili na Njonjolo, 2016:22)

**Maswali**

(i) Ni mbinu zipi za kifasihi zimekuwezesha kupata maana katika matini hii?

(ii) Ni mbinu zipi za kifasihi zimekutatiza katika kupata maana katika matini hii?

(iii) Una maoni gani kuhusu kufaa au kutofaa kwa mbinu za kifasihi zilizotumika katika matini hii katika kuleta maana?

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 5.10**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandao, maktaba au matukio halisi, kusanya mazungumzo ya makundi mawili (mtoto au watoto wadogo wenye umri wa kuanza shule na kiongozi yeyote wa serikali kisha tathmini aina, maana na mpangilio wa hoja zinazotolewa katika mazungumzo ya kila kundi.

## Misingi ya ujenzi wa hoja zenye mantiki na ushawishi

Ujenzi wa hoja zenye mantiki na ushawishi humtaka mtoahoja awe razini na makini. Hoja hizo hujengwa kwa kuzingatia misingi ya uadilifu, ushawishi, kudhihirisha uhakika wa jambo, hadhira, muundo, na mpangilio wa kimantiki.

Kwa muktadha wa ujenzi wa hoja, dhana ya uadilifu hujumuisha hali za ukweli, usawa, heshima, usahihi, na uhalisi wa jambo linalowasilishwa. Mjengahoja hutakiwa kuepuka kuwasilisha jambo kwa namna ya kumshambulia au kumbeza mtu. Pia, hutakiwa kuwasilisha jambo lenye ukweli na la usahihi. Atumie data sahihi ili kuipa nguvu hoja yake. Hivyo, hadhira yake itavutiwa na kuamini hoja zake.

Mjengahoja pia hutakiwa kuwasilisha hoja zake kwa ufasaha. Aoneshe kujiamini ili aiaminishe hadhira yake kuwa ana uhakika na anachokiwasilisha. Katika maelezo ya hoja yake, aoneshe ufundi wa kuhusisha mifano na mazingira halisi. Kwa kufanya hivi, huonesha mamlaka ya kimaarifa na kiujuzi juu ya anachokiwasilisha; na hadhira hupata imani kuwa inapokea hoja kutoka kwa mtu sahihi.

Pia, mjengahoja hutakiwa kutumia mbinu ya ushawishi kwa hadhira yake juu ya kinachowasilishwa. Mjenzi mzuri wa hoja huzingatia suala la kugusa hisi za hadhira yake ili kuihamasisha kupokea, kuamini na kutumia hoja zake. Nguvu ya ushawishi husaidia kuimarisha kile kilichomo katika akili ya hadhira. Pia, kama hadhira ilikuwa katika uelekeo tofauti wa jambo linalowasilishwa, ushawishi husaidia kuivutia kwenye uelekeo wa mwasilishaji. Mbinu za kujenga ushawishi ni pamoja na kutumia mifano halisi, mbazi, simulizi fupi, uteuzi wa maneno yenye uwezo wa kuamsha hisia za hadhira, na semi mbalimbali kama vile misemo, methali, nahau na misimu.

Kadhalika, mjengahoja anapaswa kuzingatia hali ya hadhira. Hali ya hadhira hujumuisha uwezo wa kuelewa, wastani wa kiwango cha elimu, wastani wa tajiriba ya maisha, mwelekeo wa malengo, matarajio, utamaduni, pamoja na hali ya kisaikolojia. Uzingatizi wa hali hizo za hadhira humsaidia mjenga hoja

FOR ONLINE READING ONLY

kuteua na kutumia maneno, vipamba-lugha (kama vile toni na kidatu), na mifano muafaka. Vilevile, humsaidia kutathimini uelewekaji wa wasilisho wakati anaendelea kujenga hoja.

Isitoshe, mjengahoja anapaswa kuzingatia muundo mzuri. Mjenzi mzuri wa hoja lazima atafakari suala hili ambalo lina athari kubwa katika mpangilio wa anachowasilisha. Hata kama hoja yake ni moja, lazima aiunde vyema. Ajiulize kuhusu nini kianze kuwasilishwa na nini kifuatie. Kama hoja zipo zaidi ya moja, atafakari kuhusu kubebana, kusababishana na kuendelezana kwa hoja hizo. Hivyo, ni vyema aliunde wasilisho lake katika namna inayorahisisha kueleweka kwake.

## Kutathmini kazi za fasihi kwa kutumia misingi ya ujenzi wa hoja zenye mantiki na ushawishi

Misingi ya ujenzi wa hoja zenye mantiki na ushawishi hutumiwa pia kutathmini vipengele mbalimbali vya fani na maudhui katika kazi za fasihi. Misingi ambayo hutumika kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi ni pamoja na uadilifu, ushawishi, kudhihirisha mamlaka, na kutilia maanani hadhira na muundo. Miongoni mwa vipengele vilivyomo katika kazi ya fasihi ambavyo huweza kutathminiwa ni matendo ya wahusika ambayo yakisawiriwa vyema hudhihirisha hoja zenye mantiki.

**Shughuli ya 5.11**

(a) Kwa kutumia kipande kifuatacho cha tamthiliya, jenga hoja zenye mantiki na ushawishi kuhusu ujenzi wa wahusika.

| | |
|---|---|
| **Mlinzi I:** | We, we … simama! (*Anamkaribia Mwari I*) |
| | Nasema simama … nani aliyekutieni msuko huu? |
| | Nani kakutieni damu mpya? Mlikuwa watulivu nyinyi … We… wewe… (Mlinzi anamfikia na kumkamata mkono mwari) |
| **Mwari I:** | Nyeupe ni nyeupe na nyeusi ni nyeusi … na nyekundu ni nyekundu, nyekundu haiwezi kuwa manjano … |
| **Mlinzi I:** | Sharrab! Unajuaje wewe? Nyeupe ni nyeusi na nyeusi ni nyeupe na nyekundu kila siku ni manjano … |



FOR ONLINE READING ONLY

Mlinzi II: (*Anamkamata mwari 2*) Nimekukamata sasa … kwa nini ukaniendesha mbio? Kwa nini unanitimua? Tazama, unaona n'navyohema hivi? Pumzi juujuu, kwa nini? Mmekuwa kama mang'ombe yaliyovunja zizi kwa njaa na kiu ilhali mnashiba? Kwa nini hamtaki kushiba utulivu wa miaka mingi uliopo Giningi? Kwa nini mnaona kiu kwenye maji safi? Nyinyi waharibifu …

Mwari II: Mchana ni mchana na usiku ni usiku; na ikiwa kumekucha basi kumekucha; asemaye bado ni usiku wa manane ni mwongo …

Mlinzi III: Nani mwongo hapa enh? (Anamwelekeza nalo rungu, lakini mwari anarudi nyuma)

Mwari III: Haijapata kutokea fujo hapa Giningi. (Huku akimfukuza … Mwari III anapiga kelele)

Mlinzi IV: Mmekula … mmeshiba; mmelishwa sumu nini nyinyi? Sumu gani? Na nani? Ah, mnataka kutwambia nini sasa? Mnataka kutwambia kwamba kuanzia leo jua halitatoka Magharibi na kuzama Mashariki? Mnataka kutwambia kwamba mchana kuna jua na usiku kuna kiza? Nani kasema hayo? Mmejigeuza watume wapya nyinyi mnakuja kuleta wahyi mpya hapa Giningi? Ah, wako wapi wafalme wetu wa Giningi? Nyinyi …

Mwari IV: Ndiyo … tunasema ndiyo, sote kwa umoja wetu, sasa tunaliona jua halitoki Magharibi: jua linatoka Mashariki na kuchwea Magharibi; hiyo ndiyo kanuni ya mwenendo wa jua enzi na azali! Ulimwenguni kote… na … na … (*Anahema*) usiku usio mbalamwezi na nyota ni kiza … kiza kitupu … na mchana usiyo mawingu ni mwangafu kwa jua linalodanda …

Mlinzi V: Ngoja utaona … (*Kwa mwari V*)

*Walinzi na wari wengine wanaingia na kutoka na sauti za mabishano zinazopandana na kuingiliana huku wakifukuzana na zogo na ghasia …*

*Kivuli kinaishi* (Mohamed, 2009:103-104)

FOR ONLINE READING ONLY

(b) Kwa kutumia misingi ya ujenzi wa hoja zenye mantiki na ushawishi, tathimini matendo ya wahusika katika tamthiliya teule mbili.

## Kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi kwa kutumia maarifa ya kifasihi

Maarifa ya kifasihi hujumuisha umilisi wa vipera mbalimbali vya fasihi simulizi na andishi. Kazi yoyote ya fasihi huwa na mambo yanayoweza kutumiwa katika maisha halisi. Miongoni mwa matumizi hayo ni kujengea hoja zenye mantiki na ushawishi. Mjenzi wa hoja za kimantiki huweza kutumia vipera kama vile methali, hadithi, na tamathali za semi ili kukazia au kunogesha hoja yake. Jambo muhimu ni mjengahoja kuteua kipengele cha kifasihi ambacho ni sahihi na muafaka katika muktadha wa hoja yake. Kwa ujumla, maneno, vifungu na tungo za kifasihi huwa na mvuto na mguso wa kipekee. Kutokana na mguso huo, zikitumiwa kwa usahihi sambamba na misingi ya kujenga hoja za kimantiki, hurahisisha kueleweka na kushawishi hadhira. Hoja zenye mantiki na ushawishi zinaweza kutumiwa na watu katika sehemu mbalimbali wakati wa kueleza au kuomba kitu fulani. Sehemu ambazo hoja za kimantiki hutumika ni kama vile kwenye usaili wa kazi au kwenye malumbano ya hoja. Maelezo yafuatayo yanafafanua namna hoja za kimantiki na zenye ushawishi zinavyotumika katika usaili na malumbano ya hoja.

### Kutumia maarifa ya kifasihi kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi katika usaili

**Shughuli ya 5.12**

(a) Soma dayalojia ifuatayo ya usaili, kisha jibu maswali yanayofuata:

Mwenyekiti wa Jopo: Jitambulishe tafadhali.

Msailiwa: Ninaitwa Nagona Dhifa Mzingile. Nina miaka 26. Nimezaliwa na kukulia wilayani Songea, mkoani Ruvuma. Nilianza masomo ya msingi mwaka 2005 katika Shule ya Msingi Mpangula na kuhitimu mwaka 2011. Kisha, nikajiunga na elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari Namtumbo na kuhitimu mwaka 2015. Baada ya hapo, nilisoma elimu ya sekondari ya juu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Songea na kuhitimu mwaka 2018. Baadaye, nilijiunga na masomo ya juu, ambapo mwaka 2023 nilitunukiwa Shahada

FOR ONLINE READING ONLY

ya Awali ya Sanaa katika Ualimu, nikizamia somo la Kiswahili.

Mwenyekiti wa Jopo: Vyema. Kwa nini umeomba nafasi hii ya kazi?

Nagona: Nimeomba nafasi hii ya kazi ya kuwa msaidizi wa ukufunzi katika chuo hiki kwa sababu nina uwezo na ninapenda kutumia elimu na taaluma yangu kuwasaidia wengine kupitia taasisi hii.

Mwenyekiti wa Jopo: Bi. Nagona, kuna taasisi nyingi ambazo ungeweza kuzitumia kutimiza shabaha na mapenzi yako hayo, kwa nini iwe taasisi hii?

Nagona: Ndugu mwenyekiti, nimependa kuwa hapa kwa sababu mbili. Mosi, hii ni taasisi ya ndoto yangu kwa sababu siku nyingi nimekuwa nikiota kufanya kazi hapa. Pili, ni sababu ya kuwapo kwa hiyo ndoto. Nimekuwa nikiifuatilia taasisi hii tangu nikiwa katika hatua za chini za elimu; na nimekuwa nikishuhudia jinsi taasisi hii ilivyo tegemeo la taifa kwa kuzalisha wataalamu wa kada mbalimbali. Hivyo, nikapata shauku ya mimi kuwa mmoja wa wapishi wa wataalamu hao. Sababu ya tatu ndugu Mwenyekiti ni kuwa taasisi hii imekuwa ya kwanza kutoa tangazo la kazi tangu nihitimu. Hivyo, kama wasemavyo wahenga kuwa, "mvua za kwanza ndo za kupandia", nami niliona niichangamkie mvua hii ya kwanza kunyesha kwa muktadha wa kusaka ajira.

Mwenyekiti wa Jopo: Karibuni wajumbe tumuulize maswali msailiwa.

Mjumbe 1: Bi. Nagona, una kipi cha kutushawishi kuwa wewe ni bora kuliko waombaji wengine wa nafasi hii?

Nagona: Ndugu Mwenyekiti na jopo zima, ninawahakikishia kuwa mimi ni bora kuliko wengine kwa sababu zifuatazo: Mosi, matokeo yaliyomo katika vyeti vyangu vya elimu na taaluma yananibainisha

FOR ONLINE READING ONLY

mimi kama dhahabu iliyo katikati ya mchanga. Pili, ni uzoefu nilioupata katika kufundisha somo la Kiswahili katika shule za sekondari wakati wa mafunzo kwa vitendo na wakati wa ufundishaji wa kujitolea baada ya kuhitimu masomo yangu ya elimu ya juu.

Mjumbe 2: Una ahadi au matumaini gani ya kipekee unayotupatia ikiwa tutakuajiri?

Nagona: Ninaahidi kuigeuza taasisi hii kuwa kijiji imara cha wataalamu wa Kiswahili.

Mjumbe 3: Kufanya kazi katika taasisi kama hii kuna changamoto nyingi. Je, unazifahamu changamoto hizo? Na umejiandaaje kuzikabili?

Nagona: Ninatambua kuwa taasisi kama hii ambayo hujumuisha watu wengi lazima itakuwa na changamoto. Mfano wa changamoto hizo ni kuwapo kwa akili na mitazamo tofauti ya kuyakabili masuala kadha wa kadha, wingi wa mambo yanayotokea, na masuala mengine yanayoendana na tabia za watu. Hata hivyo, nimewahi kusoma riwaya moja iitwayo *Kusadikika* ambayo mhusika wake mkuu, Karama, alinifundisha kuwa mapambano ya maisha yanahitaji vitu vikubwa vitatu ambavyo ni ubongo wenye utulivu, ulimi wenye staha, na moyo wenye ujasiri na saburi. Ninalihakikishia jopo hili kuwa nitatumia zana hizo tatu kukabiliana na changamoto zitakazotokea hapa. Ijapokuwa natambua kuwa si kazi rahisi, bali penye nia pana njia, hivyo ninatia nia ya kufanikiwa kuzikabili.

Mjumbe wa 4: Bi. Nagona una matarajio gani kuhusu kiasi cha mshahara kama ukipata kazi hii?

Nagona: Ninashukuru sana kwa swali hili. Matarajio yangu ni kulipwa kufuatana na viwango vya mishahara vinavyoendana na ujuzi na elimu yangu.

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti wa Jopo: | Bi. Nagona, jopo limekusikiliza na kukagua vyeti vyako. Tunakuruhusu uende. Nasi tunaendelea kukamilisha mchakato huu. Tutakujulisha matokeo yoyote yatakayoamuliwa kwa kutumia mawasiliano uliyoyaweka katika barua ya maombi pamoja na taarifa za wasifu kazi wako. |
| Nagona: | Asanteni sana, ninasubiri kwa hamu matokeo hayo. Je, ni lini yanatarajiwa kuwa tayari? |
| Mwenyekiti wa Jopo: | Ndani ya juma moja kuanzia leo utapata majibu. |
| Nagona: | Asanteni, na kwa kwaherini. |

**Maswali**

(i) Kwa nini unafikiri utambulisho ni muhimu katika usaili?

(ii) Je, unafikiri hoja za msailiwa zilikuwa na mantiki na ushawishi? Kwa nini?

(iii) Ni maeneo yapi msailiwa ametumia maarifa ya kifasihi kujenga hoja zake?

(iv) Ungekuwa Nagona, ungejibuje swali kutoka kwa Mjumbe wa 1, Mjumbe wa 3 na Mjumbe wa 4?

(b) Tumia maarifa ya kifasihi kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi wakati wa kuigiza kama msailiwa wa nafasi ya kazi.

(c) Tumia maarifa ya kifasihi kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi wakati wa kuigiza kama mgombea wa nafasi ya uongozi katika uchaguzi wa shuleni kwenu.

**Shughuli ya 5.13**

Chagua mada mojawapo kati ya zifuatazo, kisha andaa hoja unazoweza kuwasilisha katika malumbano ya hoja kwa kutumia maarifa ya kifasihi kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi.

(i) Athari za utandawazi kwa vijana

(ii) Mchango wa fasihi katika utunzaji wa mazingira

FOR ONLINE READING ONLY

(iii) Nafasi ya lugha ya Kiswahili katika kukuza uchumi wa taifa

(iv) Dhima ya lugha ya Kiswahili katika kuleta umoja wa Afrika ya Mashariki.

**Kutumia maarifa ya kifasihi kuwasilisha hoja zenye mantiki na ushawishi katika malumbano ya hoja**

Malumbano ya hoja ni jukwaa muhimu katika kuwasilisha masuala mbalimbali. Vilevile, ni nafasi nzuri ya kukuza maarifa ya kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi. Katika ulimwengu wa kidijiti, malumbano ya hoja yanaweza kufanyika kwa kutumia vyombo vya habari kama vile runinga, redio na majukwaa ya mtandaoni. Wahusika hupeana mada kwa ajili ya kufanya maandalizi (yaani kuandaa taarifa za msingi, ushahidi na kupangilia mawazo kimantiki), kisha hukutana kwa ajili ya uwasilishaji. Kwa kawaida, hoja huwekwa mezani kisha kila mmoja hutoa mawazo yake kulingana na uelewa wa hoja hiyo. Ni muhimu kupeana nafasi wakati wa uchangiaji wa mawazo ili kuruhusu maelewano na kuheshimu mawazo ya mwingine katika mjadala. Vilevile, malumbano ya hoja huongeza maarifa ya usikivu.

**Shughuli ya 5.14**

Andaa hoja zenye mantiki na ushawishi unazoweza kuziwasilisha katika malumbano ya hoja kuhusiana na mada yoyote kwa kutumia maarifa ya kifasihi.

**Tamrini**

1. Kwa kutumia mifano, fafanua mbinu zinazotumika kujenga ujumi.
2. "Kujenga hoja kimantiki hakuna tija yoyote" Jadili hoja hii kwa mifano thabiti.
3. Eleza namna utakavyojenga hoja zenye mantiki na ushawishi kwa kutumia misingi ya kifasihi.
4. Fafanua namna misingi ya kifasihi inavyoweza kutumika kutathimini matendo ya wahusika katika kazi ya fasihi.
5. Kwa kutumia mada ya 'athari za dawa za kulevya kwa watoto wa mtaani', andaa hoja zenye mantiki na ushawishi.
6. Tumia misingi ya kujenga hoja zenye mantiki kutathmini maudhui ya simulizi yoyote.

FOR ONLINE READING ONLY

7. Chambua vipengele vya ujumi vilivyotumika katika mashairi mawili kutoka diwani teule.

8. Waandishi wa tamthiliya wametumia mbinu za kiujumi kutunga kazi zao. Jadili kauli hii kwa kutumia tamthiliya teule moja.

9. Chambua vipengele vya ujumi katika tamthiliya ya *Nguzo Mama*.

10. Fafanua vipengele vya kiujumi vilivyotumika katika nyimbo mbili za taarabu.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Sita

# Kubuni kazi changamani za fasihi

## Utangulizi

*Kazi za fasihi ni muhimu katika jamii kwa sababu huburudisha, huelimisha, hueneza tamaduni mbalimbali na huchochea mawazo mapya kwa wasomaji. Katika sura hii, utajifunza juu ya miktadha inayochagiza utunzi wa kazi changamani za fasihi, fursa zinazotokana na kazi za fasihi; na mchango wa TEHAMA katika kutambua fursa zinazotokana na kazi za fasihi. Pia, utajifunza hatua na kanuni za utunzi, na kutunga kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi. Umahiri utakaojenga katika sura hii utakuwezesha kutunga maigizo, mashairi na hadithi za watoto; na kuzitumia kazi hizo kama fursa ya kujipatia kipato binafsi na cha jamii kwa ujumla.*

*Namna utunzi wa kazi za fasihi zinavyochochea maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla*

**Shughuli ya 6.1**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, eleza miktadha inavyochagiza utunzi wa kazi za kifasihi.

(b) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni au maktabani, kusanya kazi tano (5) za fasihi za tanzu tofauti kisha chunguza na chambua miktadha iliyoziibua.

### Miktadha ya utunzi wa kazi changamani za fasihi

Kazi za kifasihi ni matini ambazo hutumia lugha, ubunifu na vionjo vya kifasihi. Kwa hiyo, kazi hizo ni matini ambazo huwasilishwa kwa ubunifu. Kazi hizi hutofautiana na kazi nyingine zisizo za kifasihi kutokana na mbinu za uandishi kama vile uundaji wa wahusika na matumizi ya lugha ya kisanaa. Kazi za kifasihi

FOR ONLINE READING ONLY

hujumuisha matini iliyo katika umbo la utungo mmoja kama vile semi mbalimbali, hadi matini zenye mchanganyiko wa mambo mengi. Mifano ya matini hizo ni insha za kifasihi, ushairi, tamthiliya, hadithi fupi, na riwaya. Kazi changamani ni zile zenye mchanganyiko wa mbinu nyingi za kisanaa. Pia, kazi hizi huwa na idadi kubwa ya vipengele kama vile vya wahusika, visa, mikasa, migogoro, mandhari na dhamira.

Kubuni ni mchakato wa kusawiri mawazo kwa kutumia mbinu za kisanaa. Mchakato huu huweza kufanyika katika nyuga mbalimbali, ambapo huanzia akilini mwa mtu kisha hudhihirika kupitia maumbo mbalimbali. Katika uga wa fasihi, ubunifu hujitokeza kupitia maumbo kama vile shairi, insha, hadithi, riwaya, tamthiliya na utenzi. Watunzi wa kazi za fasihi huwa na kipaji, lakini wengine huwa watunzi bora kwa kujifunza. Kazi ya kubuni hutakiwa iwe na sifa kama vile: fikra za kisanaa kuhusu jambo au tukio; lengo au ujumbe maalumu; upya wa namna fulani; umuhimu kwa jamii, na izingatie maslahi na maadili ya jamii.

Uandishi wa kazi za fasihi ni mchakato wa kiubunifu. Katika kuandika kazi za fasihi, msanii au mwandishi huanza kwa kujiuliza maswali kadha wa kadha. Baadhi ya maswali hayo ni: Anaandika kuhusu nini? Anamwandikia nani? Anaandika kwa kutumia mandhari ipi? Lengo lake ni nini? Na, anaandika kwa namna gani? Kwa kuwa mwandishi huandika kazi yake ili isomwe na watu wengine, hana budi kuzingatia mahitaji na mitazamo ya wasomaji wake ili aweze kuwapeleka anakotaka huku wakiendelea kufurahia kusoma kazi husika.

Waandishi wa kazi za fasihi huandika kazi zao kwa malengo tofauti. Miongoni mwa malengo hayo ni kusawiri uhalisi wa kijamii ili kuurekebisha au hata kuubadili ikibidi. Hii ina maana kuwa mwandishi sharti aibuke na vitu vipya ambavyo vitawavutia wasomaji katika kuwahabarisha yale yanayotokea katika jamii yao. Vilevile, waandishi wa kazi za fasihi huandika kwa lengo la kuelezea hisia zao ambazo wanaamini kuwa zitawavutia wasomaji wao ili wayaone maisha kama wanavyoyaona wao. Pia, waandishi wanaandika ili kuwaburudisha wasomaji wao. Hii inatokana na ukweli kuwa katika mchakato wa usomaji, msomaji hupata maarifa na burudani. Halikadhalika, waandishi huandika ili kuwashawishi wasomaji wao wakubali ukweli na namna ya kufasili mambo mbalimbali kama wanavyofanya wao. Mbali na hayo, waandishi huandika kwa lengo la kujipatia fedha kutokana na mauzo ya kazi hizo. Baadhi ya waandishi huandika ili watambuliwe na jamii zao.

FOR ONLINE READING ONLY

Kuna miktadha mbalimbali ambayo humsukuma mwandishi kuandika kazi ya fasihi. Miktadha hiyo ni mipana na inaweza kutofautiana kulingana na mtu binafsi. Hata hivyo, kuna baadhi ya miktadha ya jumla ambayo mara nyingi huweza kuchochea ubunifu na uandishi mzuri wa kazi za fasihi. Hivyo, utunzi wa kazi yoyote ya fasihi huweza kuchochewa na miktadha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijiografia.

Muktadha wa kisiasa huchangia utunzi wa kazi za fasihi kwa kuangazia masuala ya kisiasa katika jamii na athari zake. Masuala ya kisiasa hujumuisha vipengele kama vile mifumo ya uongozi, haki za binadamu, sera mbalimbali, mapinduzi, mageuzi na hali za matabaka ya watu. Vilevile, mazingira ya kisiasa yanaweza kusababisha mizozo na migogoro, uhasama, na changamoto kwa watu binafsi, familia na jamii kwa ujumla. Masuala haya yanaweza kumsukuma mwandishi kutunga hadithi, mashairi, tamthiliya na riwaya au andiko lolote la kiubunifu linalosawiri masuala hayo.

Muktadha wa kijamii hujumuisha matatizo, mahitaji, uhusiano, kuamiliana, changamoto za kijamii kama umaskini na ukosefu wa ajira, na matarajio ya jamii. Kwa kuzingatia muktadha huu, mtunzi anaweza kuchochewa kuandika kazi za kifasihi zinazogusa masuala yanayohusu maisha ya watu katika jamii.

Muktadha wa kiuchumi unaweza kuwa chanzo cha msukumo wa uandishi wa kazi za fasihi kwa namna mbalimbali. Uchumi unaweza kuhusisha masuala ya kazi, ajira, umaskini, utajiri, biashara, ujasiriamali na mifumo ya kiuchumi. Mwandishi anaweza kuandika hadithi zinazochunguza maisha ya watu katika mazingira ya umaskini, mapambano yao, na jinsi hali ya kiuchumi inavyowaathiri. Pia, uandishi wa fasihi unaweza kuchunguza masuala ya maadili katika uchumi kama vile ufisadi, uaminifu, uadilifu wa kibiashara, na misingi mingine inayohusiana na fedha na utajiri.

Muktadha wa kiutamaduni hutumika katika utunzi wa kazi za fasihi kupitia usawiri wa mavazi, vyakula, mila, desturi na dini za jamii husika. Kadhalika, mwandishi anaweza kuchochewa kuandika kazi ya fasihi inayochunguza migongano ya tamaduni na mila za jamii mbalimbali. Vilevile, mazingira ya dini yanaweza kumvutia mtu kuandika kazi ya fasihi kwa kuzingatia migogoro, mazungumzo na mwingiliano wa imani za kidini. Aidha, mwandishi anaweza akasawiri historia ya sehemu na matukio ambayo yameacha athari kubwa katika jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

Muktadha wa kijiografia hujumuisha vipengele kama vile: sura ya nchi, uoto, bahari, maziwa, mito, na hali ya hewa. Vipengele hivi vina nguvu ya kushawishi kuandika kazi ya fasihi. Aghalabu, kazi zinazotokana na msukumo wa kijiografia husawiri masuala ya mazingira. Mwandishi anaweza kutunga hadithi, mashairi, riwaya au tamthiliya zinazojadili masuala ya viumbe hai na mazingira ya asili kulingana na uzoefu wake.

Mbali na miktadha hiyo, uandishi wa kazi za kifasihi, kwa kiasi kikubwa, huchochewa na maisha ya mwandishi na uzoefu wake binafsi. Mambo haya huibua hisia, matukio muhimu maishani, na changamoto anazokutana nazo mwandishi. Hayo yote humchochea mwandishi kuandika utungo wa kiubunifu ili kuyawasilisha kwa wengine. Hata hivyo, licha ya kuwa kila mwandishi ana vyanzo vyake vya kipekee vinavyomchagiza kuandika kazi za fasihi ni muhimu kujifunza kutoka kwa wengine, na wakati huohuo kudumisha msukumo wa ndani wa kuandika ili kuendeleza uwezo wake wa kiubunifu katika uandishi wa kazi za kifasihi.

**Zoezi la 6.1**

1. Eleza maana ya kutunga kazi changamani za kifasihi.
2. Jadili dhana ya muktadha katika utunzi wa kazi za kifasihi.
3. "Fasihi ni zao la kisiasa". Jadili kauli hii kwa mifano thabiti.
4. Fafanua namna masuala ya kijamii yanavyochagiza utunzi wa kazi za kifasihi.
5. Jadili namna utunzi wa kazi za kifasihi unavyoweza kuchochewa na muktadha wa kiutamaduni.

**Shughuli 6.2**

Tumia maktaba na vyanzo vya mtandaoni, eleza fursa mbalimbali zinazotokana na kazi za kifasihi za Kiswahili.

## Fursa zinazotokana na kazi za kifasihi

Ubunaji wa kazi za kifasihi unatoa fursa nyingi ambazo humwezesha msanii binafsi, kikundi na mashirika kukuza kipato kutokana na mchakato wa kuhariri, kuchapisha, kusambaza, na kuuza kazi za kifasihi. Vilevile, uandishi wa kazi za

FOR ONLINE READING ONLY

fasihi husaidia kueneza utamaduni na sanaa ya jamii husika. Hivyo, kazi za fasihi huweza kutoa fursa mbalimbali ambazo huinua pato la mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Ufuatao ni baadhi ya ufafanuzi wa fursa hizo:

Fursa mojawapo ya kazi ya fasihi ya Kiswahili ni mwandishi wa vitabu vya mashairi, tamthiliya, hadithi/hadithi za watoto, riwaya na kazi nyingine za kiubunifu kujipatia kipato. Vitabu hivi huingizwa kwenye soko la vitabu ambapo huweza kununuliwa na kusomwa na watu mbalimbali ndani na nje ya nchi, ambapo mwandishi hujipatia kipato na kujikimu maisha yake. Vilevile kupitia fursa hii, mwandishi anaweza kupata umaarufu kutokana na kazi yake na ambapo anaweza kupata fursa ya kualikwa kwenye makongamano mbalimbali ya kiubunifu, jambo ambalo huweza kumsaidia kumwongezea uzoefu. Kadhalika, kazi bora za fasihi huweza kuingia katika ushindani wa tuzo mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Zinaposhinda, mwandishi hutunukiwa tuzo ambazo aghalabu huambatana na kipato.

Fursa nyingine ya mwandishi wa kazi za kifasihi ni kuuza nakala laini za kazi zake katika mitandao ya kijamii, hivyo kujipatia kipato. Mwandishi anaweza kuamua kufungua jukwaa la mtandaoni kwa ajili ya kurusha kazi mbalimbali za fasihi alizotunga. Pia, anaweza kuingia mikataba na wamiliki wa vituo vya runinga, redio na vyombo vingine vya habari na kupeleka kazi zake kwa ajili ya kusomwa, kutazamwa na kusikilizwa na jamii. Fursa zote hizi si kwamba humnufaisha mwandishi kwa kipato tu bali huweza kumpa umaarufu, hivyo watu kupenda kazi zake. Hali hii humhamasisha mwandishi kutunga kazi nyingi zaidi ambazo zitainua uchumi binafsi na wa kitaifa.

Kazi za kifasihi zinaweza kuchapishwa katika magazeti mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Mwandishi anaweza kuingia mikataba na wamiliki wa makampuni ya magazeti kwa ajili ya kuchapisha hadithi, riwaya, mashairi na kazi nyingine za kifasihi kwa ajili ya kusomwa na jamii. Uzuri wa kazi husika unaweza kusababisha kuwa na wafuasi wengi wa kazi hizo, suala linalomuwezesha mwandishi kujipatia kipato na umaarufu katika jamii. Kwa mfano, hadithi zilizoandikwa na Eric Shigongo zilipendwa na watu wa rika mbalimbali, kiasi cha kumwongezea kipato na kumpa umaarufu mkubwa.

Uandishi wa kifasihi unaweza pia kumwezesha mtu kuwa mtaalamu wa kuhariri makala na vitabu vya fasihi ya Kiswahili. Uandishi huo hutoa fursa kwa mhariri kuwa na nafasi ya kusoma na kuhariri kazi binafsi au za mwandishi mwingine. Hii husaidia kuboresha ubunifu, ubora wa lugha, muundo, maudhui na mtiririko mzuri wa andiko husika kabla ya kuchapwa. Hii ni fursa nzuri katika kuimarisha

na kuboresha stadi za uandishi. Vilevile, mhariri atakuwa na nafasi ya kushirikiana na wahariri wengine katika kuboresha kazi mbalimbali.

Aidha, kazi za fasihi hutoa fursa ya kukuza na kuendeleza sanaa. Hii ni kutokana na kuwepo kwa watu wenye vipaji na hata kujifunza kutoka kwa wengine kwa sababu ya kuangalia tamthiliya mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Fursa hii huwawezesha watu kuingia katika ulimwengu wa sanaa na kujipatia kipato. Fursa nyingine ya kisanaa ni kuwa mchoraji katika kazi mbalimbali za kifasihi, na vitabu vya watoto.

Fursa nyingine itokanayo na uandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili ni kuwa mwalimu wa kuifundisha fasihi hiyo. Mwalimu humwezesha mwanafunzi kujenga misingi ya fasihi ya Kiswahili na kuwahamasisha wanafunzi kupenda kujisomea kazi mbalimbali za fasihi. Kadhalika, kazi za fasihi hutoa fursa ya kuwa mwalimu wa kufundisha masuala ya uandishi wa kazi bunifu. Kazi hizo za kibunifu zinaweza kuwa za hadithi/hadithi za watoto, riwaya, tamthiliya, mashairi, na insha za kifasihi.

Kazi za fasihi humwezesha mtu kupata fursa ya kutafsiri vitabu vya fasihi. Tafsiri hizi huweza kuwa za vitabu vilivyoandikwa kwa lugha za Kiafrika na lugha za kigeni kwenda lugha ya Kiswahili na kinyume chake. Tafsiri hizo sharti zifanywe na mtu ambaye ana ujuzi wa kazi za fasihi ili kufumbata vionjo vya kifasihi katika lugha lengwa. Mfano wa vitabu vilivyotafsiriwa ni pamoja na tamthiliya za *Mabepari wa Venisi, Juliasi Kaizari, Mfalme Edipode* na *Nitaolewa Nikipenda;* na riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii.* Vitabu vilivyotafsiriwa huingia kwenye ushindani wa kibiashara, hivyo huingiza kipato kwa mtafsiri.

Utunzi wa kazi za kifasihi humwezesha mtunzi kuwa mtafiti wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Kupitia utafiti mtu hujijengea ujuzi wa mitindo mbalimbali ya uandishi wa kazi za kifasihi.

Kimsingi, kazi za fasihi ya Kiswahili hutoa fursa nyingi kwa jamii. Fursa hizo ni kama za uaimbaji, uchoraji, uhariri, ualimu/uhadhiri, utafiti na uigizaji. Kazi zote hutoa fursa za kujipatia kipato na kukuza uchumi binafsi na wa nchi.

**Shughuli ya 6.3**

Kwa kutumia majukwaa ya kidijiti kama vile *Instagram*, *WhatsApp* na *Youtube* eleza mchango wa TEHAMA katika kuongeza fursa za kutangaza na kuuza kazi za fasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Mchango wa TEHAMA katika kukuza fursa za utunzaji, usambazaji, usomaji na uuzaji wa kazi za fasihi

Matumizi ya TEHAMA yamechangia sana katika kutambua fursa mbalimbali zinazotokana na kazi za fasihi. Ufuatao ni mchango wa TEHAMA katika kutambua fursa hizo:

Mosi, TEHAMA ina mchango mkubwa katika kuchambua kazi za fasihi. Hii inatokana na matumizi ya programu mbalimbali kama vile *akili unde* ambayo hutumika katika kuchambua kazi za fasihi simulizi na andishi.

Pili, imewezesha uhifadhi na usambazaji wa kazi mbalimbali za kifasihi kwa urahisi na haraka kupitia mitandao ya kijamii. Kutokana na hilo, hadhira imekuwa ikitumia mitandao hiyo kusoma kazi hizo na kupata maarifa mbalimbali yanayohusiana na kazi za fasihi.

Tatu, imesaidia kukuza hali za kiuchumi za watunzi kutokana na baadhi ya kazi hizo kuwekwa mitandaoni na kuwataka wasomaji kuzilipia kabla ya kuzipakua ili kuzisoma au kuzisikiliza.

Nne, imechangia kukuza usomaji wa kazi za kifasihi kupitia vyanzo mbalimbali vya mtandaoni. Wasomaji hufungua programu mbalimbali ambazo huzisoma wakati wowote na mahali popote na kujipatia maarifa kutoka katika kazi za fasihi ya Kiswahili.

Tano, TEHAMA imerahisisha mawasiliano kwa sababu imewaunganisha waandishi kwa kutumia majukwaa mbalimbali ya mitandao katika utendaji wao. Majukwaa hayo ni kama vile, makundi ya *WhatsApp* na majukwaa mbalimbali ya majadiliano. Majukwaa haya yamewezesha waandishi hao kushirikiana katika kazi za uandishi na usambazaji wa kazi zao kwa urahisi.

Kwa ujumla, TEHAMA ina mchango mkubwa katika kuleta fursa mbalimbali kwenye fasihi ya Kiswahili kwa kutoa njia za utunzaji, usambazaji, usomaji na uingizaji wa kipato kwa watumiaji wa kazi za fasihi andishi.

**Shughuli ya 6.4**

Eleza jinsi TEHAMA inavyoweza kutoa fursa za kubidhaisha kazi ya kifasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la 6.2

1. Jadili hoja kwamba matumizi ya TEHAMA yana athari katika kazi za fasihi ya Kiswahili.
2. Jadili umuhimu wa kutumia majukwaa ya kidijiti katika kusambaza kazi za fasihi ya Kiswahili.
3. Kwa kutumia mifano, fafanua namna uigizaji unavyoweza kuwa fursa ya kukuza uchumi.
4. "TEHAMA haina mchango wowote katika kuchangia miktadha ya utunzi wa kazi za fasihi". Jadili.

**Shughuli ya 6.5**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni na maktabani, jadili hatua za utunzi wa kazi za kifasihi.

### Hatua za utunzi wa kazi za fasihi

Uandishi wa kazi za fasihi huongozwa na hatua mbalimbali ambazo hutegemeana na kukamilishana. Mtunzi wa maigizo, mashairi au hadithi za watoto hana budi kuzingatia hatua hizo ili aweze kuandika kazi yenye ubora na ushawishi. Uandishi wa kazi za fasihi unaweza kujumuishwa katika hatua kuu tano ambazo ni: maandalizi, uandishi/utungaji, uboreshaji, uhariri, na mapitio ya mwisho. Ufuatao ni ufafanuzi wa hatua hizi:

**(a) Kufanya maandalizi**

Katika hatua ya maandalizi, mwandishi anaweza kujiuliza maswali kadhaa kuhusu uandishi wake. Mifano ya maswali hayo ni: Ni jambo gani anataka kuandika? Kwa nini aandike kuhusu jambo hilo? Anamwandikia nani? Wapi atapata ukweli/uhakika kuhusu mambo anayotaka kuandika? Vifaa gani muhimu vinahitajika katika uandishi wake? Maswali haya yanadokeza mambo muhimu ambayo mwandishi anapaswa kuyafanya kabla ya mchakato mzima wa uandishi. Hivyo, katika hatua hii, mtunzi hupaswa kubuni wazo au mada ya uandishi, na kuanza kufanya uchunguzi kuhusu mada hiyo, na kuamua kuhusu utanzu wa

FOR ONLINE READING ONLY

kuandikia. Vilevile, mtunzi anapaswa kusoma kazi za utanzu husika, kuteua hadhira, kuandaa vifaa atakavyohitaji, na kuandaa ratiba ya kazi. Kisha, anatakiwa kuandika dondoo muhimu za kazi. Ufuatao ni ufafanuzi wa vipengele hivi

**(b) Kubuni wazo au mada**

Uandishi wa kazi ya fasihi hujengwa katika wazo kuu ambalo ndilo huchanuza mawazo madogomadogo ili kufikisha ujumbe kwa hadhira husika. Mtunzi wa kazi ya fasihi anapaswa kubuni wazo au mada itakayowavutia wasomaji na kuwapa hamasa ya kusoma kazi yake. Mada au wazo hilo linaweza kuwa la kufikirika, la kihistoria au mada inayohusu masuala muhimu ya kijamii. Mwandishi anaweza kupata wazo kutokana na uzoefu wake au mambo aliyoyapitia katika maisha na miktadha mingine. Vilevile, anaweza kufanya utafiti ili kuelewa masuala yanayogusa jamii yake, ambayo yatamsaidia kupata wazo la kuandikia. Mambo yanayoigusa jamii yanaweza kuwa ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na masuala mtambuka. Ni vizuri mwandishi abuni mada anayoipenda na atakayoimudu kuiandikia kazi yake.

**(c) Kufanya uchunguzi**

Baada ya kupata wazo au mada, mtunzi anaweza kukusanya taarifa anuai kuhusu wazo alilolipata. Anaweza kusoma vitabu, makala, au hata kufanya utafiti kuhusu wazo hilo. Lengo ni kupata maarifa ya kutosha na taarifa sahihi kuhusu wazo/ mada. Vilevile, uchunguzi humwezesha mtunzi kuelewa mazingira ya jamii, historia, utamaduni, na masuala mengine yanayohusiana na wazo au mada iliyochaguliwa.

**(d) Kuamua kuhusu utanzu wa kuandika**

Kila utanzu huwa na mtindo wake wa kiuandishi. Kwa hiyo, mtunzi anapaswa kuamua kuhusu utanzu atakaoutumia katika kuwasilisha wazo au mada aliyoibuni. Utanzu huo unaweza kuwa wa ushairi, tamthiliya, hadithi au riwaya. Hii itamsaidia kufikisha ujumbe wake kwa kuzingatia muundo na mtindo wa kiuandishi wa utanzu husika. Kwa mfano, ikiwa ni mashairi, mtunzi atapaswa kuzingatia kaida mbalimbali za ushairi kama vile: muundo, mtindo, lugha ya kishairi na mambo mengine yanayohusu ushairi. Ni vyema mwandishi akaandikia utanzu anaoumudu.

**(e) Kusoma kazi za utanzu husika**

Usomaji wa kazi husika za fasihi humpa mwandishi fursa ya kujifunza kutoka kwa waandishi wengine, ili kupata maarifa na kuimarisha stadi ya kuandika. Pia, humsaidia mtunzi kuwa na uelewa mzuri wa vipengele vya uandishi kama vile

FOR ONLINE READING ONLY

lugha, mtindo, na muundo unaotumiwa katika utanzu husika. Kufanya hivyo humwongezea mtunzi maarifa ya namna ya kuandika kazi yake.

**(f) Kuteua hadhira**

Mwandishi huandika kazi yake ili iweze kusomwa na jamii. Kwa mantiki hiyo, hana budi kujua aina ya watu anaowaandikia kazi husika. Mwandishi anatakiwa kujua mahitaji ya wasomaji wake, ikiwamo mitazamo yao kuhusu kile anachokiandikia. Kwa mfano, kama mwandishi anawaandikia watoto, anatakiwa kuandika kwa kutumia lugha nyepesi itakayowawezesha kuelewa maudhui hayo kwa urahisi. Aidha, anaweza kuweka picha au michoro yenye rangi mbalimbali ili kuwavutia watoto na kuwajengea kumbukumbu.

**(g) Kuandaa zana**

Katika hatua hii, mwandishi anaweza kubainisha vifaa na mahitaji mengine ambayo yatamsaidia kuandaa kazi husika, zikiwamo shajara, kompyuta na simu. Pia, mwandishi anaweza akaandaa ratiba ambayo itamwongoza katika mchakato wote wa kuandika kazi yake kulingana na utanzu anaouandikia.

**(h) Kuandika madondoo ya utunzi**

Mwandishi anapaswa kuandika dondoo kuhusu sehemu muhimu za kazi yake. Dondoo hizo, ambazo zitamwongoza katika uandishi wake, zinaweza kujumuisha vipengele vya: majina ya wahusika wakuu, majina ya wahusika wengine, mandhari, dhamira mbalimbali anazokusudia kuziwasilisha, mtindo wa uandishi na mpangilio wa visa na matukio.

**(i) Kuandika/kutunga**

Baada ya kufanya maandalizi ya uandishi, mwandishi anapaswa kuanza kuandika kazi yake kwa kuzingatia dondoo au mwongozo aliouandaa. Hapa ndipo anapoweka mawazo yake katika maandishi kwa kuumba wahusika, visa na matukio yanayosawiri wazo lake la ubunifu. Vilevile, katika hatua hii, mwandishi hapaswi kuhofia makosa yoyote ya lugha bali aruhusu mtiririko wa mawazo kwa mawanda mapana ili kukamilisha rasimu ya kwanza. Anatakiwa kupangilia mawazo vizuri ili kuleta mantiki katika visa na matukio. Mawazo au dhamira ndogondogo ni lazima zijengane na dhamira kuu. Aidha, mwandishi aepuke kujaza mawazo ambayo hayana tija katika kazi yake. Hii inamaanisha kwamba kila kinachoandikwa kiwe kinalenga kuiendeleza au kuikamilisha kazi. Kadhalika, ahakikishe anawaumba vizuri wahusika ili kusawiri migogoro. Aidha, atumie lugha ya kisanaa iliyojaa taswira, tamathali za usemi na mbinu nyingine za kifasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

### (j) Kuboresha

Baada ya rasimu ya kwanza kukamilika, mtunzi anatakiwa kupitia au kukagua kazi yake ili kufanya maboresho ya kiutungaji na kiubunifu. Mwandishi anaweza kurekebisha mpangilio wa visa na matukio na kuongeza au kupunguza mambo yanayojirudia na yasiyokuwa na maana, au hata kubadilisha muundo wa sehemu kadhaa za kazi yake. Vilevile, mtunzi anaweza kuwasuka upya wahusika ili kuendana na mwelekeo wa usimulizi na matumizi ya lugha ili kuifanya kazi ivutie na kuwa na kipekee. Pia, katika mchakato huu mwandishi anaweza kuboresha miundo ya sentensi kwa kuondoa maelezo yasiyo ya lazima ili kuweka urahisi wa kueleweka kwa wasomaji. Kwa hiyo, ni muhimu mwandishi kupitia kazi yake mara baada ya uandishi ili kuhakikisha kazi ina mtiririko wenye mantiki, usahihi wa taarifa, ushikamani wa kiusimulizi na ufikishaji wa ujumbe uliokusudiwa.

### (k) Kuhariri

Hii ni hatua muhimu katika mchakato wa uandishi wa kazi za kifasihi. Katika hatua hii, mwandishi anang'arisha na kuboresha maandishi ya kazi yake ili kuifanya iwe sahihi na inayoeleweka kwa wasomaji. Hivyo, mtunzi hupaswa kuhariri kazi yake kwa kuondoa makosa ya kiuandishi, kiuakifishaji na kimsamiati kama vile sarufi, miundo ya sentensi na matumizi sahihi ya maneno. Vilevile, mwandishi huweza kuhariri kazi yake kwa kuweka mtiririko mzuri wa uwasilishaji wa matukio, mawazo na hisia ili kuifanya kazi ivutie zaidi. Mtunzi yupo huru kumpa mtu mwingine ili ahariri kazi yake, hususani mtaalamu aliyebobea kwenye utanzu husika na baadaye mhariri wa lugha. Hata hivyo, ingawa mchakato huu ni muhimu ni vyema kuhakikisha kuwa uhariri hauharibu ubunifu na mtindo wa lugha wa mwandishi.

### (l) Kupitia kwa mara mwisho

Hii ni hatua ya mwisho katika uandishi, ambapo mwandishi huisoma upya kazi yake ili kuchunguza na kurekebisha makosa madogomadogo kama vile tahajia na sarufi. Lengo la usomaji huu ni kuhakikisha kazi inazingatia ubora, usahihi na ufasaha. Baada ya hatua hii, kazi itakuwa imekamilika. Hivyo, inaweza kuendelea na hatua za uchapishaji kutegemeana na malengo ya mwandishi.

**Shughuli ya 6.6**

Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni, maktabani au vinginevyo, jadili umuhimu wa kufuata hatua za uandishi wa kazi ya fasihi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 6.3**

1. Jadili kauli kuwa "uandishi wa kazi za kifasihi ni mchakato usiohitaji utaratibu".
2. "Maandalizi ni hatua muhimu kabla ya uandishi wa kazi ya fasihi". Jadili.
3. Kwa kutumia mifano eleza masuala muhimu ambayo hufanyika katika hatua ya kuboresha.
4. Tofautisha hatua ya uhariri na ya mapitio ya mwisho katika utunzi wa kazi za kifasihi.
5. "Mapitio ya mwisho ni hatua inayompotezea muda mwandishi." Jadili.

**Shughuli ya 6.7**

(a) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni, maktabani na vinginevyo, eleza maana na kanuni zinazoongoza utunzi wa maigizo.

(b) Angalia au sikiliza maigizo kutoka katika vyanzo mbalimbali, kisha chambua kanuni zilizotumika katika utunzi wa igizo mojawapo.

## Kanuni za kutunga maigizo, mashairi na hadithi za watoto

Utunzi wa kazi yoyote ya kifasihi huongozwa na kanuni maalumu ambazo hutumika katika kutunga kazi za utanzu husika. Ufuatao ni ufafanuzi wa kanuni za kutunga maigizo, mashairi na hadithi za watoto.

### Kanuni za kutunga maigizo

Maigizo ni kipera cha sanaa za maonesho ambacho ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi. Maigizo ni sanaa ya kuwasilisha jambo au tukio kwa kutumia lugha na vitendo. Mara nyingi maigizo hutendwa kwenye jukwaa la maonesho au mahali popote maalumu mbele ya hadhira husika. Maigizo yanahitaji kutungwa kwa ustadi ili kuwakonga watazamaji. Hatua za utunzi wa maigizo kwa kiasi kikubwa zinafanana na zile za utunzi wa kazi nyingine za kifasihi isipokuwa utunzi wa maigizo hujumuisha vipengele muhimu vinavyopatikana katika maigizo tu. Kanuni muhimu za kuzingatiwa katika utunzi wa maigizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

FOR ONLINE READING ONLY

**(a) Wazo au mgogoro**

Igizo lolote, kama kazi yoyote ya sanaa, lazima liwe na wazo au mgogoro unaovutia au wenye uzito. Mgogoro ni tatizo ambalo linahitaji utatuzi.

**(b) Msuko wa matukio au matendo**

Hatua ya pili ya utunzi wa igizo ni uteuzi wa matukio yaliyopangiliwa katika mfuatano wa usababishano – tukio moja likisababisha jingine, toka mwanzo hadi mwisho. Msuko wa matukio unapaswa kuibua msisimko na taharuki kwa wasikilizaji na watazamaji. Matukio haya huteuliwa na mtunzi lakini yanaweza kubadilishwa katika uigizaji jukwaani.

**(c) Matumizi ya dayalojia**

Mazungumzo katika maigizo hayaandikwi, bali huibuka kulingana na makubaliano baina ya waigizaji, na kufuata matukio yaliyopangwa.

**(d) Wahusika**

Wahusika katika maigizo wanatakiwa kuumbwa kwa kuzingatia mahitaji ya vitendo husika. Wanatakiwa kuvutia, wawe wa kipekee na wauvae uhusika vizuri ili kufanya uigizaji kuwa hai na kuhamasisha hisia kwa hadhira. Majukumu ya wahusika yanatakiwa kuwa wazi na yanayoendana na dhamira ya igizo. Wahusika kinzani huongeza msisimko na mvuto katika maigizo kwa sababu huchochea migogoro, na migogoro ndiyo inayosukuma simulizi.

**(e) Mandhari**

Ijapokuwa mandhari ya igizo yanapaswa kuwa ya kuaminika na yenye uhalisi ili kuendana na tukio, kuna maigizo yenye mandhari za kufikirika. Kwa jumla, mandhari ya igizo inayovutia na iliyoundwa na mazingira ya kipekee, hufanya simulizi ya igizo kuwa na nguvu ya ushawishi zaidi.

**(f) Kugusa hisia za hadhira**

Kazi ya maigizo ikisukwa vizuri huibua hisia na misisimko ya aina nyingine kwa hadhira husika. Mwandishi anayegusa hisia za hadhira ndiye husemwa kuwa kafanikiwa sana katika utunzi wake.

Ikumbukwe kuwa utunzi wa maigizo si wakuandika bali ni wa kuzungumza na kutenda wazo kwa mujibu wa mfuatano mahususi wa matukio. Maigizo hayasomwi bali husikilizwa na kutazamwa.

**Shughuli ya 6.8**

Chagua suala moja mtambuka, kisha tunga igizo kwa kuzingatia kanuni za utunzi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli 6.9**

Tumia vyanzo vya mtandaoni, maktabani au vinginevyo, kueleza kanuni zinazoongoza utunzi wa shairi.

**Kanuni za kutunga mashairi**

Mashairi huwa na sifa za kipekee ambazo huyafanya kutofautiana na tanzu nyingine za fasihi. Kwa mantiki hiyo, kuna mambo muhimu ambayo hayana budi kuzingatiwa wakati wa utunzi wa mashairi. Mambo hayo ni lugha ya kishairi, muundo, muwala, taswira na ishara, mtindo na utoshelevu.

**(a) Lugha ya kishairi**

Mashairi hutumia lugha ya mkato na kibunifu kama vile matumizi ya uwekevu, tamathali za semi, misemo na nahau. Mwandishi anatakiwa kuzingatia vipengele hivi ili kuleta mvuto wa shairi lake. Katika uandishi wa shairi, mtunzi ana uhuru wa kukiuka kanuni za kisarufi ili kukidhi mahitaji ya ushairi.

**(b) Muundo**

Muundo wa mashairi unatofautiana na muundo wa matini nyingine za kifasihi kwa sababu ya vipengele mbalimbali kama vile beti, mistari, mizani na miundo mingine kulingana na aina ya shairi. Mwandishi hana budi kuandika shairi lenye muundo unaosadifu mahitaji ya shairi lake; na kwa njia hii anaweza kuibua muundo mpya tofauti na ile iliyozoeleka. Katika ushairi wa Kiswahili, miundo iliyozoeleka ni ile ya kimapokeo na ya kisasa.

**(c) Muwala**

Mtunzi hana budi kuzingatia kipengele cha muwala ambacho hushughulikia uwiano mzuri wa sehemu zote za shairi. Muwala huweza kupatikana kupitia uzingatiaji wa mtiririko wa fikra katika umbo mahsusi la shairi ambao husaidia kujenga mantiki ili kuwasilisha maudhui yaliyokusudiwa. Ushikamani wa kifikra hutokea baina ya mshororo na mshororo, ubeti na ubeti, na hatimaye, shairi zima.

**(d) Taswira na ishara**

Mtunzi wa shairi haelezi mambo moja kwa moja bali huyafumbata anayotaka kuyaeleza ndani ya taswira na picha zinazotumia ishara. Matumizi haya huathiri hisia za wasomaji kama vile za upendo, huzuni, furaha, na hasira. Mbinu hii ya matumizi mazuri ya lugha ya picha na ishara humfikirisha msomaji wa shairi kwa kumfanya azifasili taswira na ishara hizo ili kupata maana iliyokusudiwa.

**(e) Mtindo**

Mshairi huwa na uwanja mpana wa kutumia mitindo mbalimbali kiuandishi. Anaweza kutumia mtindo wa kimapokeo unaofuata kanuni za urari wa vina na mizani au wa kisasa unaokiuka kaida na kanuni hizo.

FOR ONLINE READING ONLY

**(f) Utoshelevu**

Ni muhimu shairi liwe na mtiririko mzuri wa mawazo unaolandana na mpangilio wake. Mpangilio huo ndio unaoleta utoshelevu. Utoshelevu ni kanuni ambayo inautaka kila mshororo na kila ubeti kujitosheleza kimaana ili kulifanya shairi likamilike kifani na kimaudhui.

**Shughuli 6.10**

(a) Soma mashairi mawili kutoka katika diwani teule kisha chambua kanuni zilizotumika katika utunzi wake.

(b) Chagua mada unazozipenda kisha tunga mashairi mawili yasiyopungua beti kumi (10) kwa kila shairi.

**Shughuli ya 6.11**

(a) Chunguza vitabu teule vya hadithi za watoto, kisha eleza maana na sifa za hadithi hizo.

(b) Kwa kutumia vyanzo vya mtandaoni, maktabani au kwingineko, jadili kanuni za utunzi wa hadithi za watoto.

**Kanuni za kutunga hadithi za watoto**

Hadithi za watoto ni aina ya kazi za fasihi zilizobuniwa kwa ajili ya watoto. Visa na matukio, lugha, wahusika, michoro na picha, na maudhui yanayowasilishwa katika hadithi za watoto huakisi hisia na akili za watoto. Hadithi hizi huwa na sifa ambazo ni tofauti na hadithi za watu wazima ama hadithi nyingine. Hadithi za watoto huweza kuwa na maandishi yenye ukubwa tofauti kulingana na umri wa watoto, utofauti wa nafasi kati ya mstari na mstari, nakshi ya rangi, picha na michoro, kurasa chache, lugha rahisi na wahusika wachache kulingana na umri wa watoto.

Licha ya upekee wa hadithi za watoto lakini hatua za uandishi huwa ni sawa na za kazi nyingine za kifasihi. Vilevile, vipengele vinavyojenga hadithi za watoto, kama vile, lugha, wahusika, msuko wa visa na matukio huwa sawa na kazi bunilizi nyinginezo kama vile hadithi fupi na riwaya. Pamoja na mfanano huo, utunzi wa hadithi za watoto huongozwa na kanuni zifuatazo:

**(a) Lugha**

Hadithi za watoto hutumia lugha rahisi, inayoeleweka na ya kisanaa. Sanaa katika lugha ya watoto hujumuisha semi, tamathali za semi na methali kulingana

FOR ONLINE READING ONLY

na umri wao. Urahisi huo hutokana na sentensi kuwa fupi na uteuzi wa msamiati unaoendana na kiwango chao. Vilevile, inashauriwa mwandishi wa hadithi arudierudie maneno, sentensi na vifungu vya maneno ili kumsaidia mtoto kuelewa suala linalowasilishwa. Hata hivyo, lugha inayotumika huweza kutofautiana kutokana na rika, umri na ngazi ya usomaji, kama vile ngazi ya awali, shule za msingi na vijalunga chini ya miaka 18.

**(b) Wahusika**

Mara nyingi, wahusika ni watoto au wale wanaoakisi matendo ya rika lengwa, yaani watendao au kuzungumza kitoto. Majina ya wahusika yasifanane wala yasikaribiane ili kutokuwachanganya watoto. Kwa mfano si vizuri kwenye kazi moja kutumia majina kama Avita na Avera, Paula na Paulo; Samiri, Samira na Samri; au Petro, Petronia, na Petrobasi. Vilevile, ni vyema mhusika abainishwe wazi kwa kuzingatia umbo, sifa, rangi, mavazi na tabia zake.

**(c) Msuko wa visa na matukio**

Hadithi za watoto hujengwa kwa msuko rahisi na wa moja kwa moja ambapo kisa huwa na chanzo, kati na mwisho. Kwa mfano, mhusika anatambulishwa akiwa anazaliwa, anasoma shule, mwisho anapata kazi. Vilevile, matukio yawe na taharuki ili kuwavutia watoto kutamani kuendelea kusoma hadithi.

**(d) Picha na michoro**

Hadithi za watoto huwa na picha na michoro mingi kwa ajili ya kufafanua zaidi maelezo, kuibua hisia, kurahisisha uelewa wa tukio linalowasilishwa, kujenga kumbukumbu, kuongeza ubunifu na kuvutia watoto. Picha hizo huweza kupambwa kwa rangi mbalimbali kutegemeana na maudhui na rika husika.

**(e) Mandhari halisi**

Mara nyingi, hadithi za watoto zinapaswa kusawiri miktadha ya kijamii au kitamaduni inayowafaa watoto. Vilevile, mandhari za hadithi za watoto zibainishwe wazi, zisiwe za kuwakatisha watoto tamaa ya kusoma suala linaloweza kuwafanya washindwe kuendelea kuisoma hadithi. Inashauriwa katika hadithi za watoto wadogo, rika la awali na kati, zitumike mandhari halisi.

**(f) Taswira**

Hadithi za watoto ziwe zinafikirisha na kuwajengea hisia na picha mbalimbali akilini mwao ili kuwachangamsha. Taswira hujengwa kwa kutumia lugha ya picha, tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa zinazohusiana na umri wao.

FOR ONLINE READING ONLY

**(g) Taharuki**

Hadithi za watoto hutumia taharuki ili kumtamanisha mtoto kufahamu tukio linalofuata, kujua zaidi kuhusu matokeo ya mgogoro unaoendelea na kumfanya adadisi zaidi kuhusu mtiririko wa hadithi hiyo. Mfano mzuri wa uundaji wa taharuki ni pale mhusika anapokuwa katika tukio la hatari ambalo mtoto hajui hatima yake. Kwa hiyo, hutamani kusoma zaidi ili ajue mustakabali wake.

**(h) Fantasia**

Hadithi za watoto hutumia matukio, matendo na vitu visivyo vya kawaida, dhana halisi na zile zenye maajabu ili kujenga taharuki na kuibua dhamira mbalimbali. Mfano wa hadithi hizi ni pamoja na *Marimba ya Majaliwa* (Semzaba, 2008)

**(i) Usimulizi**

Usimulizi ni uwasilishaji wa kimfuatano wa matukio katika kazi ya fasihi kama vile mashairi, tamthiliya, riwaya, hadithi fupi. Katika kazi nyingi za fasihi, usimulizi wake ni wa nafsi ya kwanza au ya tatu. Vilevile, upo usimuliaji wa nafsi ya pili. Katika tamthiliya, usimulzi hujitokeza katika mchanganyiko wa maelekezo ya jukwaa na mazungumzo baina ya wahusika au hata mandhari au muonekano wa wahusika.

**(j) Dhamira zenye mafunzo chanya**

Hadithi za watoto hupaswa kuwa na maudhui ya kuburudisha na yenye mafunzo yanayowafaa. Kama ilivyo kawaida, dhamira huwa hazibainishwi wazi bali msomaji hujenga maana kutokana na kile kinachosimuliwa. Hivyo, mtoto anatakiwa kujengewa dhamira rahisi na kadri anavyokua ajengewe dhamira za kufikirisha. Dhamira za watoto huweza kujengwa kwa kumfanya mtoto kutambua vitu na mazingira, urafiki, mahusiano ya kifamilia, makuzi bora na kukabiliana na hali tofauti za maisha.

**Shughuli ya 6.12**

Chagua mada moja kati ya zifuatazo, kisha tunga hadithi ya watoto kulingana umri utakaochagua.

**Mada za uandishi**

(i) Safari ya ajabu

(ii) Maisha ya shule

(iii) Msitu wa ajabu

(iv) Watoto wa mtaani

(v) Mwanga wa elimu

FOR ONLINE READING ONLY

(vi) Mkulima shujaa

(vii) Marafiki

(viii) Haki za watoto

(ix) Ndoto ya ajabu

## Tamrini

1. Tofautisha kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi.
2. Kwa kutumia mifano, fafanua miktadha inayoweza kuchochea uandishi wa kazi za kifasihi.
3. Jadili dai kwamba uandishi wa kazi za fasihi hauna faida yoyote
4. "TEHAMA haina mchango wowote katika kupata fursa za uandishi wa kazi za fasihi." Jadili.
5. Kwa kutumia mifano, eleza kanuni za utunzi wa maigizo.
6. Fafanua hatua za kuzingatia wakati wa uandishi wa mashairi
7. Tunga mashairi mawili ya kimapokeo na mawili ya kisasa.
8. Buni mada mbili unazozipenda kisha andika hadithi za watoto kwa kuzingatia umri na kanuni za uandishi.
9. Chagua maada mojawapo mtambuka kati ya hizi zifuatazo, kisha tunga shairi kwa kuzingatia kanuni za utunzi.
   (c) ndoa za utotoni
   (d) mimba za utotoni
   (e) rushwa
   (f) muungano
   (g) haki za watoto
   (h) dawa za kulevya

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazimradi

Chagua mada yoyote ya kifasihi kisha andaa kazimradi na andika ripoti.

## Faharasa

**Akili mnemba:** Mfumo wa kidijiti ambao umetengenezwa kwa ajili ya kutoa majibu ya masuala mbalimbali

**Buni:** Gugundua au tengeneza kitu kwa mara ya kwanza

**Falsafa** Elimu kuhusu asili, maana na sababu za mambo au vitu

**Fani:** Ufundi anaoutumia msanii katika kuwasilisha maudhui

**Fantasia:** Wazo la kufikirika lisiloweza kutekelezeka

**Fumbo:** Usemi au kauli ambayo maana yake haitolewi waziwazi bali hufichwa

**Fursa:** Nafasi ya kuweza kufanya jambo

**Futuhi:** Aina ya tamthiliya inayokusudia kufurahisha au kuchekesha, na huwa na mwisho mwema (Pia, ramsa)

**Hadithi fupi:** Simulizi ya kubuni inayosawiri tukio, tabia, mgogoro au kipengele fulani cha maisha kwa ufupi, kwa kawaida, hadithi fupi huwa na tukio moja au mawili na hutumia mawanda finyu

**Hadithi za watoto:** Tungo za kibunifu zinazowahusu watoto kifani na kimaudhui

**Hadithi:** Matukio yanayosimuliwa kwa mfuatano wa kimantiki na kiwakati

**Hekaya:** Ngano zenye visa visivyo vya kawaida vinavyoambatana na masaibu na pengine hata ujanja wa mhusika mkuu ambaye huweza kuwa mtu au mnyama

**Hurafa:** Ngano zenye wahusika wanyama tu ambao huwakilisha tabia na matendo ya binadamu kwa kurejelea masuala yanayopatikana katika jamii ili kuwasilisha maana

**Insha:** Utungo mfupi wa kinathari (wa lugha ya mjazo) ambao husimulia jambo kwa utimilifu

**Istiara:** Hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana iliyofichika. Kwa hiyo, maana huwasilishwa kwa njia ya mafumbo.

**Itikadi:** Jumla ya mfumo wa mawazo, fikra au imani inayoongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha masuala mbalimbali

**Jukwaa:** Eneo maalumu lililotengenezwa kwa kuinuliwa juu ndani ya jingo, ukumbi au uwanja ambalo hutumika kwa kutolea hotuba au michezo

FOR ONLINE READING ONLY

**Kigano:** Hadithi fupi ya fasihi simulizi ambayo hutolewa kwa kutumia matumizi mapana ya ujadi

**Kipera:** Tawi la utanzu wa fasihi

**Kisa:** Masimulizi ya tukio la kweli lililotokea

**Kisasili:** Hadithi inayoaminiwa kuwa kweli, inayoelezea chimbuko au asili ya kitu na hufungamana na imani na miviga ya jamii

**Kisasuli:** Hadithi yenye kueleza usuli na sababu za jambo, tukio au hali (yaani kwa nini jambo, tukio au hali iko kama ilivyo). Kisasuli hakina uzito mkubwa kama kisasili, na si lazima kiaminiwe na wanajamii.

**Kitendawili:** Usemi mfupi wa mafumbo wenye kutumia lugha ya picha, tamathali na ishara katika kueleza jambo lililofichika

**Lakabu:** Jina au majina ya nyongeza au ya kupanga (ambayo sio halisi) ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipa kutokana na sifa zao za kimaumbile, kinasaba, kitabia, kiujuzi au kimatendo

**Lugha:** Njia ya mawasiliano ya kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Mfano: lugha ya maandishi, lugha ya masimulizi, lugha ya ishara, lugha ya alama na lugha ya vitendo

**Maghani:** Tungo za kishairi zinazotongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji

**Maigizo:** Sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuelimisha au kuburudisha

**Majazi:** Tamathali ya usemi ambayo wahusika wa kazi ya fasihi hupewa majina yanayoakisi wasifu au tabia zao

**Majigambo:** Masimulizi ya kujisifia au kujikweza kwa mtu kuhusu mambo anayoweza kuyafanya, aliyowahi kuyafanya au atakayoyafanya

**Makala:** Habari iliyoandikwa kueleza jambo mahususi kwenye gazeti, jarida au kitabu

**Maktaba:** Mkusanyo wa machapisho kama vitabu, kanda, yaliyohifadhiwa na ambayo huweza kuazimwa na kutumiwa

**Maleba:** Mavazi, vifaa na mapambo ya msanii anapokuwa jukwaani

**Mandhari:** Muonekano wa mahali unaojumuisha ardhi, miti, mito, milima au mabonde

**Maudhui:** Jumla ya mambo mbalimbali yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi ambayo yanajengwa na dhamira, mtazamo, falsafa, itikadi, msimamo, ujumbe, mafunzo na migogoro

FOR ONLINE READING ONLY

**Mdokezo:** Tamathali ambayo kitu fulani hudokezwa au huachwa bila kukamilishwa, aghalabu, kitu hicho huwa kinafahamika katika muktadha husika

**Methali:** Semi za kimapokeo zenye hekima na busara zinazotumia sitiari kuelezea falsafa na uzoefu wa jamii fulani kwa muhtasari

**Mgogoro:** Ni hali ya watu kukosa kukubaliana kuhusu suala fulani inayoweza kusababisha mitafaruku

**Mhadhiri:** Mtaalamu au mwalimu wa taasisi ya elimu ya juu anayeelimisha watu kwa njia ya mhadhara

**Mhusika Bapa:** Mhusika ambaye habadiliki kulingana na wakati, mazingira au muktadha; yaani huonesha upande mmoja tu

**Mila:** Ni taratibu za kimaisha za mwenendo na jinsi ya kufanya mambo zinzofuatwa na jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wao

**Misingi:** Chanzo au chimbuko la kitu fulani

**Mitandao ya kijamii:** Programu inayowezesha watu kuwasiliana kwa njia ya tovuti au mfumo mwingine wa mawasiliano ya kielekitroniki

**Miviga:** Sherehe au shughuli za kijadi zinazofanywa na jamii katika kipindi maalumu cha mwaka au katika muktadha maalumu

**Mkondoni:** Kuwa katika hali ya kuunganishwa na mtandao kupitia kompyuta au vyombo vingine kidijiti

**Mleo:** mstari wa tatu wa shairi la beti za mistari mitatumitatu

**Mloto:** mstari wa pili katika ubeti wa shairi

**Mtandao:** Mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki unaopitia katika kompyuta ulimwenguni unaotumiwa kutafuta taarifa kuwasiliana au kupeana taarifa

**Mtazamo:** Namna au jinsi mtu anavyochukulia kitu au jambo kisiasa au kiuchumi

**Mtindo:** Kipengele cha kifani kinachohusu upekee au utofauti wa msanii unaojitokeza katika kazi ya fasihi na hutokana na matumizi ya lugha na vielelezo. Mtindo humtofautisha msanii mmoja na mwingine katika kazi moja na nyingine

**Muundo:** Kipengele cha kifani kinachohusu umbo au mwonekano wa kazi ya sanaa

**Mwandamizi:** Kipande au mgao wa tatu katika mshororo wa shairi ambalo mishororo yake imegawanyika katika vipande vitatu

FOR ONLINE READING ONLY

**Nahau:** Misemo ya picha ambayo huwa na maana iliyofichika. Kwa kawaida, huundwa na kitenzi na nomino

**Nathari:** Utungo unaotumia lugha ya mjazo

**Ngano:** Hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea na kuonya kuhusu maisha. Maudhui yake hujikita katika maadili, mahusiano na mwenendo ndani ya jamii

**Ngoma:** Kipera cha sanaa za maonesho za jadi ambacho huhusisha uchezeshaji wa viungo vya mwili wenye mtindo na miondoko maalumu inayoambatana na muziki. Pia ni kifaa cha muziki kilichowambwa kwa ngozi

**Ngomezi:** Fasihi itumiayo midundo ya ngoma ili kuwasilisha ujumbe

**Ngonjera:** Mazungumzo au majibizano ya kishairi ya kusemwa yanayohusu mada fulani

**Programu:** Mfumo wa kompyuta ulioandaliwa kwa ajili ya kutenda kazi fulani kama vile kutengeza vitabu, kupeleka au kupokea baruapepe

**Ramsa:** Aina ya tamthiliya inayokusudia kufurahisha au kuchekesha, na huwa na mwisho mwema

**Riwaya:** Hadithi ndefu ya kubuni itumiayo lugha ya kinathari (lugha ya mjazo) na yenye uchangamani wa visa, wahusika, mandhari na dhamira

**Sanaa:** Ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro, uchongaji, ufumaji na kadhalika

**Sanifu:** Weka taratibu za lugha zenye kufuata kanuni zinazokubalika

**Shairi:** Utungo wenye mishororo au mistari iliyogawanywa kwenye mafungu kadhaa unaoeleza au kuonesha kwa ufupi wazo au jambo au hisia fulani kuhusu binadamu na mazingira yake kwa lugha ya picha na mkato

**Sitiari:** Tamathali ya usemi inayotumika kuonesha ulinganishi wa vitu au hali tofauti bila ya kutumia maneno ya ulinganishi

**Soga:** Hadithi fupifupi za utani na ucheshi

**Sokrate:** Mwanafalsafa wa Kiyunani aliyeishi 469 - 399 K.K

**Taashira:** Tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumika kuwakilisha kitu kamili

**Tabaini:** Tamathali za semi inayosisitiza jambo kwa kutumia maneno au kauli kinzani

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| **Tafsiri:** | Ni uhawirishaji wa mawazo yaliyoandikwa kutoka lugha moja hadi nyingine |
| **Tahakiki:** | Andiko linalochambua na kufafanua kazi fulani ya fasihi |
| **Taharuki:** | Hali ya kusisimua au wasiwasi kuhusu jambo fulani litakalotokea katika kipindi kijacho |
| **Takhmisa:** | Shairi lenye mistari mitano |
| **Takriri:** | Dhana inayotumika kuelezea hali ya kurudiarudia sauti, silabi, neno au maneno |
| **Tamthiliya:** | Mchezo ulioandaliwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani |
| **Tanakali lafudhi:** | Tamathali inayotumika kuonesha mwigo wa matamshi ya watu fulani wanaotumia lugha kwa namna fulani |
| **Tanakali sauti:** | Tamathali inayotumika kuonesha mwigo wa sauti za vitu mbalimbali kulingana na lengo na muktadha husika |
| **Taniaba:** | Tamathali ambayo hutumia jina la mtu binafsi kwa watu wengine wenye tabia, mwenendo hali au kazi sawa na ya mtu huyo |
| **Tarbia:** | Shairi la kimapokeo lenye mistari minne |
| **Tarihi:** | Hadithi zinazohusu matukio muhimu ya kihistoria |
| **Tasdisa/Sudusia:** | Shairi lenye mistari sita |
| **Tashibiha:** | Tamathali inayotumika kuelezea hali ya ulinganishi kwa kutumia maneno ya ulinganishi kama vile kama, mithili ya, mfano wa, na sawa na |
| **Tashihisi:** | Tamathali ambayo vitu visivyo na uhai na uwezo wa kutenda hupewa uwezo huo |
| **Tafsida:** | Lugha ya staha yenye lengo la kupunguza ukali au matusi katika kauli |
| **Taswira:** | Picha au jazanda inayojengwa akilini mwa hadhira anapoifuatilia kazi ya sanaa |
| **Tathlitha:** | Shairi lenye mistari mitatu |
| **Tini:** | Muhtasari wa kumbukumbu za hoja au mawazo zinazoandikwa kwa ajili ya kusomwa baadaye |
| **Ubunifu:** | Uwezo wa kutafakari na kujenga fikra zinazounda na kufanya kitu au jambo jipya lionekane |
| **Uhakiki:** | Dhana inayohusika na kuchambua, kufafanua, kufasili, kutathmini, na kueleza vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi |

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| **Uhariri:** | Kazi ya kusoma, kusahihisha na kusanifu miswada kama vile makala au vitabu |
| **Uigizaji:** | Tendo la kuchukua vitu kutoka nje na kuviingiza ndani ya sehemu au eneo lenu jukwaa |
| **Ujumi:** | tathmini inayobainisha ubora au ubaya wa kazi za kisanaa |
| **Ujuzi:** | Ufundi au utaalamu au maarifa alionayo mtu katika kufanya shughuli fulani |
| **Uketo/ utao:** | Kipande cha pili katika mshororo |
| **Ukwapi:** | Kipande cha kwanza katika mshororo |
| **Umahiri:** | Ni ujuzi mkubwa wa kufanya jambo fulani |
| **Upeo:** | Ni mstari wa mwisho katika ubeti wa shairi |
| **Usawiri:** | kutoa sura halisi ya kitu |
| **Ushairi:** | Utanzu wa fasihi ambao hutumia sauti zilizopangiliwa, mizani, lugha ya mkato, lugha ya mafumbo na uimbaji au ughani ili kuwasilisha kwa hadhira maudhui yaliyokusudiwa |
| **Utafiti:** | Uchunguzi wa kitaalamu wa jambo kwa kukusanya data na kuzichambua ili kupata ukweli wa jambo fulani |
| **Utamaduni:** | Mfumo wa maisha wa jamii fulani unaojumuisha mila, jadi, desturi na sanaa za kundi la jamii fulani |
| **Utanzu:** | Kundi linalojumuisha kazi mbalimbali za sanaa zenye kuchangia sifa fulani kuu |
| **Utendi:** | Utungo mrefu wa kishairi unaozungumzia kwa mapana matendo ya kihistoria ya shujaa |
| **Utenzi:** | Utungo mrefu wa kishairi unaohusu mawaidha au masuala mengine ya kijamii |
| **Utomeleaji:** | uchopekaji wa kipengele cha kipera fulani kwenye utanzu tofauti. Mfano kipera cha nyimbo kikitumika kwenye riwaya au hadithi fupi |
| **Utunzi:** | Utungaji wa kazi yoyote ya kifasihi |
| **Wimbo:** | Utungo wa kimuziki unaowasilishwa kwa kuimbwa na huzingatia mahadhi maalum |
| **Zana:** | Kitu ambacho mtu hukitumia kufanyia shughuli fulani |

FOR ONLINE READING ONLY

## Bibliografia


Abdulla, M. (1973). *Siri ya Sifuri.* East African Publishers.

Abdulla, M. (1968). *Duniani kuna watu.* East African Publishers.

Abdulla, M. (1968). *Kisima cha Giningi.* Evans Brothers.

Abdulla, M. (1976). *Mwana wa Yungi hulewa.* Heinemann publishers.

Abdulla, M. (1984). *Kosa la Bwana Msa.* East African Publishing House.

Abedi, K. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri.* East African Literature Bureau.

Bâ, M. (2009). *Barua ndefu kama hii.* Mkuki na Nyota.

Baharoon, Z. (2021). *Mungu hakopeshwi.* Mkuki na Nyota.

Balisidya, M. (1975). *Shida.* East African Literature Bureau.

Balisidya, M. (1987). "Tanzu na fani za fasihi simulizi." *Mulika* namba. 19 uk. 2 - 10.

Banzi, A. (1970). *Tamaa mbele.* Tanzania Publishing House.

Banzi, A. (1972). *Titi la mkwe*: Tanzania Publishing House.

Brenn, E. (1929) *Alfu Lela Ulela* ([F. Johnson na E. Brenn). Longmans.

Brenn, E.W., & Johnson, F. (1921). *Mwaka katika mnyororo.* The Sheldon Press.

Bunyan, J. (1925). *Hadithi za Esopo* (D. Diva, Mf.). Longmans.

Bunyan, J. (1925). *Safari ya msafiri.* Society for the Promotion of Christian Knowledge.

Chachage, S. (1981), *Kivuli.* BCI Publishers.

Chachage, S. (1991). *Almasi za bandia.* E&D.

Chachage, S. (2002). *Makuadi wa soko huria.* E&D.

Chachage. S. (1981). *Sudi ya Yohana.* DUP.

Diva, D.E. (1949). *Msafiri katika nyumba ya Sultani.* Gospel Publishers.

Diva, D.E. [Mf.] (1937-42) *Hadithi za Esopo I-III.* Sheldon Press.


FOR ONLINE READING ONLY

el Ajjemi, A. (1985, 1907). *Habari za Wakilindi*. East African Literature Bureau.

Farsy. M.S. (1960). *Kurwa na Doto*. EALB.

Ganzel, E. (1980). *Kijasho Chembamba.* Tamasha Publications.

Habwe, J. (2010). *Mizungu ya manabii na hadithi nyingine*. Phoenix.

Haggard, R. (1929). *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (E. Brenn, Mf.). Longmans.

Hancha, A.S. (2015). *Sibanduki Afrika*. Hancha Books.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Heinemann.

Hussein, E. (1967). *Wakati ukuta*. EAPH.

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Oxford University Press.

Hussein, E. (1976). *Jogoo kijijini na ngao ya jadi*. OUP.

Hussein, E. (1980). *Arusi*. Oxford University Press.

Hussein, E. (1988). *Kwenye ukingo wa Thim*. Oxford University Press.

Hyslop, G. (1957). *Mgeni karibu*. EALB.

Kahigi, K. & Mulokozi, M.M. (1979). *Kunga za ushairi na diwani yetu*. Tanzania Publishing House.

Kandoro, S. (1972). *Mashairi ya Saadani.* Shirika la Magazeti ya Chama Ltd.

Kandoro, S. (1978). *Ushahidi wa mashairi ya Kiswahili*. Longman.

Katalambula, F. (1965). *Simu ya kifo*. East African Literature Bureau.

Kayamba, M. (1933). *Tulivyoona na tulivyofanya Uingereza*. William Hitchens.

Kenyatta, J. (1966). *Naushangilia mlima Kenya*. East African Publishing House.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. DUP.

Kezilahabi, E. (1999). *Kaptula la Marx*. DUP.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1988). *Kichomi*. East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwa maji*. East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia uwanja wa fujo*. East African Literature Bureau.

FOR ONLINE READING ONLY

Kezilahabi, E. (1978). "Utenzi wa ukombozi wa Zanzibar." *Mulika* Na. 14 uk. 45-51.

Kezilahabi, E. (1978). *Gamba la nyoka*. East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona* Dar es Salaam. DUP.

Kiango S. (1974). *Jeraha la Moyo*. Foundation Books.

Kiimbila J. (1966). *Lila na Fila*. Longman.

Kiimbila, (1972). *Visa vya walimwengu*. Longman.

Kiimbila, J. (1971) *Ubeberu utashindwa*. TUKI.

Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya fasihi simulizi*. Shungwaya.

Kitereza, A. (1980). *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanwalo na Bulihwhali*. TPH.

Komba, S.M. (1978). *Mchakamchaka wa maisha na hadithi nyingine*. Benedictine Publications.

Kuria, H. (1957). *Nakupenda lakini*. East African Literature Bureau & Kampala: Eagle Press.

Lema. E. (1995). *Safari ya Prospa*. E&D.

Lihamba, A. (1985). *Hawala ya fedha*. Tanzania Publishing House.

Liwenga, G. (1978) *Nyota ya huzuni*. Tanzania Publishing House.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Mture Educational Publishers Ltd.

Mapalala, B. (1992). *Kwa heri Iselamagazi*. TPH.

Massamba, D.P.B. (2017). *Historia ya Kiswahili: Mtazamo mpya 100KK hadi 2000BK*. Kiswahili Development Limited.

Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa ushairi na diwani ya Mayoka*. Tanzania Publishing House.

Mbatiah, M. (2000). *Mwendawazimu na hadithi nyingine*. Jomo Kenyatta Foundation.

Mbele, J. (1993). "Mhakiki, uandishi na jamii" katika M.M. Mulokozi (Mh.) *Fasihi, uandishi na uchapishaji*. DUP.

FOR ONLINE READING ONLY

Mbijima, R.J. (2019). *Halahala*. Moccony Printing Press.

Mbijima, R.J. (2019). *Kurunzi*. Moccony Printing Press.

Mbogo, E. (1981). *Tone la mwisho*. DUP.

Mbogo, E. (1988). *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Educational Services Center.

*Mbogo*, E. (2011). *Sundiata*. TUKI.

Mbogo, E. (2015). *Nyerere na safari ya Kanaani*. Vision Strategic Impact Limited.

Mbogo, E. (2015). *Sadaka ya John Okello*. Karjamel Print Technology.

Mbogo, E. (2016). *Malkia Bibi Titi Mohamed*.Vision Strategic Impact Limited.

Mboneko, K. (2004). *Pambazuko gizani*. E&D.

Mbotela, J. (1934). *Uhuru wa watumwa*. Sheldon Press.

Medical Aid Foundation (1995). *Kilio chetu*. TPH.

Mhina, G. (1977). *Mtu ni utu*. Tanzania Publishing House.

Mkangi, K (1984). *Mafuta*. Heinemann.

Mkufya, W. (1999). *Ziraili na Zirani*. Hekima.

Mlaga, W.K. (2017). *Misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi: Karne ya 21*. Heko Publishers Ltd.

Mloka, C. (2002). *Diwani ya Mloka*. Mkuki na Nyota.

Mnyaka, O. (1995). *Kimbia Helena kimbia*. Heko Publishers.

Mnyampala, M. (1963). *Diwani ya Mnyampala*. East African Publishing House.

Mnyampala, M. (1966). *Kisa cha mrina asali na wenzake wawili*: EALB.

Mnyampala, M. (1970). *Ngonjera za UKUTA, kitabu cha kwanza*. Oxford University Press.

Mohamed, M.S. (1978). *Nyota ya Rehema*. Oxford University Press.

Mohamed, M. S. (1972). *Kiu*. EAPH.

Mohamed, S. (1988). *Pungwa*. Longman.

Mohamed, S.A. (1979). *Dunia mti mkavu*. Longhorn Publishers.

FOR ONLINE READING ONLY

Mohamed, S.A. (1983, 2000). *Sikate tamaa*. Longhorn.

Mohamed, S.A. (1986). *Kina cha maisha*. Longman Publisher.

Mohamed, S.A. (1988) *Kiza katika Nuru*. Oxford University Press.

Mohamed, S.A. (1995). *Amezidi*. East African Publishers.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili*. East African Education Publishers.

Mohamed, S.A. (2002). *Sadiki ukipenda na hadithi nyingine*. Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S.A. (2013). *Posa za Bikisiwa*. Sasa Sema Publishers.

Mohamedi, S.A. (1990). *Kivuli kinaishi*. Longman Publisher.

Mohamedi, S.A. (1990). *Tata za Asumini*. Longman Publisher.

Mohammed S. (2001) *Babu alipofufuka*. Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. EPD.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki*. (EAEP).

Mtobwa, B. (1984). *Dimbwi la damu*. Heko Publishers.

Mtobwa, B. (1984). *Pesa zako zinanuka*. Heko Publishers.

Mtobwa, B. (1984). *Zawadi ya ushindi*. East African Ediucational Publishers.

Mtobwa, B. (1985). *Najisikia kuua tena*. Heko Publishers.

Mtobwa, B. (1987). *Tutarudi na roho zetu*. Heko Publishers.

Muhando, (1982). *Nguzo mama*. DUP.

Muhando, P. (1972). *Hatia*. East African Publishing House (EAPH).

Muhando, P. (1973). *Tambueni haki zetu*. TPH.

Muhando, P. & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na sanaa za maonyesho*. Tanzania Publishing House.

Muhando. P. (1975). *Pambo*. Nairobi: Foundation Books.

Muhando. P. (1984). *Lina Ubani*. Dar es Salaam: DUP.

Muhanika, H. (1981). *Njia panda*. Dar es Salaam: DUP.

FOR ONLINE READING ONLY

Mulokozi M. na Kahigi K.K. (1976). *Malenga wa bara.* East African Literature Bureau.

Mulokozi M. na Kahigi K.K (1973). *Mashairi ya kisasa.* TPH.

Mulokozi, M. (1990). *Ngome ya mianzi.* MPB Press.

Mulokozi, M. (1997). *Utenzi wa Nyakiiru Kibi.* ECOL Publications.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili.* KAUTTU.

Mulokozi, M. (Mh.) (1999). *Tenzi tatu za kale.* TUKI.

Mulokozi, M.M. (1991). *Ngoma ya mianzi.* TPH.

Mulokozi, M.M. (1996). *Moto wa mianzi.* ECOL.

Mulokozi, M. na Kahigi K. (1982). *Kunga za ushairi na diwani yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. (1979). *Mukwava wa Uhehe.* DUP.

Mung'ong'o, C. (1977). *Mirathi ya hatari.* Tanzania Publishing House.

Mung'ong'o, C. (1979). *Njozi iliyopotea.* Tanzania Publishing House.

Musiba, A. (1986). *Njama.* Tanzania Publishing House.

Musiba, E. (1980). *Kikomo.* Continental Publishers.

Mutembei, A. (2006). "Nadharia ya fasihi simulizi na maendeleo katika sayansi na teknolojia." katika *Mulika Na. 27.* Uk. 1-17.

Mwakyembe, H. (1981). *Pepo ya mabwege.* Dar es Salaam University Press.

Mwanakupona, M. (1858). *Utenzi wa Mwanakupona.* East African Literature Bureau.

Mwanga, Z. (1983). *Kiu ya haki.* Ruvu Publishers.

Mwengo, A. (1728). *Utenzi wa Tambuka.* (Mswada) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nassir S.A. (1939, 1972). Mh. W. Hitchens. *Utenzi wa Al-Inkishafi.* OUP.

Ndossa, S. na wenzake (2019). *Adili za Nyembe 1: Tungo za Ustadh Mohamed Ally Nyembe (Akhery).* Central Tanganyika Press.

FOR ONLINE READING ONLY

Ngahyoma, N. (1973). *Huka.* Tanzania Publishing House.

Ngomoi J. (1976). *Ndoto ya Ndaria*. TPH.

Ngozi, I. (1977). *Machozi ya mwanamke.* TPH.

Ngugi, G. (1961). *Nimelogwa nisiwe na mpenzi.* East African Literature Bureau.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu.* Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. (1967). *Mzishi wa baba ana radhi.* EALB.

Nkwera, F. (1976). "Fasihi" katika J. P. Mbonde (Mhariri). *Uandishi wa Tanzania: Insha.* EALB.

Nkwera, F. (1978). *Sarufi na fasihi, sekondari na vyuo.* Tanzania Publishing House.

Omari, S. (2009). *Safari ya Chinga.* Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Ponera, A. (2014). *Utangulizi wa nadharia ya fasihi linganishi.* Karljamer Print Technology.

Rajab, H. (1974). *Ufunguo wa bandia.* Eastern Africa Publications.

Rajab, H. (1984). *Roho mkononi.* Busara.

Robert, S. (1948). *Pambo la lugha.* Witwatersrand University Press.

Robert, S. (1952). *Adili na nduguze.* Macmilan.

Robert, S. (1966). *Maisha yangu na baada ya miaka hamsini.* Thomas Nelson and Sons Ltd.

Robert, S. (1967). *Wasifu wa Siti Binti Saad.* Thomas Nelson and Sons Limited.

Robert, S. (1968). *Kufikirika.* Thomas Nelson and Sons Limited.

Robert, S. (1968). *Siku ya Watenzi Wote.* Thomas Nelson and Sons Limited.

Robert, S. (1991). *Kusadikika.* Mkuki na Nyota.

Ruhumbika, G. (1978). *Uwike usiwike kutakucha.* Eastern Africa Publications.

Ruhumbika, G. (1992). *Miradi bubu ya wazalendo.* Tanzania Publishing House.

Ruhumbika, G. (2014). *Wachamungu wa Bibi Kilihona.* E & D.


FOR ONLINE READING ONLY

Saffari A. (1984). *Harusi.* BCI Publishers.

Saffari A. (1976). *Kabwela.* Longman.

Sehoza, S. (1921). *Mwaka katika minyororo.* The Sheldon Press.

Seme, W. (1976). *Njozi za usiku.* Longmans.

Semzaba, E. (1984). *Tendehogo.* TPH.

Semzaba, E. (1988). *Ngoswe penzi kitovu cha uzembe.* DUP.

Semzaba, E. (2008). *Marimba ya Majaliwa.* E & D.

Sengo T.S.Y. na Kiango, S.D. (1973). *Hisi zetu.* TUKI.

Sengo, T., & Kiango, S. (1975). *Hisi zetu 1 & 2.* TUKI.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi na jamii.* Press and Publicity Centre.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi. Nadharia na tahakiki.* Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi.* KAUTTU.

Shafi, A. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuadi.* Tanzania Publishing House.

Shafi, A. (2013). *Mbali na nyumbani.* Longhorn Publishers.

Shakespeare, W. (1964) (J.K. Nyerere, Mf.). *Juliasi Kaisari.* OUP.

Shakespeare, W. (1969) (J.K. Nyerere, Mf.). *Mabepari wa Venisi.* OUP.

Shakespeare, W. (1969) (S.S. Mushi, Mf.). *Tufani.* Tanzania Publishing House.

Simbamwene, J. (1972). *Kwa sababu ya fedha.* Longhorn.

Steere, E. (1870). *Swahili tales.* Bell & Daldy Publisher.

Summers, H. (1989). "Literature" katika *The world book encyclopedia, Juz. 12:351-357.*

Swift, J. (1932). *Safari za Gulliver* (F. Johnson, Mf.). Sheldon Press.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Kiswahili shule za sekondari: Kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano na sita – fasihi.* TET.

Thomas, R. (2011). Taswira ya nyoka katika ngano za Kisambaa, Tasnifu ya umahiri katika Kiswahili, TATAKI, Kikuu cha Dar es Salaam.

FOR ONLINE READING ONLY

Topan, F. (1971). *Mfalme Juha*. OUP.

Topan, F. (1973) na *Aliyeonja Pepo*. TPH.

wa Mberia (2001). *Kifo kisimani*. Marimba Publications.

wa Thiong'o, N. na wa Mirii, N. (1982). *Nitaolewa nikipenda*. EAP.

wa Thiong'o, N. (1970). *Mtawa mweusi*. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Walibora, K. (2007). *Damu nyeusi na hadithi nyingine*. Macmillan.

Walibora, K. (2015). *Nasikia sauti ya mama*. Sasa Sema Publishers.

Wamitila K. (2003). *Kichocheo cha fasihi simulizi na fasihi andishi*. Focus Publications.

Wamitila K. (2010). *Shingo ya mbunge na hadithi nyingine*. Vide-Muwa.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa fasihi: misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publisher.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Focus Publications.

Wamitila, K. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide Muwa Publishers Ltd.

Wellek, R., & Warren, A. (1986). *Theory of literature*. Harmondsworth: Penguin Books.

Zirimu, P. & Gurr, A. Wah. (1973). *Black aesthetics: papers from a colloquium held at the University of Nairobi*. East African Literature Bureau.

FOR ONLINE READING ONLY